# MWEGA WA UJUMI KATIKA NGANO SIMULIZI ZA WACHUKA

**REBECAH WANJA KIRIMI**

**Tasnifu ya Utafiti Iliyowasilishwa Katika Shule ya Mafuzu Kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA 2023**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada au stashahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi____________________ Tarehe 12/10/2023.

Rebecah Wanja Kirimi
AM12/7855/12

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi____________________ Tarehe 12/10/2023

Dkt Allan M. Mugambi
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi____________________ Tarehe 12/10/2023

Dkt. Onesimus Gitonga Ntiba
Chuo Kikuu cha Chuka.

CHUKA UNIVERSITY
13 OCT 2023
DIRECTOR BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES AND RESEARCH
P.O. Box 109-60400 CHUKA

## HATILINZI

©2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu iliyoruhusiwa kutolewa kwa kurudufisha, kunakili, kupiga chapa au kuhifadhi kwa mfumo wowote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

# TABARUKU

Ninatabaruku kazi hii kwa wazazi wangu marehemu Bw. Eustace Gitari na Bi. Annastacia Gitari kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunipa moyo na imani katika kila hatua maishani na katika kipindi chote cha masomo yangu. Aidha, ninaitabaruku kwa mme wangu mpendwa Dkt. Humphrey Kirimi ireri na Wanangu Ezra ireri Kirimi, Gamaliel Muthomi Kirimi na Debra Gatugi Kirimi kwa uvumilivu na upendo wao katika kipindi hicho chote cha masomo yangu.

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa kila kitu kwa kunijalia siha, uwezo, akili, maarifa, busara, uvumilivu na utulivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Pili, ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. Allan Mugambi na Dkt. Onesimus Gitonga Ntiba kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Bila jitihada zao chombo cha utafiti huu kingesombwa na mawimbi. Siku zote, hawakusita wala kuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Ninawashukuru kwa kuwa na imani kwangu kuwa nitamudu utafiti huu. Ninamwomba Maulana awabariki na kuwakirimia siha na baraka, Amin. Tatu, ningependa kuishukuru familia yangu, ndugu na dada zangu kwa kunitia moyo wa kuendelea na masomo yangu. Aidha, ningependa kumshukuru kwa dhati mume wangu mpenzi, Dkt. Humphrey Kirimi, kwa upendo wake, subira, msaada wake wa hali na mali, ushirikiano na ustahamilivu katika kipindi chote cha masomo na utafiti huu. Shukrani za pekee kwa marafiki walionitia moyo kujizatiti mpaka nikaupita utepe wa uzamili. Mwisho, ningependa kuwashukuru wahadhiri Bwana James Ndwiga wa Chuo Kikuu cha Tharaka, Dkt. Mary Kinoti wa Chuo Kikuu cha Chuka, Prof. Kobia na Bw. Matundura kwa kunichochea kutia bidii wakati nilijihisi kulemewa na kunipa wosia niliohitaji. Shughuli hizi za masomo na utafiti wangu zilihusisha watu wengi ambao singeweza kuwataja wote walionifaa. Naomba radhi na kuwashukuru wote walionifaa kwa njia moja au nyingine. Nawaombea baraka na ufanisi maishani.

## IKISIRI

Fasihi simulizi ni zao la jamii ambalo ni nyenzo kuu ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, kuelekeza jamii na kuendeleza lugha kwa jumla. Ngano zimeshughulikiwa katika utafiti wa fasihi simulizi kutoka jamii za Kiafrika. Tafiti zilizofanyiwa kipera hiki cha ngano, zimefanyiwa lugha ya Kimuthambi, Kikuyu, Kitharaka na lahaja nyinginezo. Aidha, tafiti hizo zilijikita katika maudhui, taswira ya mwanamke, mtoto wa kiume na fani. Kadri mtafiti ajuavyo,ngano simulizi za Wachuka hazijashughulikiwa hasa kwa nia ya kubainisha mwega wa ujumi katika ngano hizi. Hali hii ilichochea kuwepo haja ya utafiti huu ulioegemezwa kwenye ujumi katika ngano za Wachuka. Utafiti huu ulishughulikia mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa: Kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka, kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi na kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Utafiti ulitumia mbinu ya kithamano. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma inayotetea upekee wa kiujumi wa kazi za kisanaa. Utafiti huu uliendelezwa nyanjani ambapo mtafiti alikusanya hadithi kutoka kwa magwiji wa usimulizi wa ngano ambao wako katika tarafa ya Chuka.Uteuzi ulizingatia ufahamu na tajriba ya msailiwa kuhusu ngano, umri wa msailiwa, kumbukumbu nzuri ya msailiwa na ulumbi na ukwasi wa lugha wa msailiwa. Wasailiwa watano waliofikia vigezo hivi walihusishwa katika utafiti huu. Jumla ya ngano kumi na tano zilizotambwa na fanani zilishirikishwa kuwakilisha jumuiya lengwa. Kati ya ngano hizo, ngano tano ziliteuliwa kimakusudi kuwakilisha thuluthi moja ya jumuiya lengwa na kuchanganuliwa. Mtafiti alitumia ushiriki kama mbinu ya kukusanya data. Data hii ilihifadhiwa kwenye kanda za kunasia sauti. Baadaye ngano hizi zilifanyiwa unukuzi kwa kutumia kalamu na karatasi. Uchanganuzi wa kimaelezo wa data ulifanywa na kuwasilishwa kwa maandishi ya kinathari. Data iliwasilishwa kupitia maelezo ya kiufafanuzi, mifano na vielelezo. Utafiti huu ulibaini yakuwa mtiririko wa matukio huendeleza ujumi katika ngano za wachuka, pili utafiti huu uligundua kuwa wahusika katika ngano za wachuka hugawika mara mbili yaani mhusika mui ma mwema ili kujenga ujumi katika ngano. Mbinu mbalimbali za lugha zilibainika kuwa mwega wa ujumikwa kuimarisha uhalisia wa matukio na kutimiza dhima na funzo katika Imani za jamii ya wachuka. Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha wanafunzi, walimu na wahakiki wa fasihi simulizi ya Kiafrika, hususani kuhusu suala la ujumi katika ngano na pia uchambuzi wa kazi za fasihi simulizi. Utafiti Zaidi wa ngano simulizi unaojiegemeza kukuza fasihi simulizi ya kiafrika pamoja na ya kisasa inahitajika. Aidha mtafiti alilenga kuweka ngano za Wachuka katika kumbukumbu kupitia kuzihifadhi katika maandishi.

**ABSTRACT**

Oral literature is an important tool in the society that preserves society's traditions and enhances language use. Studies on aesthetism in various genres of oral literature are mostly based on themes, characterization and the role of women in the society. The study of aesthetism in gichuka oral naratives has received scanty attention. This study sought to address the core of aesthetisism in Gichuka narratives. The objectives of the study are: to investigate how plot is developed aesthetically in formation of Wachuka folk tales, discuss how characterization is developed aestheticaly and analyse how the stylitic devices are used to develop aesthetism in Wachuka Folk tales. This study is based on the Emic Theory by Del Hymes. It utilized qualitative research design and employed an observation schedule as a data collection method. Ten folktales were selected purposively from those narrated based on characters and themes but only five narratives were analyzed because the saturation point was reached. Five informants who were able to narrate Gichuka folktales were used. The selection of the informants was based on the informant's knowledge, experience of the informant, age of the informant, ability of the informant to remember and capability of the informant to narrating folktales. Data collected was analysed and presented in descriptive method. The study establishes that the formation of Wachuka folk tales develops the plot aesthetically. It also finds out that characterization in Wachuka folktales splits into the protagonist and antagonist and thus enhances aestheticism in the narratives. Finally, the study further establishes that various stylitic devices are used to develop aesthetism in Wachuka Folk tales by enhancing realism and the roles of Wachuka belief systems. The findings of this study are expected to contribute to the scholary literature in narratives which traverses different fields of language study. It is expected that the study will help literary critics and social- linguists to understand the place of aesthetics and their role in Gichuka narratives. The results of this study may enable the preservation of Gichuka folktales as an important genre of oral literature.

# YALIYOMO

UKURASA


**UNGAMO NA IDHINI** ........................................................ **ii**

**HATILINZI** ........................................................ **iii**

**TABARUKU** ........................................................ **iv**

**SHUKRANI** ........................................................ **v**

**IKISIRI** ........................................................ **vi**

**ABSTRACT** ........................................................ **vii**

**YALIYOMO** ........................................................ **viii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ........................................................ **1**

1.1 Usuli wa Mada ........................................................ **1**

1.2 Suala la Utafiti ........................................................ **2**

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........................................................ 2

1.4 Maswali ya Utafiti ........................................................ 3

1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada ........................................................ 3

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................ 3

1.7 Upeo wa Utafiti ........................................................ 4

1.8 Maelezo ya Istilahi ........................................................ 5

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** ........................................................ **6**

2.1 Utangulizi ........................................................ 6

2.2 Jamii ya Wachuka na fasihi simulizi yao. ........................................................ 6

2.3 Utafiti wa Fasihi Simulizi ........................................................ 7

2.4 Utafiti katika Suala la Ujumi ........................................................ 9

2.5 Kipera Cha Ngano ........................................................ 12

2.6 Lugha ya Kisimulizi na Mguso ........................................................ 13

2.7 Tamathali za Usemi ........................................................ 15

2.8 Wahusika wa Kisimulizi ........................................................ 18

2.9 Misingi ya Nadharia ........................................................ 20

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** ........................................................ **23**

3.1 Utangulizi ........................................................ 23

3.2 Mbinu za Utafiti ........................................................................................23
3.3 Utafiti Awali..................................................................................................23
3.4 Eneo la Utafiti. ..............................................................................................23
3.5 Kundi Lengwa ...............................................................................................23
3.6 Uteuzi wa Sampuli ........................................................................................24
3.7 Vifaa vya Utafiti............................................................................................24
3.8 Hatua za Ukusanyaji wa Data. .......................................................................25
3.9 Uchanganuzi wa Data....................................................................................25
3.10 Maadili ya Utafiti .........................................................................................26

**SURA YA NNE: MTIRIRIKO WA MATUKIO KATIKA NGANO SIMULIZI ZA WACHUKA** .....................................................27
4.1 Utangulizi .......................................................................................................27
4.2 Mtiriko wa matukio katika Hadithi ya Fisi na Kindi .......................................27
4.2.1 Muhtasari wa Hadithi ya Fisi Na Kindi.....................................................27
4.2.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi ................................................................28
4.3 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya Ngongoana na Gacinci ......................30
4.3.1 Muhtasari wa Hadithi ...................................................................................30
4.3.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi ................................................................31
4.4 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya Wasichana Wanne wa Ikamba ..........33
4.4.1 Muhtasari wa Hadithi ...................................................................................33
4.4.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi ................................................................34
4.5 Muhtasari wa hadithi ya Chura na Mbuni .......................................................40
4.5.1 Mpangilio wa Matukio Kiujumi ................................................................41
4.5.2 Muhtasari wa Hadithi ...................................................................................43
4.5.3 Mpangilio wa Matukio Kiujumi ................................................................44

**SURA YA TANO: SIFA ZA WAHUSIKA WA KISIMULIZI KATIKA NGANO ZA WACHUKA** .......................................................47
5.1 Utangulizi .......................................................................................................47
5.2 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Fisi ya Kindi .....................47
5.2.1 Wahusika Wawi..........................................................................................47
5.2.2 Wahusika Wema..........................................................................................50
5.3 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Ngongoana na Gacinci .....51

5.3.1 Wahusika Wawi ........ 51
5.3.2 Wahusika Wema ........ 52
5.4 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Wasichana Wanne wa Ukambani ........ 54
5.4.1 Wahusika Wawi ........ 54
5.4.2 Wahusika Wema ........ 56
5.5 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi katika Hadithi ya Chura na Mbuni ........ 58
5.5.1 Wahusika Wawi ........ 59
5.5.2 Wahusika Wema ........ 60
5.6 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Fisi na Ndovu ........ 60
5.6.1 Wahusika Wawi ........ 60
5.6.2 Wahusika Wema ........ 61

**SURA YA SITA: MBINU ZA KIMTINDO KATIKA NGANO ZA WACHUKA ........ 63**
6.1 Utangulizi ........ 63
6.2 Mbinu za Kimtindo ........ 63
6.2.1 Mbinu za Kisanaa ........ 63
6.2.1.1 Nyimbo ........ 64
6.2.1.2 Taswira ........ 71
6.2.1.3 Dayalojia ........ 74
6.3 Mbinu za Lugha ........ 79
6.3.1 Takriri ........ 79
6.3.2 Chuku ........ 83

**SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 86**
7.1 Utangulizi ........ 86
7.2 Muhtasari ........ 86
7.3 Hitimisho ........ 88
7.4 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye ........ 89

**MAREJELEO ........ 91**
**VIAMBATISHO ........ 95**
Kiambatisho I: Ngano za Wachuka Kutoka kwa Watambaji ........ 95

Kiambatisho II: Barua ya Utangulizi ........................................................ 112
Kiambatisho III: Barua ya Idhini ya Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka ........................................................ 113
Kiambatisho IV: Idhini ya Utafiti ........................................................ 114

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Ujumi ni tawi la falsafa linaloshughulika na uzuri, ubaya na ladha. Ujumi ni elimu ya sheria na kanuni za Sanaa, (Simala, 2006). Dhana ya ujumi ilitoka kwenye nadharia ya hisia za akili katika karne ya 18 na kuitwa “Falsafa ya uzuri” au “Falsafa ya sanaa” au yote mawili kwa pamoja. Uzuri ni ukamilifu wa hisia za akili unaosababisha kulitazama jambo au mambo fulani katika mtazamo chanya kwani mwingine anaweza kulichukulia jambo hilo kimtazamo hasi lakini mtazamo wake hauondoi uzuri wa chanya kwa atazamaye chanya. Uhakiki wa ujumi ni dhana ya kijumla inayotumiwa kueleza mkabala wa kuhakiki kazi ya kifasihi ambao huchunguza kazi hiyo kwa kuangalia uhusiano kati ya sehemu mbalimbali zinazounda kazi hiyo. Aidha vipengele vya ujumi vina uamili mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi kwa hadhira yake.

Matumizi mazuri ya vipengele vya ujumi huufanya muundo wa kazi ya fasihi kuvutia hadhira lengwa. Kwa upande mwingine, kutomakinika kwa mtunzi katika matumizi ya ujumi huifanya kazi ya kifasihi kutokuwa na umbo zuri. Matokeo yake ni kuwa kazi ya kisanaa hukosa mshikamano na mwingiliano unaotarajiwa. Matini ya aina hiyo huwa haina uwezo wa kuvutia hadhira (Harmon & Holman, 2000; Hegel, 1979). Katika utafiti huu kanuni na sheria za sanaa ndizo kitovu cha kubainisha namna zilivyozingatiwa katika ujenzi wa ngano simulizi za Wachuka. Fasihi simulizi ni zao la jamii. Kulingana na Mathooko (2006), fasihi simulizi huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika. Fasihi hushughulikia masuala yanayoikumba jamii mojawapo ikiwa ni usawiri wa wahusika kama vile wahusika wa kiume, wahusika wa kike, wahusika wanyama na pia wahusika mazimwi. Ngano ni utanzu wa fasihi simulizi na ni hadithi fupi ambazo wazee huwasimulia aghalabu watoto.

Ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni pamoja na njia anazotumia kukabiliana na matatizo hayo. Dhamira kuu ya ngano nyingi ni kudhihirisha jinsi binadamu alivyo na uwezo wa kuyamudu matatizo yake pindi atumiapo akili yake vizuri. Kwa njia hii anaboresha maisha yake na kuishi raha mstarehe. Ngano huwa na aina mbalimbali ya wahusika

ikiwa ni pamoja na mazimwi, wanyama na binadamu. Inafahamika kwamba kuna aina mbalimbali za ngano kama vile ngano za mazimwi, ngano za usuli, hurafa, hekaya na mighani (Njogu & Chimera, 1999)

Fasihi imeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa katika jamii mbalimbali nchini Kenya.Tafiti kadha zimefanywa hapa nchini Kenya hasa kuhusu ngano za jamii mbalimbali. Kwa mfano, Mutegi (2014) alishughulikia suala la taswira ya mwanamke katika ngano za kimuthambi. Kadhalika, Oyoyo (2013) alichunguza fani katika ngano teule za Waswahili. Ngole na Henero (2006), wamefanya utafiti wa ngano katika Jamii ya Wasukuma nchini Tanzania. Timammy (1990), amehakiki hadithi za jamii ya Waswahili. Kwa upande mwingine, Mghanga (1984) alichambua maudhui katika ngano tano za Kidawida. Pia, ngano za jamii nyingine kama vile Kitharaka iliyotafitiwa na Mitambo (2018), kuhusu taswira ya mtoto wa kiume katika ngano za Kitharaka. Katika tafiti hizi zote ingawa zina umuhimu katika maendeleo ya ngano simulizi hazikushughulikia ngano katika mkabala wa ujumi wala hazikuhusisha nadharia za ujumi. Utafiti huu ulikuwa wa kipekee na tofauti na tafiti za awali kwa kushughulikia ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

### 1.2 Suala la Utafiti

Fasihi simulizi hushughulikia masuala mbalimbali ya kijamii. Ngano ni mojawapo wa utanzu muhimu katika fasihi simulizi. Ngano zimeshughulikiwa katika utafiti wa fasihi simulizi kutoka jamii za Kiafrika. Tafiti zilizofanyiwa kipera hiki cha ngano, zimefanyiwa ngano za jamii ya Kimuthambi, Kikuyu, Kitharaka na jamii nyinginezo. Aidha, tafiti hizo zilijikita katika maudhui, taswira ya mwanamke, mtoto wa kiume na fani. Ngano simulizi za Wachuka hazijashughulikiwa hasa kwa nia ya kubainisha mwega wa ujumi katika ngano hizi. utafiti huu uliegemea kuchunguza na kubainisha mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka ili kuonyesha ufasaha wake kisanaa na kiufundi uliofikiwa katika utunzi na uwasilihaji wake kiujumi.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka.

ii. Kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka.
iii. Kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utajibu maswali yafuatayo:

i. Mtiririko wa matukio unaendelezwaje kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka?
ii. Je, Sifa za wahusika wa kisimulizi zimeendelezwa vipi katika ngano simulizi za Wachuka?
iii. Je, mbinu za kimtindo zimetumika vipi kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka?

### 1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada

Utafiti huu ulichochewa na haja ya kutaka kuchunguza ujumi katika ngano za Kichuka.. Tatizo la utafiti huu ni kubainisha dhima ya ujumi katika ngano simulizi za Kichuka kama mojawapo wa kipengee cha kuzipa ngano hizo umbo kamili. Mtafiti amechagua mada hii kwa sababu ngano huchukua nafasi kubwa katika kukuza, kueneza na kuhifadhi kunga nyinginezo za fasihi simulizi kwa kuzijumuisha katika muundo wake. Hivyo basi, utafiti unaolenga ngano utakuwa umeshughulikia mawanda mapana ya fasihi simulizi kitanzu, jambo linalomchochea mtafiti.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa mchango kwa maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa fasihi unaoingiliana na nyanja zingine mbalimbali za lugha. Utafiti huu ulikuwa wa muhimu katika kufanikisha uhifadhi wa ngano simulizi za Wachuka kama kipera muhimu cha fasihi simulizi ya kiafrika na fasihi kwa jumla. Vilevile, ulichangia pakubwa katika kukuza hadhi ya ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika. Utafiti huu ulikuwa nyenzo ya kuhifadhi utamaduni, mila na desturi ya Wachuka kama jamii mahususi.

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Fasihi simulizi ya Kiafrika ni pana sana na haiwezi kushughulikiwa katika utafiti huu. Makabila yanayounda jamii pana ya Wameru ni mengi, Chuka ikiwa mojawapo na hayawezi kushughulikiwa katika kazi hii kwa pamoja. Utafiti huu ulifanyiwa katika jamii ya Wachuka iliyo katika kaunti ya Tharaka-Nithi. Utafiti ulijikita katika eneo bunge la Chuka Igambang`ombe. Sababu ya kuchaguliwa eneo bunge ndogo hili ni kuwa, wanajamii wengi wenye lugha na utamaduni asilia wa Gichuka hupatikana katika eneo hili.

Kipera cha ngano pekee ndicho kilichozingatiwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu kipera hiki hakijafanyiwa utafiti wa kina hasa katika jamii ya Wachuka. Ngano za aina nyingi ikiwa ni pamoja na zile za mazimwi, hurafa, mighani na hekaya zililengwa. Utafiti huu ulichunguza aina hizi zote za ngano mradi tu ziweze kuonyesha ujumi katika ngano za wachuka. Masimulizi ya fanani waliosifika katika jamii ya Wachuka yalizingatiwa. Wasailiwa watano waliteuliwa kupitia sampuli maksudi. Utafiti huu ulishughulikia ngano kumi na tano za Wachuka ambazo zilikuwa zinadhihirisha sifa za kiujumi.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi

**Gichuka**: Gichuka ni lahaja mojawapo kati ya lahaja nane za Kimeru

**Jamii**: Ni kundi la watu maalumu linalotambulikana kwa kuishi pamoja na pia kutumia lugha moja na kuwa na mila na desturi zinazofanana.

**Kipera**: Ni mgawanyiko wa kimakundi yenye uhusiano katika matawi ya fasihi. Kwa mfano ngano ni kipera kimoja cha hadithi.

**Mwega**: Neno hili litatumiwa kumaanisha, nguzo au misingi ya kitu au vipengele vya kazi ya kisanaa.

**Ngano simulizi**: Ni masimulizi ya kinathari ambayo huwa yamebuniwa au yenye uhalisia kuhusu matukio mbalimbali katika jamii.

**Ujumi:** Neno hili litatumiwa kurejelea ladha tamu au chungu ya kazi ya fasihi. Ujumi ndio unaomfanya msomaji kuisoma, si mara moja wala mbili, bali kila akimaliza, hupenda aisome tena na tena kazi ya fasihi.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia mapitio ya maandishi yanayohusiana na utafiti Jamii ya Wachuka na Fasihi Simulizi yao, utafiti wa Fasihi Simulizi, utafiti katika Suala la Ujumi, Kipera Cha Ngano, lugha ya kisimulizi na mgusotamathali za usemi, wahusika wa kisimulizi. Vilevile ilijumuisha misingi ya nadharia katika sehemu hii.

## 2.2 Jamii ya Wachuka

Kichuka ni lahaja mojawapo kati ya lahaja nane za Kimeru, Mbaabu (1978) anasema kuwa Jamii ya Wameru imeundwa na makundi yafuatayo; Wachuka, Waimenti, Wamuthambi, Wamwimbi, Watigania, Waigoji, Waigembe, na Watharaka. Kuna mwingiliano mkubwa wa kitamaduni kati ya jamii hizi zote za Wameru.Mila na desturi za jamii zote zinashabihiana kwa kiasi kikubwa katika makundi yote manane. Kichuka ni lugha ya jamii ya Wachuka. Jamii ya Wachuka hupatikana katika nyanda za chini, kusini mashariki mwa mlima Kenya. Aghalabu huwa na mipaka yake baina ya Mto Thuci katika upande wa kusini na mto Nithi upande wa kaskazini. Kwa mujibu wa lamani ya lugha ya Guthrie (2009), Gichuka huwa na kodi ya Guthrie E 541. Kwa sasa baada ya katiba mpya (2010) jamii ya Wachuka hupatikana katika eneo la Chuka katika kaunti ya Tharaka Nithi.

Miongoni mwa mitindo iliyotumika kupitisha elimu miongoni mwa jamii ya wachuka, ilikuwa kupitia kwa utambaji ngano. Kupitia kwa ngano, masuala mbalimbali yalipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Masuala yaliyokashifiwa ama kuenziwa yalifafanuliwa kupitia kwa ngano (M’Imanyara, 1992). Kwa mujibu wa Mumbere (2003), tamaduni na njia za maisha za wachuka hutumia usimulizi kudumisha ujima na mapokezano ya utamaduni kwa vizazi vya usoni. Baadhi ya simulizi hizi ni pamoja na nyimbo, ngano, methali, vitendawili na sanaa za maonyesho. Utafiti huu ulinuia kuchunguza jinsi mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka ulivyoendelezwa katika ufumaji wa ngano husika, wahusika na mbinu za kimtindo.

## 2.3 Utafiti wa Fasihi Simulizi

Mulokozi (1983) anasema kuwa utafiti, uainishaji na uchanganuzi wa fasihi simulizi ulimwenguni unaongozwa na mtazamo wa Kiaristotle unaoweka mipaka bayana kati ya tanzu. Mtazamo huu pia unatumiwa katika utafiti kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika. Kuanzia miaka ya sabini, utafiti wa kina zaidi kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika ulianza kushuhudiwa. Kimsingi, kuwepo kwa tafiti hizi ni muhimu katika kuweka msingi na kiini cha utafiti wa nyanjani katika fasihi simulizi. Utafiti huu ni sehemu ya mkufu huo katika maendeleo ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Hata hivyo, suala la ujumi katika ngano simulizi za Wachuka halijachunguzwa kitaaluma na kubainisha vipengele vyake. Huo ulikuwa wajibu wa utafiti huu katika kuchunguza mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

Utafiti wa Matti (1993) uliohusu tohara miongoni mwa Watharaka, kama mfano wa sanaa ya maonyesho. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya utendaji. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kuthibitisha kuwa, sanaa za maonyesho za jadi zilikuwa na sifa kamili za kidrama. Utafiti wake ulipambanua kuwa, sherehe za tohara miongoni mwa Watharaka hupangwa na kutendwa katika mfumo wa kidrama. Kupitia kwa mfumo huo wa kidrama, Watharaka waliweza kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wao kupitia utendaji wa mara kwa mara. Ingawa utanzu ulioshughulikiwa katika utafiti wake ulifanyiwa fasihi simulizi ya Watharaka iliyo karibu sana na jamii ya Wachuka. Hata hivyo, mtafiti huyu hakuwa na nia ya kubainisha ujumi katika tanzu za fasihi simulizi. Utafiti huu basi ni tofauti na wake kwa kuwa uliegemea ngano mbali na kushughulikia ujumi katika kazi za fasihi simulizi za wachuka.

Usawiri wa mwanamke miongoni mwa Waswahili na Wakikuyu kupitia kwa methali kwa kuongozwa na nadharia ya mtazamo-kike ni utafiti uliofanywa na Ndungo (1997). Utafiti huu ulibainisha kwamba, katika jamii hizi mbili, methali hutumiwa kuwasawiri wanawake kama viumbe duni wakilinganishwa na wanaume. Kutokana na utafiti wake, mtafiti huyu alipata kuwa, jamiii hizi mbili zilimsawiri mwanamke kwa namna inayofanana kupitia kwa methali zao. Kwa ujumla, utafiti wa Ndungo ulidadavua kuwa, fasihi simulizi ni chombo muhimu kinachotumiwa na jamii husika kuhifadhi mila na desturi zake, hususan kuhusu nafasi ya mwanamke. Ingawa utafiti wake ulilenga utanzu wa semi ulio tofauti na utanzu wa ngano unaoshughulikiwa katika utafiti huu,

unamchochea mtafiti kuepuka kushughulikia maudhui katika utafiti wa tanzu nyingine za fasihi simulizi kwa kuwa umeshughulikiwa sana; amechagua kipengee cha ujumi ambacho hakijachunguzwa katika ngano simulizi za kichuka. Hali hii inabaini upya wa mada ya utafiti huu ili kujaza mwanya ulioachwa na watafiti hawa wa awali.

Alembi (2002) alitafiti kuhusu mitazamo ya Wanyore kuhusu kifo kwa kutumia maghani ya maziko. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa Wanyore hueleza masuala kama vile asili, kiini na maana ya kifo kupitia kwa maghani ambayo hutolewa na wanajamii wakati wa kuomboleza. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma katika kuchanganua namna maghani ya maziko hutelekeleza wajibu wake katika utendaji. Jambo hili litakuwa muhimu kwa utafiti huu, kwani uchanganuzi wa ujumi katika ngano za Wachuka utajumuisha mihimili ya ujumi wa Kinudhuma. Hata hivyo, Alembi hakushughulikia kipera cha ngano wala kuainisha vipengele vya ujumi ambalo ndilo suala la utafiti huu.

Ndege (2003) alitafitia ngano za Wameru kwa kubainisha kwamba, ngano hizo huwa na muundo maalum ambao huzisaidia kutekeleza wajibu wake barabara, wakati wa utendaji.  Ndege (2003) alichambua ngano za Wameru kwa kuongozwa na nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma. Uchambuzi wake utafaa sana utafiti huu, kwani nadharia hiyo ya Ujumi wa Kinudhuma imetumiwa katika kupambanua ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Seitei (1980), aliweza kudhihirisha kuwa, ngano zenyewe hupata uamilifu wake kutokana na hali halisi ya utendaji Hata hivyo, Seitei na Ndege hawakunuia kudadavua namna ngano hizo za kijadi hudhihirisha ujumi wa kisimulizi. Utafiti huu ulikuwa na wajibu wa kufanya hivyo.

Ndimofor (2011) alifanya utafiti kuhusu nyimbo za kitamaduni za Waakum na kudhihirisha kuwa, nyimbo hizo hubeba maudhui mazito kuhusu utamaduni wa jamii husika. Matokeo ya utafiti wake, yalibainisha nafasi muhimu ya fasihi simulizi katika kuhifadhi mila na desturi za jamii husika. Ingawa utafiti wake hauna uhusiano wa moja kwa moja na utafiti huu, utafiti wake ni wa muhimu katika kuchochea utafiti unaogemea tanzu nyingine za fasihi simulizi zaidi ya nyimbo. Kwa msingi huu utafiti huu uliegemea utanzu wa ngano katika jamii ya Wachuka na kwa mkabala wa ujumi.

## 2.4 Utafiti katika Suala la Ujumi

Immanuel Kant (1790) ni mwanafalsafa aliye na mchango mkubwa sana katika ujumi na nadharia ya ujumi kwa jumla. Kwanza, ni mwanafalsafa aliyeandika vitabu muhimu vihusuvyo ujumi na tahakiki ya maamuzi. Kitabu kimojawapo ni kile kiitwacho „Kritik der Urteilskraft. (Critique of judgement/ Tahakiki ya maamuzi). Kitabu hiki kilitolewa mwaka 1790, na ndicho pekee kilichoeleza maamuzi ya ujumi kwa mawanda mapana zaidi. Kinajadili kwa undani kuhusu maamuzi ya kiujumi. Kant anaona kuwa maamuzi ya kiujumi yanatokana na utambuzi wa hisi utashi wa asili katika mtu binafsi.

Kant katika Hammermeister (2002) anasema kuwa uamuzi wa ladha au uzuri umo katika kanuni za kiupendeleo; na uamuzi huo una uhalisi wa kijumla. Kanuni za mapendeleo huamua kitu kipi kinatufurahisha na kipi hakitufurahishi kwa kupitia tu katika hisi au mawazo. Kwa hiyo, kanuni hizi hutokana na uwezo au uhuru uliomo katika ala zetu na utambuzi ambao huleta uelewa sawa kwa kila mmoja aliye na uwezo wa utambuzi. Hivyo basi, uamuzi wa kiujumi, kwa namna moja, una kanuni za kimapendeleo na ukubalifu wa kijumla.

Katika kuielezea dhana halisi ya uzuri katika uamuzi, Kant ametoa mitazamo minne tofauti inayodokeza namna uzuri unavyoweza kujitokeza. Mitazamo hiyo ni hii ifuatayo:

i. Ladha ni ustadi wa kukisia kitu au namna ya uwasilishaji kwa kupendeza sana au kuchukiza sana, mbali na namna yoyote ya upendeleo. Hali hii ya upendeleo ndiyo huitwa uzuri.
ii. Kitu kizuri ni kile kinachofurahisha au kupendeza wengi bila wazo au fikra zinazohususiana na kitu hicho. Katika dhana hii, Kant anaona kuwa kitu chaweza kuwa kizuri iwapo kinawafurahisha watu wengi, pasipo kufikiria maana na sababu za watu hawa kupenda kitu hicho. Kutokana na kanuni hiyo, uzuri na ubaya wa kitu hutokana na kukubalika kwa watu wengi walio na idili zinazokubaliana na maisha yao ya kila siku. Uzuri wa maumbo ya akina mama au rangi nyeupe ya wanawake, kwa mfano, ni baadhi ya uzuri unaotokana na idili za jamii. Uzuri au ubaya unaokubalika katika jamii moja waweza kuwa si uzuri au ubaya kwa jamii nyingine, Pia uzuri au ubaya wa kitu katika kipindi fulani, cha wakati chaweza kuwa si kizuri au kibaya katika kipindi kingine.

Uzuri wa kitu huendana na idili, mabadiliko pamoja na maendeleo ya jamii kihistoria.

iii. Uzuri ni ule unaotokana na lengo au kusudi la kitu hicho. Socrates (470 –469 BC) anaona kuwa, kitu chaweza kuwa kizuri kutokana na kazi kinachopaswa kuifanya. Kwa mfano, jembe linaweza kuwa zuri kutokana na kutumika katika kilimo; lisipokuwa na matumizi hayo ya kilimo, jembe hilo halina maana, kwa hiyo si zuri. Hivyo basi, jembe ni zuri kwa kilimo, lakini si zuri kwa kufyekea miti kwa vile halikutengenezwa kwa ajili hiyo. Makusudi ya kutengeneza kitu hukifanya kitu hicho kuwa kizuri au kibaya kutegemea na mahitaji ya jamii husika.

iv. Mbali na fikra au wazo, uzuri hutawaliwa na kanuni mahususi za kiujumi. Kutokana na dhana hii, ubaya au uzuri hujigeza katika mazingira mahususi yanayotawala maamuzi yake. Kwa mfano, uzuri katika jamii moja unaweza kuwa si uzuri katika jamii nyingine kutokana na kutofautiana kwa kanuni za jumla zinazolazimisha jamii kuutambua uzuri au ubaya huo. Uzuri lazima uguse idili za jamii husika.

Pamoja na mitazamo iliyotajwa hapo juu, bado Kant anaueleza utata wa kupata maamuzi ya kiujumi kwa vile watu hutofautiana katika kuuona uzuri au ubaya. Kitu kizuri au kibaya kwa mtu mmoja kinaweza kuwa si kizuri au kibaya kwa mtu mwingine kutokana na kutofautiana kwa hisi, ufahamu na akili. Kwa hivyo, kitu kizuri au kibaya ni lazima kiguse au kisiguse idili za wote na kujigeza au kutojigeza katika utumizi, na kubainisha au kutobanisha ukweli na uhalisi wa kitu chenyewe. Anasema kuwa Maamuzi ya thamani ya kiujumi hutegemea uwezo wetu wa upambanuzi katika kiwango cha utambuzi.

Kutokana na maelezo hayo hapo juu, tunaweza kuona kuwa upo utata mkubwa katika uamuzi wa kiujumi, na kwamba, uhusiano kati ya uhalisi na uidili ni vitu muhimu sana katika uamuzi huo. Mtu binafsi hubebwa na idili za jamii yake katika kuamua kitu fulani ni kizuri au si kizuri. Mara nyingi, mtu huamua kuwa kitu Fulani ni kizuri au kibaya kutokana na umuhimu wa kimatumizi wa kitu hicho. Aidha, ulinganifu wa utumizi huo wa kitu katika muundo wake ndio ujengao uidili wa kitu hicho. Mawazo

yake kant yatafaa sana katika uchanganuzi wa data kwani itatusaidia katika kubainisha ujumi katika ngano teule za gichuka.

Wapo watafiti mbalimbali walioweza kufanya utafiti kuhusu ujumi katika Fasihi, ingawa hawakufanya katika ngano za wachuka. Khamisi (1981) katika kazi yake ya "The Aethetics idiom of Mohamed Suleiman.s writings" anaangalia ujumi kwa ujumla, hususani, vipengele vya sifa na matumizi ya simo katika kazi za Mohamed Suleiman. Hata hivyo, mtafiti alijigeza katika uga wa kiisimu, licha ya kwamba data alizozitumia amezichota katika kazi za Fasihi. Kazi yake ilikuwa na mchngo kwa utafiti huu hasa katika mwauo wa maandishi.

Ziada (2011) katika tasnifu yake ya ujumi wa kisanaa katika mtindo wa Riwaya teule za M. S. Abdulla, ameweza kuhakiki kazi teule za Fasihi za mwandishi huyo kiujumi, hasa ujumi wa kisanaa. Hata hivyo, kipengele alichofanyia utafiti ni miongoni mwa vipengele vya Fasihi Siyo ngano.kwa hivyo, hata kama kazi hii ina mchango kwa utafiti huu kwani ni ya kiujumi lakini zinatofautiana kwani utafiti huu unalenga fasihi simulizi bali sio andishi.

Kiganza (2011) katika tasnifu yake ya „Ujumi katika Mashairi ya Mathias Mnyampala., ameangalia vipengele vikuu vya kiujumi vinavyojitokeza katika mashairi ya Mathias Mnyapala. Pamoja na kuwa kazi alizozichunguza ni miongoni mwa kazi za kifasihi zilizofanywa na mwanafasihi, bado tunaona kuna pengo, kwani aliangalia moja ya tanzu za Fasihi andishi na siyo kipera cha ngano.

Sanga (2012) katika tasnifu yake ya 'Ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili ': Mifano kutoka Riwaya za Muhammed Said Abdulla na Elvis Aristablus Musiba., amechambua riwaya pendwa za Kiswahili za Aristabus Elvis Musiba na Muhammed Said Abdulla kwa kutumia taaluma ya ujumi. Japokuwa kazi alizozichunguza ni miongoni mwa kazi za Fasihi zilizofanywa na mwanafasihi, bado hakushughulikia kipengele cha ujumi wa Kichuka katika ngano.

## 2.5 Kipera Cha Ngano

Wataalam mbalimbali wametoa maelezo kuhusu maana ya ngano. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), ngano ni hadithi fupi ambazo wazee huwasimulia aghalabu watoto. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni pamoja na njia anazotumia kukabiliana na matatizo hayo. Dhamira kuu ya ngano nyingi ni kudhihirisha jinsi binadamu alivyo na uwezo wa kuyamudu matatizo yake pindi atumiapo akili yake vizuri. Kwa njia hii anaboresha maisha yake na kuishi vizuri. Pia wanaeleza kuwa ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni. Maelezo haya yanaingiliana sana na sifa za ngano simulizi za Kichuka kwa hivyo yalifaa sana katika utafiti huu. Kwani ilibainika kuwa ngano za wachuka zilizotafitiwa ni hadithi zinazotoa mifano mingi maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni pamoja na njia anazotumia kukabiliana na matatizo hayo.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo huwatumia wahusika wa aina mbalimbali wakiwemo wanyama, miti au watu Kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo. Anaendelea kueleza kuwa neno ‘ngano’ hutumiwa katika jamii zetu kwa maana pana kiasi kwamba aina nyingine ya simulizi au hadithi zinaweza kujumlishwa kwenye kundi pana la ngano.

Hadithi hizi zimegawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni la zile hadithi ambazo hujengwa katika misingi ya ubunifu au kuwaza na kufikiria kisa fulani. Ubunifu huu ni wa kijamii, yaani kisa fulani kinatungwa na kupokezwana. Hizi huitwa hadithi za kibunifu. Mifano ni hekaya, hurafa, istiara, mbazi na kadhalika. Kundi la pili la hadithi ni zile zenye misingi yake katika matukio ya kihistoria, yawe ya kikweli yaliyotendeka au la. Utafiti huu ulijishughulisha zaidi na kundi la kwanza la hadithi, yaani hadithi za mapokeo na za kibunifu.

Ngure (2007) anasema kuwa kuna tamaduni tatu za fasihi kutoka Afrika. Kwanza ni ule utamaduni wa fasihi simulizi au fasihi ya kutoka kinywani hadi sikioni ambayo huwa inapitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Utamaduni huu hujumuisha nyimbo, mashairi, drama, methali, mafumbo, misemo na ndiyo turathi iliyo kongwe na tajiri

kuliko zote. Mbali na hayo imejaa uhai na uchangamano ambao hutegemea wakati na muktadha.

Hii inamaanisha kuwa, ngano zina vipengele mbali mbali katika kustawishwa kwake. Kipengele mojawapo kikiwa ni usimulizi ambao unaonekana kuwa na mabadiliko kulingana na wakati kile anachoita muktadha. Hii inamaaanisha kuwa ngano husimuliwa mahali maalum na wakati maalum. Watoto, vijana na watu wazima katika jamii ya jadi na hata ya sasa walifunzwa utamaduni wao pamoja na uhalisi wa maisha yao kwa njia ya masimulizi. Jamii nzima ilihusika katika kuwafunza na kuwaelekeza vijana wake. Mambo haya yalitekelezwa kupitia kwa hadithi, nyimbo, methali, vitendawili na tanzu nyingine za fasihi simulizi

M’ Ngaruthi (2008) anaeleza ngano kama masimulizi ya hadithi za kimapokeo ambazo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa minanjili ya mabadiliko ya kila uchao tunapata kuwa usimulizi wa ngano umechukua mtindo mpya. Kwa mfano siku hizi masimulizi ya ngano yanajumuishwa katika redio na televisheni na pia katika michezo ya kuigiza katika shule na vyuo. Hali hii inaashiria namna utanzu wa ngano unavyozidi kukua na kuimarika kimtindo. Matumizi yake yamepanuka na hata ngano zenyewe kuwa na thamani kubwa. Kutokana na mawazo hayo ni wazi kuwa pana haja ya kuchunguza ngano simulizi za kichuka.

M’Ngaruthi (kasha tajwa) anaendelea kusema kuwa hadithi ni kisa au matukio halisi au zilizobuniwa. Hadithi hizi za kimapokeo hujulikana kama ngano. Anaendelea kueleza kuwa baadhi ya ngano hizi zimebadilika kiasi kwamba zinaposimuliwa na wasimulizi tofauti husikika kama ngano tofauti. Baadhi ya wasimulizi wataondoa au kuongeza mambo fulani katika hadithi wasimuliapo ama kwa kutaka kuongeza chumvi au kutokana na usahaulifu wa baadhi ya sehemu za hadithi asilia. Bila shaka hii ndiyo huchangia kwa urefu au ufupi wa vitanzu vya hadithi.

## 2.6 Lugha ya Kisimulizi na Mguso

Lugha inayotumika katika kazi ya fasihi inapendeza, inavutia na kulazamisha msomaji kuitafakari zaidi. Maana hii ya fasihi ndiyo iliyotolewa na wanamuundo Wakirusi kama Pia kwa mujibu wa wanamuundo, kitu kinachotofautisha lugha ya fasihi na lugha

nyingine ni uwezo wa fasihi wakurembesha lugha ya kawaida Eagleton, (2011). Mawazo ya Kirumbi (1975) ni kuwa, iwapo fasihi hujengwa na maneno, lazima maneno hayo yawe ni maneno zaidi ya maneno mengine. Fasihi si kuwa na maneno ya kisanaa, bali ni kutumia maneno ya kila siku kisanaa. Kirumbi anathibitisha kuwa lugha itumiwayo katika fasihi imerembeshwa ili kuleta mvuto kwa hadhira. Uwezo huu katika kazi za sanaa ndio hufahamika kama sifa ya ujumi.

Katika utafiti huu lugha hii itachunguzwa ilivyofumwa ili kutoa uwezo huu katika ngano simulizi za Kichuka. Kwa kuwa, katika uhakiki wa kazi ya kifasihi, mhakiki hawezi kukwepa suala la lugha kwa maana hiyo ndiyo nyenzo kuu ya fasihi, katika utafiti huu atabainisha sifa za lugha ya ngano pamoja na dhima yake ya ujumi na jinsi inanvyojipambanua na lugha ya kawaida. Mtafiti ataangalia kiwango cha lugha cha tamathali za usemi, taswira, viliwazo na usimulizi katika uhakiki huu ili kuona jinsi ambavyo lugha ni muhimu katika ujumi wa kazi ya kifasihi.

Njogu na Chimerah (1999) wakimnukuu mhakiki wa kirusi, Roman Jacobson (1960) Fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimakusudi Katika kauli hii, Jacobson ana maana kwamba fasihi huichukua lugha ya kawaida halafu ikaifinyanga, ikaiunda huku na huku hadi ikaifanya ipendeze. Hivi ni kusema kwamba, kile kinachosemwa kifasihi huwa kimeinuliwa kwa matumizi ya lugha hivi kwamba mdundo wake si wa kaida. Yaani, fasihi ni matumizi ya lugha kwa ufasaha. Mawazo haya yatafaa katika utafiti huu kwani mojawawapo ya malengo ya utafiti huu ni kuchanganua jinsi lugha simulizi ilivyotumika katika ngano za Kichuka ili kujenga mguso.

Lugha ya fasihi ni lugha iliyofanywa geni. Kwa sababu ya ugeni wake, ulimwengu wa kawaida nao unakuwa mgeni, usiokuwa wa kawaida na uliokengeushwa (Ntarangwi, 2004). Utafiti huu ulichunguza mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika ngano za Wachuka.

Njogu na Chimerah (1999), wamezungumzia fani katika ngano kwa mapana na kueleza kuwa haiwezekani kutenganisha fasihi simulizi na vipengele mahususi vya fani kama vile methali, jazanda, tashbihi, chuku, tanakali za sauti na kadhalika. Mjadala wao

kuhusu tamathali hizi za semi utakuwa wa manufaa kwa mtafiti kwa sababu atachunguza matumizi ya lugha katika ngano atakazoteua. Uchambuzi wao wa fani umeweka mhimili mzuri wa kuchambua fani katika kazi hii. Hii ni kwa sababu katika ngano za Wachuka ilibainika kuwa lugha simulizi na yenye mguso ilitumika.

## 2.7 Tamathali za Usemi

Tamathali za usemi hujulikana pia kama lugha ya kitamathali. Tamathali za usemi ni mojawapo wa dhana kongwe zaidi katika fasihi za ulimwengu. Dhana hii imeelezwa na kuainishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au iliyozoeleka. Ukiushi huu unaweza kuwa katika viwango vya maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Kwa hivyo, tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa, tamathali ya usemi huwa ni mbinu ya kupimia usemi wa mtunzi. Ubunifu lazima ujitokeze katika matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi. Pia tamathali za usemi huvutia hadhira na kuwapa hamu zaidi. Huwafanya hadhira kutafakari kuhusu wanayoshuhudia katika fasihi na kulinganisha na mazingira na mandhari yao. Mawazo haya yaliingiliana sana na utafiti huu kwani nadharia ya ujumi mweusi husisitiza kuwa mandhari na lugha ya masimulizi ni muhimu katika kuleta ule uzuri wa kazi za fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Kuhenga, (1977), Holman na Harmon, (1986), Tamathali za usemi ni nyingi mno. Zile zinazochukua nafasi muhimu katika kazi za kifasihi na hasa ngano ni pamoja na sitiari, tashbihi, kinaya, chuku, tafsida, tabaini, maswali ya balagha, nidaa, usambamba, tashihisi na taashira. Kwanza ni tashbihi, ambayo ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye hulka tofauti kama vile sitiari. Hata hivyo tofauti na sitiari, tashbihi hutumia viungo vya ulinganishaji. Aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi ‘ja’, ‘mithili ya’, ‘mfano wa’, ‘sawa na’ na ‘kama’. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi (Msokile, 1992).

Pili tuna chuku ambayo pia hujulikana kama udamisi. Ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukikuza kitu, mtu au hali kupita kiasi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusisitiza na pia kuchekesha. Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitu kinachohusika hukiukwa. Kitu hicho huweza kudunishwa au kukuzwa. Katika Kiswahili chuku hujulikana kama "kutia chumvi". Kulingana na Wales (2001:349) anafasili kuwa tashihisi; 'Ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa za kidhahania kinapewa sifa za binadamu.' Tamathali hii hutumiwa kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani za kihisia.

Kuhusu dhihaka ama Kinaya, Wamitila (2003) anasema kwamba msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kumhusu mtu au kuihusu hali fulani. Kimsingi, pana kinaya fulani katika maneno yaliyotumiwa. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka na kumkera mtu. Nidaa nayo ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao hutumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa.

Takriri ni mojawapo wa tamathali za usemi ambayo inahusu urudiaji katika lugha. Ingawa urudiaji ni wa aina nyingi sana, baadhi ya urudiaji umepewa majina mengine kama vile usambamba. Msokile (1992:61) anaeleza kuwa; Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa. Lengo kuu la msimulizi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulititilia mkazo jambo linaloelezwa. Usambamba nao ni aina maalum ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambapo hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi.

Kuna aina mbalimbali za usambamba. Miongoni mwa aina hizi ni usambamba wa kimuundo na usambamba wa kisintaksia. Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika nyimbo za ngano na katika ushairi wa Kiswahili ambapo muundo sawa wa baadhi ya mishororo hurudiwa katika beti mbalimbali. Kwa upande mwingine usambamba wa kisintaksia ni aina ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao unahusu uruduaji wa vipengele au vipashio vya kisintaksia katika mfuatano. Vipengee

virudiwavyo viwe virai au vishazi, hupatikana katika sehemu ile ile ya sentensi vikiwa vimeandamana.

Tanakali ni neno ambalo huiga sauti fulani, jinsi kitu kiangukavyo au kilivyo. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kumwezesha msomaji kupata taswira kamili na hisia za mlio wa kitu kinachozungumziwa. Wamitila (2003) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kilivyo n.k. Katika uhakiki, wataalamu wanatofautisha kati ya tanakali sauti inayotuletea hisia za mlio wa kitu fulani na tanakali sauti inayotukumbusha maneno yanayohusiana na neno fulani maalum. Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Aidha hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibiha na sitiari. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya hadhira aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani.

Wamitila (2003) anasema kiliwazo ni sehemu ya hadithi ambayo huwa imekusudiwa kuituliza hadhira kidogo hasa kwenye hadithi zinazozungumzia masuala ya kusikitisha au ya kitanzia. Kiliwazo kinaweza kuwa kifungu kilichojaa ucheshi kilichokusudiwa kuiondoa kwa muda ile hali ya kusikitisha. Nyimbo hutumiwa kama viliwazo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa usimulizi ni uelezi wa matukio katika hadithi. Mawazo ya Wamitila ni kuwa kazi zote za fasihi lazima ziwe na matukio na hayo matukio yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia nyingi za usimulizi. Msimulizi hana budi kuchagua mtindo fulani ambao ni wa kufaa zaidi kuwasilisha mawazo yake yatakayomwathiri msikilizaji kwa njia moja au nyingine. Usimulizi unaweza kuwa wa kufululiza matukio moja kwa moja bila ya kutatiza, au unaweza kuwa usimulizi wa kirejeshi na ule wa kiutomaji ambapo msimulizi hukatiza mtiririko au hurejelea mambo yaliyopita (kirejeshi) au aweze kukatiza mtiririko wa hadithi na kuweka vifungu kama vile barua.

Kwa mujibu wa Miruka (1994), katika usimulizi nafsi ya kwanza kuna mhusika ambaye anashiriki katika hadithi. Yeye huwa anajielezea tu tajriba zake lakini hana uwezo wa kueleza za mtu mwingine. Msimulizi huyu huweza kujenga uhusiano wa karibu mno kati yake na hadhira. Wasikilizaji huona anachoona, kusikia anachosikia na kuhisi

anachohisi. Anaposimulia, yeye hutumia viwakilishi “mimi” na “ni” vya nafsi ya kwanza. Usimulizi wa nafsi ya pili huhusisha viwakilishi vya nafsi ya pili “wewe” na “u”. Kulingana na Wamitila (2003), aina hii ya usimulizi ni nadra sana kupatikana katika Kiswahili hata katika lugha nyingine. Matumizi ya nafsi ya pili yanaweza kuwarejelea wahusika wanaopatikana katika ulimwengu huo, au kurejelea ulimwengu wa wasikilizaji ambapo kuna kuvunjwa kwa mpaka uliopo kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi. Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa na matumizi ya ‘a’ na ‘yeye’ katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasomi. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani. Mawazo haya yatafaa katika utafiti huu hasa katika uchunguzi wa jinsi lugha simulizi inavyotumika katika kujenga mguso kwa hadhira.

Wellek na Warren (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo kushiriki moja kwa moja, huwaacha wahusika peke yao na kumruhusu msomaji kuwahakiki bila kumwelewa msimulizi. Usimulizi mwingine humruhusu msikilizaji kumwelewa msimulizi na mitazamo yake kuhusu mambo yanayoikabili jamii. Usimulizi wa matukio huweza kuwa wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu.

Katika ngano, usimulizi ni muhimu sana kwani huwasilisha ufafanuzi zaidi wa sifa za mandhari, wahusika wake, majukumu yao na matukio yakiwa katika mbinu ya mfululizo. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi msanii atakaowasilisha. Katika utafiti huu mtafiti aliangazia jinsi ujumi hujengwa kwa kutumia tamathali mbalimbali za usemi kama vile, tashbihi, chuku, dhihaka, takriri, usimulizi, taswira, viliwazo na tanakali za sauti katika ngano za Kichuka.

### 2.8 Wahusika wa Kisimulizi

Wahusika wa kisanaa huwa ni viumbe ambao huumbwa na msanii kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu anayokusudia katika sanaa yake (Wamitila 2002). Matendo, mienendo, lugha, vionjo, uhai na ufu wa wahusika wa kifasihi hudhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya mwandishi. Lugha wanayopewa huonyesha matumaini na imani ya mwandishi kwa sababu lugha yao huwa ya wengine. Misemo na maelezo ya

wahusika wa kifasihi huathiriwa na matamanio ya wengine na hivyo kuzua ukinzani kati ya lugha ya mwandishi na ya wahusika wake (Bakhtin, 1981). Mawazo haya ni ya muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa kila kazi ya fasihi huwa na wahusika wa kipekee. Kwa misingi hiyo mtafiti anashawishika kuwa wahusika katika tanzu za fasihi simulizi huwa na sifa za kipekee za kisimulizi kutokana na upekee wa mandhari na muktadha wa fasihi simulizi. Upekee huu wa sifa za wahusika unakisiwa kuwa na sifa ya kiujumi katika muundo wa ngano simulizi za Kichuka; hivyo kuchunguzwa katika utafiti huu.

Kineene wa Mutiso, (2005) anadai kuwa wahusika wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe ni watu, wanyama, ndege, wadudu miti, mashetani, majini na kadhalika. Maelezo yao yanaeleza tu mifano jumla ya wahusika katika kazi za fasihi. Hata hivyo, Madumulla (2011) anaweka mpaka wa wahusika wa kisimulizi kwa kudai kuwa, wahusika katika hadithi Simulizi na baadhi ya Hadithi Fupi kwa kawaida huwa ni wanyama, wadudu, mimea, mashetani na miungu. Tukizingatia mazingira na muktadha wa nyakati za kutungwa kazi nyingi za kimapokeo za fasihi simulizi ni dhahiri kuwa wahusika wa kisimulizi huwa wa aina ile.

Hali hii inaweza kuchangiwa na maisha ya vichakani, msituni pamoja na imani za kishirikina zilizotawala tamaduni za jamii nyingi za Kiafrika. Mtafiti anaona kuwa nafasi ya wahusika wa aina hii ni muhimu kuchunguzwa katika kazi yoyote ya kimapokeo katika fasihi simulizi. Upekee huu wa wahusika unachukuliwa kama kiungo cha ujumi wa ngano simulizi za Kichuka kama ilivyo katika mada ya utafiti huu. Mtafiti ataangazia jinsi msimulizi wa ngano anavyowachora wahusika katika ngano za Kichuka na kueleza jinsi sifa za wahusika zilivyotumika kupamba ngano simulizi za Kichuka kama nyenzo ya mguso na hisia kwa hadhira.

Steere (1889), alikusanya simulizi mbali mbali kutoka kwa jamii ya Waswahili wa Zanzibar na kuzihariri. Hadithi hizi zilikuwa maarufu sana. Lengo la Steere lilikuwa kuwahamasisha watu wengine waliojua kusoma na kuandika kuweza kupata picha ya uandishi wa hadithi. Yeye alishughulikia waliojua kusoma na kuandika tu na kulisahau tabaka la wasio wasomi. Malengo ya fasihi simulizi kwa jumla ni mengi, miongoni mwao yakiwa kufunza maadili kwa jamii, kuburudisha, kuonya na kuendeleza tamaduni za jamii na kadhalika. Utafiti wa ngano simulizi za Kichuka utalenga tabaka

la wasio wasomi na wasomi kwani zinasimuliwa kwa lugha ya Kiasili ya kichuka hivyo kueleweka kwa urahisi.

## 2.9 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ujumi wa kinudhuma. Kwa mujibu wa Foley (1995), nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma ilianzishwa kule Marekani mwaka wa 1960 na waasisi wake wakiwa Dennis Tedlock na Dell Hymes. Akina Dennis Tedlock na Dell Hymes walibuni nadharia hii kutokana na utafiti wao wa matini simulizi miongoni mwa Wamarekani. Nadharia hii inajihusisha na ujumi katika upangaji wa matini simulizi kishairi kwa misingi ya taaluma za Isimu-Amali, Isimu Jamii, Ethnografia ya Mawasiliano na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ndani ya Muktadha wa Utendaji. Dennis Tedlock alisisitiza zaidi sifa ya usimulizi katika matini pamoja na mpangilio maalum wa mistari. Vilevile, anadai kuwa matini simulizi inapaswa kuwasilishwa kwa mistari kama ilivyotolewa na fanani katika utendaji wa fani ya usemaji.

Uwasilishaji huu huzingatia vipengele kama vile, uradidi, shadda, kiimbo na matumizi ya jazanda. Mwisho, anasema kuwa, utafiti wa nyanjani huwa lazima katika uchanganuzi wa fani ya usemaji, lakini sio matini simulizi iliyoandikwa. Matini simulizi isiandikwe tu kwa maneno bali pawe na maelezo ya ziada yanayofafanua matendo-ambatano ili kuonyesha namna ambavyo ilitendwa katika hali halisi.

Naye, Dell Hymes (1982) anadai kuwa, kufaulu kwa uwasilishaji wa matini hutegemea sana uzingatiaji wa muwala na mfumo unaokubalika katika jamii husika. Vilevile, mtafiti anastahili kuchunguza matumizi ya aina yake ya kiujumi katika fani pamoja na uzingatiaji wa sarufi ya lugha husika. Anazidi kupambanua kuwa, atafanya hivyo, kwa kuzingatia Isimu Amali, kwani anachunguza maana ya ishara na maneno katika muktadha wa matumizi ndani ya mawasiliano. Hii ni kwa sababu, maana hubainishwa kwa kuchunguza uhusiano kati ya ishara au kitaja na mtumiaji wake katika jamii maalum.

Harvilahti (2001) alichangia nadharia hii kwa kusema kuwa, maana katika matini simulizi huumbwa na vipande sauti pamoja na utamaduni wa jamii husika. Aidha, Alembi (2002) aliiboresha nadharia hii kwa kusema kuwa, mawazo ya Hymes na

Tedlock kuhusu asili ya data ya kuchambuliwa, yanaungana katika mchakato wa ung'amuzi wa maana katika kuhusisha jamii tafitiwa. Mawazo ya waasisi yalitumiwa kuzalisha mihimili ya nadharia hii:

i. Kuna mfumo maalum wa kishairi unaotokana na mpangilio wa mistari na aya katika matini simulizi. Mpangilio huu maalum unazingatiwa na kutambuliwa na jamii mahsusi.
ii. Mistari na aya hazipangwi tu kwa mujibu wa sheria za kishairi, lakini pia hutumiwa kuwasilisha ujumi na tajiriba ya pamoja ya jamii husika kwa kutumia takriri, mianzo maalum na jazanda.
iii. Matini simulizi hupangwa katika mistari inayopokezana, kuingiliana na kukamilishana bila kuzingatia kwa dhati mipaka ya kimatini.
iv. Matini simulizi huwa na matumizi maalum ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio na wa kihistoria. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi.
v. Ungamuzi wa matini simulizi unalenga usikiaji na uelewaji wa utendaji wa matini simulizi kwa kujikita zaidi katika ung'amuzi wa matamshi; kwani matini simulizi inategemea sana utamkaji (ubora wa sauti na ufaraguzi)

Mihimili iliyozingatiwa katika utafiti huu ni pamoja na:

i. Mistari na aya hazipangwi tu kwa mujibu wa sheria za kishairi, lakini pia hutumiwa kuwasilisha ujumi na tajiriba ya pamoja ya jamii husika kwa kutumia takriri, mianzo maalum na jazanda. Mhimili huu ulitumikizwa katika kuchanganua nafasi ya mbinu kama vile takriri katika uendelezaji wa ujumi wakati wa utunzi na uwasilishaji wa ngano za wachuka. Ulitoa mwongozo na mamlaka ya kuhakiki mbinu za kimtindo zenye kutumika katika uwasilishaji wa ujumi pamoja na tajiripa ya pamoja ya jamii ya wachuka.
ii. Matini simulizi huwa na matumizi maalumu ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio na wa kihistoria. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani

yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Nguzo hii ilielekeza uchambuzi wa fani inayotumika katika ngano simulzi za Wachuka kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa Wachuka. Aidha, mhimili huu ulielekeza katika kutathmini jinsi mtiririko wa matukio huendeleza ujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka. Pia, mhimili huu ulitumiwa kubainisha namna sifa za wahusika wa kisimulizi zilitumika kupamba ngano simulizi za Wachuka.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii itashughulikia mbinu za utafiti zitakazotumiwa katika utafiti huu. Utafiti huu ni wa kiuchambuzi. Mtafiti ataelezea mbinu za utafiti, utafiti wa awali, eneo la utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, hatua za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti.

### 3.2 Mpango wa utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu elezi. Lengo lilikuwa kutambulisha vifungu fani katika ngano za wachuka, kuchunguza, kuchanganua pamoja na kubainisha vipengele vya kimuundo vya ngano vinavyojenga maana, kuleta ujumi na umbo kamili la ngano.

### 3.3 Utafiti Awali

Utafiti awali ulifanywa kwa lengo la kufanyia majaribio vifaa vya utafiti, kuviimarisha pamoja na kujizoesha na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti kamili. Mtafiti alikusanya ngano tatu kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Gichuka wanaoishi makazi tofauti. Pia utafiti awali ulimsaidia mtafiti katika kujifahamisha na eneo la utafiti na pia kujiepusha na makosa ya uchanganuzi wa data katika utafiti kamili.

### 3.4 Eneo la Utafiti.

Utafiti huu ulilenga jamii ya wachuka na magwiji wa usimulizi wa ngano wanaoishi katika tarafa ya chuka, eneo mbunge la Chuka Igamba ng'ombe. Eneo hili la utafiti liliteuliwa kama kielelezo kuwakilisha jamii nyingine za Kiafrika. Pia, Mtafiti ana umilisi wa lugha ya Kichuka kwa hivyo ataweza kutangamana na walengwa kwa urahisi.

### 3.5 Kundi Lengwa

Utafiti huu uliendelezewa nyanjani. Mtafiti alielekekea nyanjani ili kukusanya ngano miongoni mwa wanajamii wa Wachuka. Utafiti huu ulilenga ngano simulizi kumi za Wachuka kutoka kwa manju na wasimuliaji tofauti. Kusudi la kuchukua ngano hizo ni kuepuka kuacha nyingine kando na kukosa ngano zinazoweza kuwa sampuli inayotosha

kuwakilisha ngano ambazo hazijafanyiwa uchambuzi. Aidha hii imetokana na kumakinikia zaidi na ngano zile ambazo zina athari kubwa ya ujumi.

**3.6 Uteuzi wa Sampuli**

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), sampuli ni sehemu inayoteuliwa kuwakilisha jumla ya watu wote waliolengwa katika utafiti. Mbinu ya uteuzi wa sampuli kimarejeleo ilitumika kuteua watambaji wa hadithi. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika katika utafiti huu kuchagua idadi ya ngano zilizozalisha data ya kutosha. Hii ni kwa sababu mtafiti ana uhuru wa kuteua ngano zilizo na habari anazotaka. Utambaji ngano unahitaji fanani aliye na kipawa cha kutamba ngano. Mtafiti alipata wasailiwa waliomtambia ngano. Wasailiwa walitambulishwa na wazee wa vijiji.

Kwa kuzingatia ufahamu na tajriba ya msailiwa kuhusu ngano, umri wa msailiwa, kumbukumbu nzuri ya msailiwa na ulumbi na ukwasi wa lugha wa msailiwa, wasailiwa watano (5) waliojitokeza na ambao walikuwa tayari kutamba ngano walihusishwa katika utafiti huu. Baada ya kuwatambua fanani, mtafiti aliwasiliana nao ili kuwaeleza lengo la kutaka kutambiwa ngano. Aliwaeleza kuwa alitaka kukusanya ngano ili kuchunguza vipengele vya kiujumi vinavyotumika katika ujenzi wa ngano za Gichuka kwa lengo la kiusomi. Alikutana na wasailiwa na wakamtambia ngano kila mmoja wao. Ngano tano (5) ziliteuliwa kutokana na kumi (10) zilizosimuliwa.

**3.7 Vifaa vya Utafiti**

Kinasa sauti ni mojawapo ya kifaa kilichotumika katika kunasa na kurekodi sauti katika hali zote za muktadha wa utambaji kwani kulikuwa na ngano ambazo wakati mwingine zilikuwa na matukio marefu. Kalamu na shajara vilitumika maktabani na nyanjani. Mtafiti alichukua nukuu muhimu na kuziandika kwenye shajara kwa kutumia kalamu. Data hizo zilihifadhiwa kwa uangalifu mpaka hapo zilipotumika wakati wa kuandaa na kuandika ripoti ya utafiti na tasnifu ilipomalizika Tarakilishi ni kifaa kingine muhimu kilichotumika. Licha ya kuwa data za maktabani na nyanjani zilihifadhiwa humo, tarakilishi ilitumika kama sehemu ya maktaba tembezi ambapo mtafiti aliweza kupata fursa ya kusoma makala yanayohusiana na utafiti wake. Hivyo basi, tarakilishi ilitumika katika kipindi chote cha utafiti, yaani kuanzia wakati wa maandalizi ya utafiti, wakati wa kuchanganua data na wakati wa kuandaa

tasnifu.Mtafiti alitumia shajara kunukuu mambo muhimu yanayohusiana na utafiti wake.

## 3.8 Hatua za Ukusanyaji wa Data.

Data iliyotumiwa katika utafiti huu ilikusanywa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulifanywa kabla ya utafiti wa nyanjani katika baadhi ya maktaba kwenye vyuo vikuu. Maktaba hizi ni maktaba ya Chuo Kikuu cha Chuka, Kenyatta na Maktaba ya kitaifa ya Kenya. Makala, majarida, vitabu na tasnifu ambazo zinaangazia vipera mbalimbali vya fasihi simulizi zilirejelewa na zaidi kusoma kuhusu Nadharia ya kinudhuma iliyoongoza uchanganuzi wa data. Mtafiti alipata barua kutoka katika Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka ya kumsaidia kupata kibali kutoka kwenye Tume ya Sayansi ya Teknolojia ya Kitaifa. Baada ya mtafiti kupata kibali kutoka kwenye NACOSTI, alijulisha Afisi ya Mkuu wa Elimu wa Kaunti dogo ya Chuka igamba ngombe. Alipata kibali akatangamana na watafitiwa kutoka jamii ya chuka katika harakati za kukusanya data. Wasailiwa walimtambia ngano na akazirekodi. Utafiti wa nyanjani ulihusu kukusanya ngano za jamii ya Wachuka kwa kutumia kinasa sauti. Baadaye ngano hizi zilifanyiwa unukuzi kwa kutumia kalamu na karatasi. Data hii yote ilihifadhiwa katika kanda za kunasia sauti.

## 3.9 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu ni ule wa maelezo ambapo data hupangwa katika makundi ya uhusiano aidha kimaudhui ama dhana na kila kutolewa maelezo (Mugenda & Mugenda, 2003). Ngano za wachuka zilizokusanywa, zilinukuliwa na kisha kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwani zilitambwa kwa lugha ya Gichuka. Ngano zilizokusanywa zilifanyiwa uteuzi wa kimaksudi ili kupata zilizo na ujumbe anaohitaji mtafiti. Kisha, ngano zilizodhihirisha ujumi zilifanyiwa uchambuzi kwa misingi ya malengo ya utafiti na kuelekezwa na nadharia ya kinudhuma. Kwa kutumia vigezo vya wahusika, taswira, mtiririko na lugha simulizi mtafiti aliweza kubaini kuwa mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka huendelezwa na mtririko wa matukio kiujumi, sifa za wahusika kisimulizi na mbinu za kimtindo hasa mbinu za kisanaa na za lugha.

### 3.10 Uwasilishaji wa matokeo

Baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti hutakiwa kuchambua, kujadili na kuwasilisha data zilizokusanywa. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zilisaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Hii ni hatua muhimu katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Katika kushughulikia data iliyokusanywa kuhusiana na mwega wa ujumi katika ngano za Gichuka, uwasilishaji wa kimaelezo ulizingatiwa. Mtafiti aliongozwa na uchambuzi wa kifasihi katika uchanganuzi wa data. Njia hii ni mwafaka katika uchambuzi wa utafiti huu kwa kuwa utafiti ni wa kifasihi. Mbinu hii humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma kazi ya kifasihi, kuelewa maudhui, falsafa, lugha na utamaduni wa kazi husika na kutolea maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa kwa namna ambayo itawezesha kujibu maswali ya utafiti. Uchambuzi wa data umefanywa kulingana na maswali ya utafiti na malengo ya utafiti huu. Data zilizokusanywa katika utafiti huu zimechambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo. Hii ina maana ya mfumo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu.

### 3.11 Maadili ya Utafiti

Kabla ya ukusanyaji data mtafiti alipokea kibali kutoka kwa kamati ya maadili ya Chuo cha Chuka, Kisha akachukua kibali kutoka kwa NACOSTI. Mtafiti alielekea nyanjani na kujitambulisha kwa wasailiwa na kuwaeleza malengo yake kwa uwazi. Aliwaelezea kuwa ile data waliyompa ingetumika kwa minajili ya utafiti huu pekee na kwamba angewarekodi kwa ajili ya kumbukumbu. Mtafiti alijizuia na vitendo vyote vya ufisadi mfano kutoa rushwa kwa lengo la kupata data. Mwisho mtafiti aliwarejelea wataalam wote aliorejelea au nukuu katika kazi yake kwenye sehemu ya marejeleo. Matokeo ya utafiti pia , yatawekwa kwenye maktaba ili kufaidi wanajamii.

# SURA YA NNE

# MTIRIRIKO WA MATUKIO KATIKA NGANO SIMULIZI ZA WACHUKA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mtiririko wa matukio katika ngano za wachuka. Malengo yalikuwa kueleza mtiririko wa matukio na kuthibitisha jinsi mtiririko wa matukio huendeleza ujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka. Mtafiti aliangazia tukio la wema, msukosuko wa mwenendo, harakati za kupata ukombozi na hatima ya mui kama vipengele vya mfumo maalum wa utunzi wa ngano simulizi za Wachuka.

## 4.2 Mtiriko wa Matukio katika Hadithi ya Fisi na Kindi

Dell Hymes (1982) anadai kuwa, kufaulu kwa uwasilishaji wa matini hutegemea sana uzingatiaji wa muwala na mfumo unaokubalika katika jamii husika. Matini simulizi huwa na matumizi maalum ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio na wa kihistoria. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Uhakiki wa matukio katika hadithi hii ulitangulizwa kwa kutoa muhtasari kisha kuchanganua mpangilio wa matukio kiujumi.

### 4.2.1 Muhtasari wa Hadithi ya Fisi na Kindi

Fisi na kindi wanaanza kama marafiki. Wanakubaliana kuwa na mradi wa kupanda kunde. Baada ya kunde kukomaa, wote wawili wanaanza kuvuna kidogokidogo. Kindi ndiye anatangulia kuvuna huku fisi akimwadama kila anapokwenda kuchuma. Fisi anakuwa laghai na kumuhini Kindi kwa kuiba mbaazi zake. Muda unavyosonga kindi anagundua kuwa kunde zake zinaelekea kuisha huku za fisi zikibakia vilevile ingawa huwa anakutana naye akielekea kuvuna. Kindi anapasua mbarika na kumdadisi mwenziwe iwapo humwono yeyote akivuna kunde zake baada ya kindi kuondoka. Fisi anakana kisha kindi kuamua kuwe na tambiko la kumtambua mwizi. Wanakubaliana kuwa kila mmoja aje na wenzake kando ya mto Ginci Kiiri. Agizo linatolewa kwa kila mmoja kuchupa na kuruka mto Ginci Kiiri na yule atatumbukia basi itakuwa ndiye mwizi. Kindi anatangulia kuruka na kuvuka ngambo nyingine. Awamu ya fisi inafika huku fisi akishindwa kuruka na kutumbukia mtoni mara yote tatu aliyojaribu. Mara za kwanza pili anatumbukia na kuwarai wenzake kumtoa. Mara ya tatu wote wanahamaki

na kumwacha asombwe na maji ya mto kwa kuwa ilikuwa bayana kwamba ndiye alikuwa akiiba kunde za kindi.

### 4.2.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi

Kwa mujibu wa nadharia ya ujumi wa kinudhuma, iliyorejelewa katika misingi ya nadharia kwenye sura ya pili, kuna mfumo maalum wa kishairi unaotokana na mpangilio wa mistari na aya katika matini simulizi. Ingawa mtafiti hakujikita katika ushairi, mawazo ya mhimili huu yalielekeza katika kuchunguza na kufafanua mpangilio wa mistari na aya katika matini ya ngano kama kiini cha mfumo maalumu wa kijumi katika ngano za Wachuka. Pia, utafiti ulipata uchukulio kuwa mfumo huu maalum unaweza kubainika katika ngano zaidi ya kuwa katika ushairi. Ngano za wachuka huzingatia muwala na mfumo unaokubalika katika jamii kimaadili. Dhima kuu ikiwa kuonyesha nguvu ya wema dhidi ya uovu. Hadithi hutangulizwa kwa tukio la wema. Sehemu ya kati inakuwa msukosuko wa kimaadili kwa wahusika kuingilia tendo la uovu kisha harakati za kupata haki. Hitimisho inakuwa hukumu na hatima ya wahusika waovu kuangamia kama funzo. Mtiririko huu wa matukio katika hadithi ya fisi na kindi umejitokeza ifuatavyo:

**Tukio la wema**: Hadithi inaanza kwa tukio la wema au habari njema: Urafiki unaanza baina ya fisi na kindi "*Mbiti na kabare **ciatumire urata** cierana niciuge itema"* (fisi na kindi walianza urafiki wakakubaliana wapalilia konde). Urafiki ni wema ambao unakuwa kama kiunzi cha kuishi vyema kwa pamoja. Urafiki unazua mradi wa maendeleo wa kupanda kunde *"Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko*" (wakakubaliana wapande kunde). Mradi mzuri pia. Hatimaye fisi na kindi wanapanda kunde. Urafiki unajenga ushirikiano baina yao. Ushirikiano huu unawawezesha kupiga hatua mbele na kufanikiwa kupanda kunde, zikamea vizuri na kukomaa. "Thoroko ri ciakurire..." (mbaazi zilipokomaa…).

**Msukosuko wa mwenendo:** Fisi anaanza kubadili mwenendo wa uaminifu katika urafiki wao. Wema na ubaya zinaanza kuvutana. Tamaa na ubinafsi zinaanza kumtawala kisha kubadilika kuwa mnafiki na mwongo. Hili linadhirika katika kifungu kifuatacho:

"*Riu, Mbiti yathii yatua baria kabare gatuire ri, kabare gakithii kathiite gutua ri, gakiona Mbiti itatua kwayo, itwire gwako. Riu kabare gakithii gakiuria Mbiti," Mbiti' nuntu ni gweu urigirie ri, nuwonire uria untwirire nthoroko?" "Aari, aari cianjeru cianjeru ntageria kwona, ari ntamwona ntamwona".* Fisi anaanza kumlaghai kindi kunde zinapokomaa "*Thoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na Mbiti. Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria Kabare gatuire*" (pindi tu kunde zilipokomaa, kindi akaenda na kuchuma kunde kwake. Akirudi kutoka shambani akakutana na fisi akielekea kondeni pia. Fisi anakwenda na kuchuma kunde pale pale kwa kindi). Urafiki unaanza kuzorota.

**Harakati za kupata haki au ukombozi**: Tambiko la mtihani wa kutambua mwovu linaandaliwa. Kindi na fisi wanakubaliana kukutana kwa mtihani wa kuruka mto. anaambiwa:

> "*Amwira, "riu, nitutue kiatho na auke. Withiranie mbiti cionthe nan mbithiranie tubare tuunthe. Tuthi muburoni witagwa Ginci kiiru. Tuthii tutube. Uria ukagwa ku, niwe ukamenyeka niwe wiaga nthoroko cia uria wingi."*
>
> (Akamwambia, "Sasa, tupange miadi ya kesho kutwa uwalete Pamoja Fisi wote, nami niwalete kindi wote. Twende katika mto wa Ginci kiiri. Twende turuke. Yule atakayeanguka majini ndiye mwizi aibaye kunde za mwenziwe.")

Kufaulu kuruka inakuwa ishara ya uzuri wa kuondolewa lawama. Kutumbukia mtoni inakuwa ishara ya uovu wa kupatwa na lawama. Mtihani huu ni itikadi na idili ya jamii.

**Hukumu na hatima ya mui**: Adhabu inatokana na uamuzi wa nguvu za maumbile katika tambiko. Tazama hiki kifungu:

*Kabare gatuba gakinya naa rugongo ruru rungi. Mbiti yambiriria riu;*
*Ntauma x2*
*Muthooko x2*
*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

Kindi akachupa akafika ng'ambo ya pili. Fisi naye akaambiwa aimbe.

Akaimba:

Sikua x2
kunde x2
Za ndugu kindi Ginci kiiru nsombe

Mhusika mui hukumbana na maangamizi hasa mauti. Fisi anaanguka kwenye mto Ginci Kiiru.

> *Mbiti yagamba runcini ringi nku! Yagwa runcini. Yambiria gukiriria tuguru, "Ndutani rutaani ntantubite wega. Ti niu. Ti nu. Ti niu. Ndutani ntatubite weega."*
>
> *(*Fisi akaanguka majini chubwi! Akasema, "Tafadhali niondoeni. Sikuruka vizuri."Fisi wengine wakakubaliana wakamnyanyua)

Adhabu ni ridhio ya kupata haki. Wema wanashinda kwa kuponea. Waovu wanashindwa na kuondolewa kwenye ramani ya jamii.

> *Mbiti ri, yerwa yerwa ni mbiti i cingi atiri, "tutikuruta ni weu wiaga kabare. Mbiti ikinatwarwa ni runci.*
>
> (Fisi wengine wakamwambia Fisi, "Hatutakutoa. Ni wewe huiba kunde za kindi." Fisi akasombwa na maji.)

Mpangilio huu unatawaliwa na wema, mvutano wa ubaya na idili za jamii. Adhabu na njia ya kubaini mwenye haki inategemea imani na itikadi za jamii. Kutokana na matukio katika hadithi ya kindi na fisi inabainika kuwa Wachuka wana imani kwamba ukiwa mwenye haki utatetewa na hali za kimaumbile kama vile uwezo wa kuruka mto. Kindi anaponea huku fisi anazama mtoni na kuangamia. Mwizi anabainika bila mapendeleo. Fisi anaibuka kuwa ndiye aliyeiba kunde za kindi. Inavutia kuona ukweli unabainika na wema kutawala dhidi ya uovu.

## 4.3 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya Ngongoana na Gacinci

Mtriko wa matukio katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci uliangazia muhtasari wa hadithi na mtiririko wa matukio kiujumi.

### 4.3.1 Muhtasari wa Hadithi

Ni hadithi ya Ngongoana na Gacinci; ndugu wawili mayatima kutoka ukambani. Kunakuwa na ngoma za densi za kitamaduni zilizochezwa kila wakati kule vijijini na kumpa Gacinci hamu ya kushiriki. Kila anapotaka kushiriki dadake Ngongoano anamkanya kwa hofu kuwa akimwacha ataliwa na mazimwi. Wakati mmoja ngoma inakuja kuchezwa kijijini karibu na nyumbani kwao. Gacinci anakhitari kwenda kushiriki huku akimhakikishia dadake kwamba atakuwa macho kulichunga zimwi

lisiingie na kumla. Pindi tu Gacinci anapotoka zimwi lililokuwa karibu na mlango linajitokeza na kuingia chumbani alikokuwa Ngongoana. Zimwi linamwomba Ngongoano maziwa na kuyanywa yote kisha likamwomba alibebe. Ngongoanga akachukua kamba akalifunga zimwi huku akiwa haliwezi. Akalibeba kwa kujitahidi. Akaenda akilia. Walienda wakiimba kuhusu njia ya mugumo. Zimwi linamwomba alipitishie njia ya Mumbu. Ngongoana akiwa kwenye ngoma anasikia Gacinci akimwambia wimbo wa hadhari. Gacinci anaomba msaada kutoka kwa wenzake washiriki wa ngoma ili kukabiliana na zimwi na kumwokoa dadake. Kakake anajitokeza na kusaidiwa na wenzao waliokuwa wakicheza ngoma pamoja na kulikimbiza zimwi. Zimwi linakabiliwa na kakake kisha kuliangamiza kwa mishale na mkuki. Lilipokufa, Gacinci na dadake wakarejelea nyumbani.

#### 4.3.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi

Hadithi ilitangulizwa pia kwa tukio la wema. Sehemu ya kati ikawa msukosuko wa kimaadili kwa wahusika kuingilia tendo la uovu kisha harakati za kupata haki. Hitimisho ilibainika kuwa hukumu na hatima ya wahusika waovu kuangamia kama funzo. Mtiririko huu wa matukio katika hadithi hii uliendelezwa ifuatavyo:

**Tukio la wema:** Hadithi inatanguliza suala la undugu wa Ngongoana na Gacinci.

> "*Kwari na Ngongoana na Gacinci. Muntu na muru wa ng'ina.*
> (Paliondokea Ngongoana na Nduguye Gacinci kutoka ukambani)

Ingawa ni mayatima wanashirikiana na kusikizana. Ngongano anakuwa mtiifu na kutilia maanani ushauri na makanyo ya Gacinci

> *"Ngongoano akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkariwa ni marimarimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua akarega kuthii…"* Atua kumwiraga bu wa rionthe akigucaga*"* (Gacinci akamwambia Ngongoana, "Ebu niende kwenye wimbo." Akamkanya…. Akawa akimwambia hivo kila wakati akisikiliza). Udugu na utiifu wa Gacinci ni wema unaoridhisha katika jamii.

**Msukosuko wa mwenendo:** Gacinci anaanza kubadilisha mwenendo. Anakaidi makanyo ya Ngongoana na kwenda kushiriki ngoma hapo kijijini.

> "*Ntuku i ingi rwainwa bakubi muno. Amwira, "Ari nee, gankegue baba ii ngakuthikagiriria ii nkegucaga irimarimu rikigita atia? Rigiigica." …. Athii. Akinya rwimboni."*

> (Siku nyingine, ngoma ikaimbwa karibu na pua na mdomo. Akamwambia, "Ebu nikasikilize hapa. Nitakuwa macho zimwi likija." …. Akaenda akafika kwenye Ngoma).

Ukaidi wa Gacinci unawaletea matatizo. Zimwi lililokuwa karibu na mlango linaingia na kuanza kumtesa Ngongaono baada ya kumpata akiwa peke yake. Ushirikiano wake na dadake inakuwa na mwanya. Zimwi linapta nafasi ya kumla Ngongoano. Tazama huu muktadha:

> *Irimarimo nario riari wa baba ruriini rikinathungira. Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria… "Ngua. Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria. Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikuribota na arikua.*
>
> (Zimwi lililokuwa karibu na lango likaingia. Likamwita, "Ngongoana," akaitika, "wuu." "Nipe maziwa." Akalipa maziwa kwenye dundu likatikisa, likanywa yote.… Likamwambia, "Nibebe kama kuni ni mie nitakula." Ngongoana akachukua kamba akalifunga zimwi huku akiwa haliwezi. Akalibeba kwa kujitahidi. Akaenda akilia)

**Harakati za kupata haki au ukombozi**: Ngongoana anaanza kuimba wimbo kwa sauti ili kumtaarifu kakake aje amkomboe kutoka mikononi mwa zimwi.

> *Ngongoana akiriraga muno. Akiinaga:*
>
> *Gacinci ii Gacinci mwile,*
> *Ndagukanilie wathi wa utuku*
> *Gacinci mwile x3*
>
> Naye Ngongoanga alikuwa akilia sana. Akiimba:
>
> Gacinci ii Gacinci mwambie
> Nlikuonya nyaimbo za usiku
> Gacinci mwambie x3

Gacinci anasikia sauti ya dadake akiimba kwa kilio na kuwaomba wenzake kusitiza ngoma ili asikilize wimbo wa dadake vyema. Ngoma inasita kisha Gacinci anawaeleza kuwa sauti wanayoisikia ni ya dadake anayesumbuliwa na zimwi. Anawaomba waandamane naye ili kumsaidia dadake. Kakake anaibukia na kutangulia kwenda kulikabili zimwi. Wote wanafika kwa pamoja na kuamrisha aliyebebwa mgongoni mwa Ngongoana dadake Gacinci kutua mara moja. Zimwi linashuka.

> *"Gacinci akinegua mwang'ina akina. Akinela antu, "Takirani mbigueni." …. Akimera, "riu ncuni ii, mumbile nuntu riu ni irimarimu rikuthinia mwana wetu," Makiria rwimbo. Muruang'ina aca arumirirwa ni antu mau mangi. Magikinya methiriria ni irimarimu rikuitwe ni mwang'ina akiriraga… Mauga, "unu ukuite niakinye nthi." Irimarimu riauma.*

Gacinci akasikia dada ake akiimba akaambia watu, "Ebu nyamazeni nisikie" Akasikia…. Akawaambia, "Sasa njooni mnipeleke kwa kuwa hilo ni zimwi linalomsumbua msichana wetu." Wimbo ukatulia. Kakake akaja akatangulia na kufuatwa na wengine…Walipofika wakapata zimwi lilikuwa limebebwa na dadake akilia. Wakase, "Huyo aliyebebwa akanyange chini." Zimwi likashuka.

**Hukumu na hatima ya mui**: Adhabu ya kushambuliwa kwa zimwi inatekelezwa. Likashambuliwa kwa mishale na kuchomwa kwa mikuki, likafa. Lilipokufa, Gacinci na dadake wakarejelea nyumbani. Katika kifungu hiki tunambiwa:

> *Riambilia kurathwa na migwi, kumuntangwa na matumo, riakua. Riakua nirio Gacinci menukile na mwang'ina*
> (Zimwi likashambuliwa kwa mishale na mikuki mpaka likaaga. Lilipokufa ndipo Gacinci walirejea nyumbani)

### 4.4 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya Wasichana Wanne wa Ikamba

Sehemu ya mtiririko wa hadithi ya wasichana wanne wa ikamba ilishughulikia muhtasari wa hadithi kisha mtiririko wa matukio kwa ujumla. Sehemu ya kwanza ililenga muhtasari kisha sehemu ya pili ikajikita kwenye mtiririko.

#### 4.4.1 Muhtasari wa Hadithi

Ni hadithi ya wasichana wanne kutoka ukambani wanaokuwa pamoja. Kunatokea mpango wa kuwatia Mwanya kwenye meno ili kuwaongeza urembo. Baada ya kutiwa mwanya wanakubaliana kufanya jaribio la kubainisha mwanya mzuri. Wanafikiana kuwa na mtihani wa kutema mate hadi ng'ambo nyingine ya mto. Aliyeweza kutema mbali kupitia kwa mwanya wake wa meno alikuwa atajwe kuwa na mwanya mzuri zaidi ya wenzake. Mweru msichana mmoja kati yao akawa pekee aliweza kuvusha mto mara ya kwanza na ya pili. Wenzake watatu wanapatwa na wivu na kupanga njama ya kumuua. Walimtupa Mweru kwenye shimo moja na kulifunika kwa jiwe katika maeneo ya milima yenye mabonde marefu. Walimwacha kule kisha walipofika nyumbani walindanganya kuwa aliwaacha, akatangulia na labda akaliwa na fisi. Wazazi wake wanaamini na kuishi kumwomboleza siku zote. Muda mrefu ulipita Mweru angali hai mle shimoni. Siku moja, inasadifu kuwa Nyaga, kakake, akiwa marishoni alikalia jiwe lililofunika shimo alimotupwa Mweru. Mbuzi mmoja alipomkasirisha Nyaga alimlaani kwa sauti kupotelea mbali kama Mweru wao. Mweru akasikia akiwa shimoni na kujibu kwa wimbo. Nyaga aliweza kutambua sauti ya dadake. Nyaga akawaarifu jamaa zake

nyumbani kisha kukapangwa shughuli ya Kwenda kuthibitisha na kumwokoa Mweru. Mweru aliokolewa na wanakijiji akiwa hai ingawa baadhi ya sehemu za mwili wake zilikuwa zimeoza na hata nguo kuisha. Mweru alitunzwa hadi akapata nafuu. Mweru alipopata nafuu aliwaandalia wenzake sherehe na kuwapa kinywaji spesheli kilichokuwa na mchanganyiko wa gudi ya kunasia ndege. Baada ya dhifa Mweru aliwasidikiza. Wakiwa njiani, wasichana wale watatu wanageuka na kuwa vipepeo.

### 4.4.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi

Katika misingi ya nadharia ya ujumi wa kinudhuma, matini simulizi hupangwa katika mistari inayopokezana, kuingiliana na kukamilishana bila kuzingatia kwa dhati mipaka ya kimatini. Hadithi hii ilipangwa katika mfumo huu kimakusudi ili kuendeleza ujumi. usimulizi ulitangulizwa kwa tukio la wema. Sehemu ya kati ikawa msukosuko wa kimaadili kwa wahusika kuingilia tendo la uovu kisha harakati za kupata haki. Hitimisho ikawa hukumu na hatima ya wahusika waovu kuangamia kama funzo. Tazama mtiririko huu wa matukio ufuatao:

**Tukio la wema:** Hadithi inatanguliza habari njema za wasichana wanne kutoka ukambani kuongezewa urembo. Kuongezewa urembo ni kitu cha thamani sana kwa wanawake katika jamii. Wasichana hao wanatiwa mwanya wa meno ili kuwa warembo zaidi.

> *Airitu mana ma Ikamba meerwa ni magacawe njarumi. Mathii gucawa magego.*
> (Wasichana wane kutoka Ukambani waliambiwa wangechongwa meno kuyatia mwanya wa Urembo. Wakaenda Kuchongwa Meno)

Zaidi, wote wanne walikuwa na ushirikiano wanapotiwa mwanya. Kwa Pamoja wanakubaliana kwenda mtoni kutathimini kiwango cha uzuri wa mwanya wa kila mmoja wao. Wanaenda pamoja mtoni na kushindana kutupa mate nga'mbo ya mto. Ushirikiano pia ni tukio la wema na la kuvutia katika jamii.

> *Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii, u ukaringia munyiri rugongo ruria atuike niwe ena njarumi I mbega. Na ururia akaguithia runciini atuike njarumi yawe ti mbega tucoke tugacawe riingi."*
> *Mathii riu macawa maca riu mathii muburoni uria meranite, makinambiriria gutua munyiri. Mau monthe matua matua airitu mathatu ukigwicaga runcini. Muiritu umwe wetagwa Mweru, agera wawe wakinya rugongo ruuria.*

(Baada ya shuguli hiyo kukamilika, waliambiana "Twendeni mtoni tuone nani ataweza kutema maji kupitia kwa mwanya wa meno hadi ng'ambo ya pili. Atakayefanya hivyo ndiye atakayesemekana kuwa na mwanya mzuri zaidi. Atakayeshindwa kufanya hivyo, asemekane kuwa na mwanya duni, hivyo arudi akachongwe tena.")

Walielekea katika ule mto waliokuwa wameafikiana wakaanza kushindana kuvusha mchirizi kwenye mto. Wasichana watatu wakajaribu ila hawakuvusha. Msichana mmoja aliyeitwa Mweru ndiye aliyeweza kuvusha hadi upande wa pili wa mto huo. Hao watatu wakasema "Lazima turudi kuchongwa tena. Hatuwezi kushindwa na mtu mmoja.

**Msukosuko wa mwenendo:** Mweru anapowashinda wenzake watatu unakuwa mwanzo wa chuki na utengano. Wasichana wenzake watatu wanapanga njama ya kumuua.

*Mathii kuri antu monete irima iraca muno muntu arikibingirwa ku akaurira ku. Mathii ri, mathiuba mbele ya mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku, na twekira mweru ku agakuira kuu.*

Wakaambiana, "Twendeni tufunue shimo kwa kuondosha lile jiwe tumrushe Mweru ndani. Na tukimtia mle, atafia humo. Kisha turejee nyumbani haraka sana. Tukiulizwa kuhusu habari yake, tuseme alitangulia na huenda alililiwa na fisi."

Wasichana waliokuwa na ushirikiano na waaminifu wanabadilika na kuwa wasaliti na wabaguzi. Wanamtenga Mweru kwa kuwa na mwanya mzuri kuwashinda. Wanakuwa waongo na kundanganya kuwa Mweru aliliwa na fisi baada yao kumrusha kwenye shimo. Wanamhandaa Mweru kuingia shimoni kwa ahadi ya kumtoa kwa kuvuta kamba lakini wanakosa kutimiza na kumwacha kufia mle ndani.

*Na twinukange na karugi muno, twathii tuge atiri, nuntu kwina mbiti, twaurua tuge nimbuga karirwe ni mbiti nuntu niwe enukire mbele yetu". Makinerana, "nitumuthairirie ii, turume mukanda, twaruma mukanda, muntu athungira akaburutwa ni antu mathatu akauma. Indi muntu wa cietu ambe athungire ari wa mbele, kenda mweru akarigia akiugaga akarutwa turege kumuruta."*
*Mabanga ugu. Mathungira ria mbele makirutanaga makirutanaga makirutanaga. Marutana monthe kinya ona mweru maruta. Macekera ria kairi. Mathii mathatu akirutagwa. Mweru arigia. Arigia ri, akiinamia mukanda arutwa ri, akunikirwa na ibari (ibiga)*

*Mweru atigwa kuu, atuura ku. Atuura ku ri, makinya mucii, maurua mauga "Mweru niwe winukire mbele yetu ii, nwakigua atunganire na mbiti ariwa"*

Wakasemezana, "Tumdanganye. Tuchukue Kamba. Mtu mmoja akiingia, anavutwa na wale watatu anatoka. Mmoja wetu atangulie ili Mweru aingie akiwa wa mwisho. Halafu tukatae kumwondoa mle. Wakapanga hivyo.
Wakaingia kwa awamu ya kwanza kila mtu akiviutwa na kutoka. Hata Mweru akatolewa. Wakarudia mara ya pili. Wa kwanza watatu wakatolewa. Mwerru akaingia wa mwisho. Akatikisha Kamba wamwondoe lakini wakamfunikia mle ndani kwa jiwe kubwa. Akabaki humo. Akakaa mle,
Walipofika nyumbani, wakaulizwa aliko Mweru wakasema "Mweru ndiye alitangulia kuelekea nyumbani. Huenda alikutana na fisi akaliwa."

**Harakati za kupata haki au ukombozi**: Nyaga kakake Mweru anamfokea mbuzi mmoja aliyemkasirisha huku akimlaani kupotea kama Mweru dadake. Mweru anayasikia maneno ya Nyaga na kumjibu kwa wimbo akiwa ndani ya shimo. Nyaga aliyasikia maneno ya wimbo wa Mweru na kujaribu kumfokea mbuzi yule wa kuirudia kauli ile tena. Mweru akamjibu tena kwa wimbo ule ule.

Nyaga ri, kathuura muno ni mburi kamiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."

*Nawe kaana karia gekaririte ibaari riri, gatikumenya kana ni ibiga rikunikanie.*
*Gekarite o baria Mweru ari. Mweru egua akinaina:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*NItwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

*Nyaga abnga "ari kambire mburi iria bu ringi"*
*Amiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*
*Akinegua:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*NItwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*

*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

Mweru alikuwa na kakake aliyefahamika kama Nyaga. Alikuwa akichunga mifugo malishoni. Siku moja akiwa anawachunga mifugo, mbuzi mmoja akamkasirisha mno. Akamwambia, "ewe mbuzi potelea pote kama yule Mweru wetu aliyetokomea toko!" Kijana huyu alikuwa amekalia jiwe pasi kung'amua kuwa chini ya jiwe hilo palikuwa na shimo. Humo ndimo alimokuwa Mweu. Akasikia Nyaga akimfokea mbuzi yule.

Mweru akaimba:

Kanga i kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Nyaga akaamua, "Ebu nimwambie mbuzi yule hivyo tena." Akamwambia, "Ewe mbuzi potelea pote kama yule Mweru wetu aliyetokomea toko!"

Akasikia:

Kanga i kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Nyaga akapeleka habari za Mweru kuwa hai. Kupitia babu yake, jamii yake ikaungana na kuanza harakati za kumtoa Mweru ndani ya shimo ili kumwokoa. Wakamfuata Nyaga na kupata alimokuwa shimoni.

*Icue akinamera "Taciani nimwireni, ruyu ruyu ruyu, mwithiranie antu ma mena binyama gutegatekia ibari riu negua nirio akunikiritwe nario. Nuntu Nyaga tiika atikumenya baria ibari ririkunikire na niwe urithagia. Athii atwonie, indi untu tukathii, nuntu mwana unu niaina akauga niathiritie nguo, urume anwa rucuka kana nguo yaku ukamwikirira ii? Na ukie gakie wikire katheguni na uthii na gakuniko ga gukuniika naga kumukundia nako. Nuntu mwana unu, ari bo ugu nyaga ambira. Tigani kuukagia untu na karugi ugu. Mwana, atirigwa ni untu. Na mwana niwe uririkanaga."*
*Merana, "nibu tukathii kirauko."*

*Ng'ina auga, "ana ngakia tene muno. Wegua nibu ri, tukathii na ngaceria antu. Antu matiura.*
*Riu mabanga ugu na icue. Riu Nyaga ana ataringwa ringi. Akumama cacawa. Gwakia kirauko erwa "Nyaga tuthiiugu uraugire kenda umwigua akiaria" Maukira tene mathii.*

Akamwita, "Babu," akaitikia. Akamwambia, "wajua, Mweru angalipo, Japo huwa tunaambiwa kuwa aliliwa. Yumo humo chini. Nilikalia jiwe nikaskia akiimba huko chini. Aliimba mara mbili babu. Nilipowaambia wazazi wangu wakaanza kunipiga. Ndiyo maana ninalia."

Babu akamwambia, "Hakuna tashwishi. Binafsi nitamwambia," Wakaenda hadi nyumbani. Babu akawauliza, "Eti mmemwadhibu Nyaga kwa nini?" "Ametwambia mambo ya kishetani; eti Mweru angalipo hali twajua vyema kuwa alikufa." Baba akajibu. Mama yake alipoulizwa, alijibu, "anatutonesha kidonda kwa kutuambia kuwa Mweru angali hai nasi tunajua kuwa aliaga dunia kitambo."

Babu akawaambia, "Ebu niwaambieni, kesho, tafuteni watu wenye nguvu wa kusongeza jiwe hilo nililoskia Mweru amefunikiwa nalo. Nyaga anafahamu lilipofunikwa shimo. Yeye ndiye hupeleka mifugo malishoni. Aende atuonyeshe. Mtoto huyu anaimba akisema kuwa nguo zimemwishia, Beba angalau nguo ya kumvisha. Saga uji utie katika dundu. Beba kizibo cha kumnywesha uji nacho, Maadamu Mweu angalipo kama alivyoniambia huyu kijana. Mtoto ndiye ajuaye, ndiye akumbukaye. Wakakubaliana kuwa wangeenda asubuhi.

Asubuhi ilipofika watu wakaandamana na Nyaga hadi malishoni. Nyaga akakalia jiwe na kuyarudia maneno yake. Mweru akasikia na kumjibu kwa wimbu huku watu wasikiliza. Wakathibitisha ukweli wa madai ya Nyaga. Watu wakafunua jiwe na kumwona Mweru. Mweru akafutwa kwa kamba na kuokulewa akiwa hai ila baadhi ya sehemu za mwili wake zilikuwa zimeoza.

*Gwakia kirauko erwa "Nyaga tuthii ugu uraugire kenda umwigua akiaria" Maukira tene mathii.*
*Mathii makinya nabo, nau Nyaga arithagia, Nyaga athii ekarira ibiga riria. Antu mari au? Mathikiritie muno megua kana ka Nyaga amabenagia Nyaga auga "Tui Mburi iria uroura ukaura ta Mweru wetu uria waurire."*
*Makithikiriria bu makwaragianteto megua:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*NItwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

*Antu kugaa na kwigua ugu, makunura ibari mari na mikanda iri. Muntu umwe athungirua kuna mukanda, obereretwe mbaru. Athii, oberera Mweru, anenkererwa erwa "riu twitithirie we."*
*Ambiriria kumurutha weega, ameera "Nkumuthaika weega muruteni riu,"*
*Mweru arutwa akinya nthi nawe ekirwa mukanda nawe athaikwa arutwa.*

Kulipopambazuka, Nyaga akaambiwa, "Utaenda useme hivyo ulivyosema ili tumsikie Mweru akizungumza." Wakaamka mapema na kusanzuka. Wakafika Malishoni Nyaga akakalia jiwe lile. Watu wakatega masikio yao nchi! Nyaga akasema, Ewe mbuzi potrelea pote kama yule mweru wetu aliyetokomea toko!"

Wakasikia: Kanga I Kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Watu wale waliposikia hivyo, wakaondosha jiwe. Walikuwa na Kamba mbili. Mtu mmoja akaingia humo na Kamba moja. Akamfunga Mweru huku naye amefungwa kifuani. Baada ya kumtayarisha vizuri, aliwaambia, "Tayari nimemfunga vizuri. Mvuteni sasa."
Mweu akavutwa akafika nje.

**Hukumu na hatima ya mui**: Tambiko na adhabu zinaandamana, nguvu za maumbile zinatumika kubaini haki na kutoa hukumu kwa usawa. Mweru anawaandalia wasichana wenzake kinywaji chenye gudi ya kunasia ndege baada ya kuwaalika na kuwapokelea kwake. Anapowasindikiza wanageuka kuwa vipepeo kama adhabu na hatima ya uovu wao.

*Riu ri, amakinyia menuka. Akinamatwira kiatho na auke. "Muce na nkegua nimukuirite ii, wana iria ni mukethira riri bo." Amera "nibu tugaca gugukethia Mweru."*
*Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urimbo.*
*Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugag makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe*

Mweru akawasindikiza warejee makwao. Akawakaribisha tena kwa mwaliko wa siku mbili ambazo zingefuata. Akawaambia, "Karibuni, Nitawaandalia maziwa na uji wa kusagwa." Nao wakasema, "Tutakuja

tukusalimie Mweru," Mweru alikuwa amekasirika. Alitaka kulipiza kisasi kwa kuwaliga.
Akabaki. Akatafuta rojorojo ya kutengeneza gundi ya kuwanasa ndege kutoka kwenye miti ya kila nui. Angeitia rojorojo hiyo kwenye maziwa ambayo angewapa. Siku ikafika. Wakaja Mweru akawapokelea tena. Akawapa maziwa yenye rojorojo sumu naye akayanywa yale salama wasijue. Wakanywa. Baadaye akawaambia, "Twendeni niwasindikize." Akawasindikiza. Walipofika njiani, wote wakageuka na kuwa vipepeo isipokuwa Mweru.

### 4.5 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya chura na mbuni

Sehemu ya mtiririko wa hadithi ya Hadithi ya chura na mbuni ilishughulikia muhtasari wa hadithi kisha mtiririko wa matukio kwa ujumla. Sehemu ya kwanza ililenga muhtasari kisha sehemu ya pili ikajikita kwenye mtiririko.

#### 4.5.1 Muhtasari wa hadithi ya Chura na Mbuni

Wanyama wote walijumuika Pamoja, Wakakubaliana kila mnyama aje na kuni. Wanyama wote wakabeba kuni, Naye chura akabeba kuni za mti wa 'muboru" Akaenda huko. Wakachinja.Walipochinja wakaamua wachome nyama. Wakazichoma nyama wakaanza kuzila. Chura akadharauliwa na Wanyama wote na wakakosa kumpa nyama walizozichoma. Chura alighadhabishwa sana na tendo hili la wenzake. Ndipo chura akaamua kulipiza kisasi kwa kuhakikisha kuwa wanyama hawakupata maji ya kunywa baada ya kula nyama. Alilani mito yote ikauke na ikawa vile.

Baada ya wanyama kumaliza kula nyama walibanwa sana na kiu, ikawalazimu wamtafute chura wambembeleze ili aamuru maji yarudi kwenye mito. Wanyama walimwendea chura kuomba msamaha lakini kwa maringo, mbuni aliapa kuwa hawezi kuyanywa maji yalikanyagwa na chura hata akifa. Kwa huruma zake chura aliweza kuyareejesha maji kwenye mito. Mbuni aliamua kwenda kuyanywa maji aliyoyakataa, alipopatwa na chura akiyanywa, chura alikasirika na kumngonga mbuni na kuuvunja upembe wake.

Mbuni alikasirika sana na tendo hilo na ndiposa akamlaani chura. Kuanzia siku hiyo chura alianza kufura miguu na pia watoto wake waliaga kila mara alipowazaa. alioona kuwa mabo yamezidi aliamua kwenda kumtafuta mbuni ili amwombe msamaha na

aondolewe laana. Alibeba mafuta yakumwagilia kenye upembe wa mbuni uliovujika na akasamehewa na mbuni na kuondolewa laana.

Chura akaahidiwa kuwa kuwa hata wanawe angewapata wakiwa wazima chura naye akamwambia mbuni awe akinywa maji.

**4.5.2 Mpangilio wa Matukio Kiujumi**

Mpangilio wa matukio katika hadithi hoii pia ulibainika kuwa saw ana ule hadithi tangulizi hapo juu. Usimulizi ulianza kwa mchakato wa tukio la wema kisha kufuatwa na msukosuko wa kimienendo.

**Tukio la wema**: Hadithi inaanza kwa tukio la wema au habari njema: Urafiki unaanza baina ya chura na wanyama wengine. Wanyama wote walijumuika Pamoja. Wakakubaliana kila mnyama aje na kuni. Wanyama wote wakabeba kuni. Naye chura akabeba kuni za mti wa 'muboru" akaungana nao. Wakachinja.Walipochinja wakaamua wachome nyama. Wakazichoma nyama wakaanza kuzila. Umoja ni wema ambao unakuwa kama kiunzi cha kuishi vyema kwa pamoja. Umoja huu unazua wazo nzuri la kuungana pamoja na kuchoma nyama ili wale pamoja, wazo mzuri pia. Hatimaye wanyama wote wanaleta kuni na kuchoma nyama kwa pamoja na wanaanza kula. *Nyamu ciothe ciakua nku, riu, nako kaura gakinauna tuku twa miboru. kathii nabo. Kathii ri, mathinja. Mathinja matwika nyamu ino nikaigwokia nyama. Ciokia nyama gwokia gwokia gwokia. Ciokia ciambiria kuria*.

**Msukosuko wa mwenendo:** Urafiki unajenga ushirikiano baina yao lakini tunapata chura aliwachukiza wanyama wengine kwa ajili ya kuleta kuni mbovu hivyo wote wakachukizwa na hili jambo. *Riu kaura gakinamenererua ni nyamu cionthe gakinaurwa,* (Chura akadharauliwa na Wanyama wote akaulizwa, "Nawe chura uso makalio umepeleka hizo kuni zako wapi?" Hatutakupatia nyama zetu.)

Chura anatengwa na wanyama wengine anaanza kubadili mwenendo wa uaminifu katika urafiki wao.

Chura akasema,

> "Nitakaa hapa nione." Chura akakaa hapo. Wanyama wakachoma nyama. Wakaanza kula. Wakala. Wakashiba. Wakaanza kupachika vijiti kwenye nyama zingine kutokana na shibe.

> Chura naye hakupewa akaambiwa, “Chura aso na makalio amekuja hapa kufanya nini?” Chura akakasilika.

Wema na ubaya zinaanza kuvutana. Tamaa na ubinafsi zinaanza kumtawala kisha kubalidilika kuwa mnafiki na Urafiki unaanza kuyeyuka kwani chura alikasirika na kufanya mito yote ikauke.

Chura akakasirika. Akawauliza,

> “Hivi, mnaponiambia hivyo mtatoa wapi maji ya kunywa?” “Tutakunywa mtoni.” “Na nikiikausha?” “Kwani utakausha mito yote?” “Na hivyo mimi nitaenda nikaushe mito, nanyi hamtapata ya kunywa. Nione iwapo nyama hizo zenu zitamfaa bila kuyanywa maji.
>
> Wanyama wale wakaanza kumcheka chura wakimwambia, “ata ukaushe, utakausha yote. Tutayanywa maji. Huwezi kuikausha mito yote. Nenda uikaushe basi.”
>
> Chura akaondoka hapo akiwa amekasilika sana kwa kuwa alinyimwa nyama kama mzaha. Akaenda akakausha mito yote. Akabakiza mto mmoja wenye maji kiasi kidogo sana, maji yaliyokuwa na ndongo.
>
> Wanyama walienda katika mito yote kutafuta maji wakakosa. Walikuwa wamekabwa na kiu hata wakajuta kuzila nyama zile. Nusura wafe kutokana na kiu. Walipata maji yale yenye dongo, hayakunyweka

Pia, baada ya chura kunyima mbuni maji, uovu uliendelezwa na mbuni kwani alimlaani chura na ndipo vikembe vya chura vilianza kufa.

**Harakati za kupata haki au ukombozi**: tunapata kuwa wanyama wanaamua kuondoa huu uovu kwa kumbebeleza chura mwovu ili akubali kuwarejeshea maji kwenye mito. pia, chura anaamua kusuluhisha mgogoro wake na mbuni ili aondolewe laana kwa kufanya tambiko.

> Chura akafahamu kuywa lahana ya mbuni ilikuwa imemfika. Akasema, “Sasa nitaenda nikiulizia aishiko mbuni nikiwa na vizibo saba vya mafuta ya karafuu.”
>
> Chura alikata vijiti vya karafuu na kutia yale mafuta humo. Akaunganisha hadi vikafika saba.
>
> Akaanza safari. Alipokutana na Wanyama njiani akawambia. Muthunthuri muthunthuiga, kwa mbuni ni wapi? Muthunthuiga, nipeleke vyombo vya mbuni, muthunthuiga wanangu wamekwisha, muthunthuiga, wameugua baridi na homa ya malaria, muthunthuiga. Chura akaimba, “muthunthuri….” Mbuni akatoka. Akamuliza, “umekuja kwangu kufanyani na tulikosana?” Chura akamwambia kuwa alikuwa amekuja wapate kusameheana. “Sasa mbuni tusameheane.” Chura akaulizwa iwapo alikuwa na vile vizibo saba akasema vipo. Chura akaambiwa na mbuni, “Ebu ng’oa upembe huu.” Akang’oa. Akaambiwa auweke chini akafanya hivyo.

**Hukumu na hatima ya mui**: Adhabu inatokana na uamuzi wa nguvu za maumbile katika tambiko. Chura wanafanya tambiko la kuondolewa laana na mbuni.

> Chura akaimba, "muthunthuri…." Mbuni akatoka. Akamuliza, "umekuja kwangu kufanya nini na tulikosana?" Chura akamwambia kuwa alikuwa amekuja wapate kusameheana. "Sasa mbuni tusameheane." Chura akaulizwa iwapo alikuwa na vile vizibo saba akasema vipo. Chura akaambiwa na mbuni, "Ebu ng'oa upembe huu." Akang'oa.Akaambiwa auweke chini akafanya hivyo. Kila alipotia kizibo kimoja cha mafuta katika upembe alivyoambiwa na mbuni, kiwavi kilitoka. Alipotia kizibo cha saba, kiwavi cha mwisho kilitoka na chura akapona. Wakasameheana. Mbuni akamwambia kuwa ata yeye amepata shufaa. Chura akaahidiwa kuwa kuwa hata wanawe angewapata wakiwa wazima chura naye akamwambia mbuni awe akinywa maji.

Wema unashinda uovu hivyo ushirikiano kurejeshwa miongoni mwa wanajamii. Mpangilio huu unatawaliwa na wema, mvutano wa ubaya na idili za jamii. Adhabu na njia ya kubaini mwenye haki inategemea imani na itikadi za jamii. Kutokana na matukio katika hadithi ya chura na mbuni, inabainika kuwa Wachuka wana imani kwamba ukiwa mwenye haki utatetewa na hali za kimaumbile kama vile uwezo wa kurejesha maji na pia kurejesha pembe za mbuni kupitia tambiko. Tunapata kuwa vikembe wa chura wanaponea na pia mbuni kuweza kupata maji. Inavutia kuona ukweli unabainika na wema kutawala dhidi ya uovu.

### 4.6 Mtiririko wa Matukio Katika Hadithi ya tembo na fisi

Sehemu ya mtiririko wa hadithi ya Hadithi ya ilishughulikia m Hadithi ya tembo na fisi muhtasari wa hadithi kisha mtiririko wa matukio kwa ujumla. Sehemu ya kwanza ililenga muhtasari kisha sehemu ya pili ikajikita kwenye mtiririko.

#### 4.6.2 Muhtasari wa Hadithi ya tembo na fisi

Tembo na fisi walikua marafiki. Wakaafikiana wawe wakilala katika pango moja. Tembo alikua na wanawe na fisi vivyo hivyo. Wakaishi kwa muda mrefu kwa lile pango moja. Walikua marafiki wa kufa kuzikana. Siku moja, tembo akamwambia fisi, "baki na wanangu niende mahali Fulani." Fisi akakubali. Tembo akaenda mahali, huko mbali walikoishi tembo wengine wengi.

Tembo alipoenda, alianza kuishi na tembo wengine. Hakurudi. Alijiambia, “maadamu wanangu wako mikononi mwa fisi ambaye ni sahibu yangu nitawapata nikirejea. Watakua wakila Pamoja na wana wa fisi.” Aliishi na tembo wengine siku ayami bila kurejea pangoni. Kila jioni, kikembe cha fisi kingeanza kulia na kusema, “m…m…m…m… ninalilia mwana wa ndovu.” Fisi angemwambia, “ng’ata ila usimg’ate kwa nguvu.” Papo hapo, mwanatembo angeliwa bila kusazwa na vikembe vya fisi.

Mchana, walishinda vizuri wakila pale malishoni. Kila magharibi waliporejea pangoni, mwanafisi angelia ili aruhusiwe kumla mtoto wa ndovu. Wakazoea kufanya hivyo kila uchao. Ndipo mwanatembo akaamua kwenda kumtafuta mamake. Alipofika pale lakini hakuweza kumtambua mama yake miongoni mwa wale ndovu wengi. Akaona wimbo ungemsaidia akaimba, alienda akiimba hadi alipomfikia mamake ya cianyaga. alipompata alidai anyonye kwanza kisha akamweleza mambo yalivyokua tangu alipowaacha na fisi pale pangoni. kisha, wakashika safari kurejea walikoishi mle pangoni.

Ndovu alisubiri hadi usiku huku akidai fisi amwaambie waliko wanawe. Fisi alimwambia asubiri kidogo wanakuja. Aliendelea kuitisha wanawe hadi akapandwa na mori. Fisi akanyamaza. Akashikwa na tembo. Akakanyangwa akafa. Wanawe wakashikwa. Wakakanyangwa wakafa.

### 4.6.3 Mpangilio wa Matukio Kiujumi

Mpangilio wa matukio pia uliradidi mtindo ule ule wa hadithi zilizochanganuliwa hapo juu. Dhima kuu ya kimaadili ilionekana kutawa mtiririko wa matukio.

**Tukio la wema:** Hadithi inatanguliza suala la udugu wa fisi na tembo.

> *Njogu na mbiti ni ciatumite urata. Cierana, riu niilalage irimani rimwe. Ciatua kuraraga irimani rimwe. Njogu yari na twana twayo na mbiti yari na twana twayo.*
>
> *Riu, ciekara muno muno muno ikilalaga ilimani rimwe. Ciikarite muno, ntuku imwe njogu niyerire mbiti nuntu numendanite muno, “Ntigirwa na ciana. Nthii bantu nkwenda kuthii.”Mbiti yamira, “nibu.” Njogu yathii. Guntu kuraca. Guntu ku njogu i mingi muno ciekaraga.*

Tembo na fisi walikua marafiki. Wakaafikiana wawe wakilala katika pango moja. Tembo alikua na wanawe na fisi vivyo hivyo. Wakaishi kwa muda mrefu kwa lile pango moja.

Walikua marafiki wa kufa kuzikana. Siku moja, tembo akamwambia fisi, "baki na wanangu niende mahali Fulani." Fisi akakubali. Tembo akaenda mahali, huko mbali walikoishi tembo wengine wengi.

**Msukosuko wa mwenendo:** fisi anaanza kubadilisha mwenendo. Anawala watoto wa tembo pamoja na wanawe. Ulafi wa fisi na wanawe unawafanya kuwala wanatembo wote nakusaza mmoja tu.

**Harakati za kupata haki au ukombozi**: mwanatembo anaaza safari ya kwenda kumtafuta mamake aliye malishoni, anaanza kuimba wimbo kwa sauti ili kumtaarifu mamakeke aje amkomboe kutoka mikononi mwa fisi.

*Riu, kaana ga kari na nthoongo, kona matigara mari mairi. Kandika riu, "gatuthii tutigare na ciana ino, indi untu twathii kuria, nuntu ninkumenya narega kuriwa, nig aka kangi gakaliwa nuntu turi mairi, na tucioke tuthire, niu nintoroka, ngacerie ku maitu ekaraga. Na tukathii kuria wega muno kithakani, indi niu, nkaricaga ni kuraja muno. Ikinuka, tinicuma thuuba. Riu gaka gakinya kariwa, niu, maganceria mbure. Metere minuka, timinunka. Kana karia ka nthongo kabanga ugu. Ciathi kuria. Kibwai gigikinya ri, cionthe ciice ciinukite cionthe ri, cienuka ciici kari wabo. Karia nako gatinda kuthii. Cienuka, ciathii. Kana karia na kathii karira, " m…m..m…m…!" "ni indu ukulilila?" "Ni rutende rwa njogu nkulilila." "kutha na utigakuthe wica." Kaana karia kaliwa*

Mwanandovu aliyekuwa na chongo akatanabahi kuwa wamebaki wawili tu. Akasema, "tutaenda malishoni kula na wana wa fisi. Lakini, kwa kuwa sijui iwapo ni mie au ndugu yangu ataliwa na fisi nitatoroka. Sitasubiri tuliwe sote. Nitaenda kumsaka mama aishiko. Nitakua nikila mbali na fisi pale kichakani. Sitawafuata wakirejea pangoni. watamla ndugu yangu ila mimi watanifuata wanikose. "akaamua.

Wakaenda malishoni kama ilivyokuwa mazoea. Yule chongo akasafiri mchana kutwa. Ndugu yake akarejea pangoni na kuliwa na wana wa fisi.

**Hukumu na hatima ya mui**: Adhabu ya kushambuliwa kwa fisi inatekelezwa. alishambuliwa kwa mateke na kukanyagwa na ndovu hadi akafa.

*Kaana karumirira ng'ina. Ciathii ciathii ciathii… Ciakinya kibwai. Nuntu ni kuraca. Ciakinya kibwai ciathii, nuntu ni kibwai ri, njogu*

*nikwona twana twa mbiti. "Ambu Njogu ciana ciakwa ri, ciiku?" "Niciicite, kaikuria." Mekara mekara mekara.*

*"Mbiti, ciana ciakwa ciiku?" "Nimacite. Tia cu. Mari nau kithakani i, indi nimacite."*

*Njogu yekara yekara yekara. Yona gutukire, kwabetukania. "Ntigukuria mbiti, ciana cia ri, ciiku?" "Nimacite metaetarere." Mbiti ni ciana ciakwa nkwenda n aguti gwetaeterera ringi. Guti mwana unkigua ari kithakani thaa ino. Cionthe niciinukire. Ga ciaku ciinukire ciakwa ciatigwa ku?| |Wegua nukwenda wega, ciana ciakwa lete."*

*Mbiti yakira. Mbiti yambatwa. Yakinyithanua ni njogu yakua. Twana twambatwa. Twakinyithanua twakua. Rugono rukinathira*

Mwanandovu akamfuata mama yake wakafika huko machweo kwa kuwa kulikuwa mbali. Ndovu akawaona wana wa fisi. "Kwani wanangu wako wapi?" "Wanakuja wanakula."
"Wanakuja. Hawajarejea. Wako malishoni lakini wanakuja."
Ndovu alisubiri hadi usiku. "Fisi, niambie waliko wanangu." "Subiri kidogo wanakuja."
"Ninataka wanangu. Sitasubiri tena. Hakuna mwana awezaye kuwa kichakani wakati huu. Wote washarejea. Nipe wanangu kabla ya mambo kwenda mrama."

Fisi akanyamaza. Akashikwa na tembo. Akakanyangwa akafa. Wanawe wakashikwa. Wakakanyangwa wakafa.

Kutokana na ngano zilizochanganuliwa Sehemu hii iliweza kubaini kuwa mtiririko wa matukio kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka hufuata utaratibu wa ngazi tatu za matukio. Utangulizi kuchukua nafasi ya tukio la wema, kati kuwa sehemu ya msukosuko wa mwenendo na hitimisho kuwa harakati za kupata haki au ukombozi. Kwa jumla, mtitiriko wa matukio kiujumi uliweza kubainishwa na kuthibitishwa katika ngano zote .

# SURA YA TANO

# SIFA ZA WAHUSIKA WA KISIMULIZI KATIKA NGANO ZA WACHUKA

## 5.1 Utangulizi

Sehemu hii ilishughulikia sifa za wahusika wa kisimulizi katika ngano za wachuka na kubaini mchango wake katika kupamba ngano za Wachuka. Wahusika mbalimbali walirejelewa kutoka ngano anuwai zilizoteuliwa kimakusudi. Utaratibu wa uchambuzi ulizangitia hadithi ya fisi na kindi, Ngongoana na Gacinci, Wasicha wanne wa ikamba, chura na mbuni na mwisho hadithi ya fisi na mbuni.

## 5.2 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Fisi ya Kindi

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) wahusika ni dira msingi katika kazi za kifasihi kwa sababu huwa waendelezaji wakuu wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira ama maudhui ya kazi husika. Kadhalika, kama asemavyo Wamitila (2013), wahusika wanyama, mazimwi, majini, wadudu na hata binadamu ni wahusika wa kisimulizi wanaojitokeza katika fasihi simulizi. Katika hadithi ya fisi na kindi wahusika wote ni Wanyama. Kuna muhusika fisi na mwenzake kindi. Katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci wahusika ni mesto wa binadamu na majitu. Hadithi ya wasichana wanne wa ukambani inahusisha wahusika binadamu na wanyama. Katika hadithi ya chura na mbuni wahusika ni wanyama na pia katika hadithi ya fisi na tembo. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wahusika huchanganuliwa kwa namna wanavyoingiliana na dhamira. Hili hutokana na maneno, tabia na matendo yao.

Kwa mujibu wa nadharia ya ujumi wa kinudhuma Matini simulizi huwa na matumizi maalum ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Wahusika katika ngano simulizi za Wachuka waligawika katika kategoria mbili kuu kimatendo. Wahusika wawi na wahusika wema.

### 5.2.1 Wahusika Wawi

Wahusika wawi wanajitokeza katika katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Kwenye utangulizi wahusika wote wanaaanza wakiwa wema. Hadithi inapotangulia

kwa tukio la wema wahusika wote wanakuwa sawa kimienendo na hulka. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi, fisi na kindi wanakuwa na sifa sawa. Wenye upendo: waanza kama marafiki "*Mbiti na kabare ciatumire urata*". Wenye ushirikiano: wanashirikiana kupalilia konde na kupanda kunde

> *"...cierana niciuge itema, ciauga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko.*"

Sehemu ya pili ya matukio ya hadithi inakuwa msukosuko wa mienendo. Muhusika mmoja anaanza kwenda kinyume na matarajio. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi, fisi alichukua nafasi ya muhusika muwi. Kunde zilipokomaa fisi alianza kwenda kinyume cha urafiki wao na kindi kwa kuanza ujanja na ulaghai

> "*Nthoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na mbiti. Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria kabare gatuire.* Fisi aliacha kuwa mwaminifu na kuwa mwongo "*Kabare ntuku ingi kakithii kethiria kethiria nthoroko ciako iri bakubi guthira, kamiuria "mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga n ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?" ...Aari aari ntamwona. Ntamwona. Ntamwona."*

(Kunde zilipokomaa, kindi akawa akienda kuchuma zake. Kila akirejelea alikutana na fisi.)

Fisi naye alizoea kuchuma kunde palepale alipochuma kindi. Kindi alipoelekea kuchuma tena, akagundua kuwa fisi hakuchuma kwake bali katika shamba la kindi. Kindi akaenda akamuuliza fisi , "fisi, maadamu ni wewe ulienda shambani mwisho, ulimwona aliyechuma kunde zangu?" "La! La! Cheupe cheupe, sikumwona. Kila siku, kindi alipochuma kunde zake ,fisi akamfuata, naye akazichuma.Kwa fisi kunde hazikuchumwa; ni kwa kindi tu za fisi hazikuguswa kamwe Hazikuchumwa.)

Fisi alikuwa mwenye tamaa, mlafi na mbinafsi. Alikuwa na shamba lake la kunde zilizokomaa wakati mmoja na zile za kindi lakini alitamani zile za mwenzake hadi kuwa mwizi .Fisi alifikia kiwango cha kuwa nafiki. Wakati wa kuruka mto anaendelea kuruka huku akijua kuwa ndiye mwizi. Alipoanguka mtoni mara ya kwanza aliwaomba wenzake kumtoa kwa kuwa alitumbukia baada ya kukosa kujiandaa vyema. Alipoanguka tena alisisitiza kuwa bado hakuwa amejitayarisha ingawa alijua ni kwa sababu ya kuwa mwizi.

> *Mbiti yagamba runcini butu! Yauga, "Ruutana ndutani ii, gantatubite wega Mbiti cietikira ciaruta Mbiti. Aya! yarutwa ri, Kabare kerwa, "ruuga ringi riu nuntu mbiti yauga nika itarugite weega, iruge weega." Kaina;*
>
> *Ntarumaa x2*

*Muthororoko x2*
*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwaara.*
*Kabare ri, karuga gakinya rugongo ruria.*

*Mbiti yambiria gutantaura;*

*Ntauma x2*
*muthooko x2*
*wa muu wa kabare Giinci kiiru ntwara*

*Yagamba runcini nku! Yerwa riu mbiti i cingi,*
*"Ai nee riu ni weu wiite." Yauga ari rutaana ndutani ii gantatubite weega ri, tingwa ku."*

(Fisi akaanguka majini chubwi! Akasema, "Tafadhali niondoeni. Sikuruka vizuri." Fisi wengine wakakubaliana wakamnyanyua. Alipotolewa, Kindi akaambiwa aruke tena kwa vile fisi alikuwa amedai hakuwa ameruka vyema, ili aruke vizuri.

Kindi akaimba:

Sikula x2

kunde x2

Za ndugu fisi Ginci kiiru nsombe

Kindi akaruka akafika upande wa pili.

Fisi akaanza kugugumiza:

Sikuax2

Kunde x2

Za ndugu kindi Ginci kiiru nombe

Akaanguka majini tena, chubwi!

Fisi wengine wakamwambia, "Hivi ni wewe mwizi wa kunde," Akasema, "Hapana.Tafadhli nitoeni sikuruka vizuri. Nikichupa vizuri, sitaanguka mtoni.")

Hatima ya mhusika muwi ni maangamizi huku ukweli ukibainika na wenye haki kuipata. Fisi alianguka mtoni mara ya tatu kisha wenzake kumwachilia kufa maji ili apate adhabu na wengine wajifunze kuwa na adabu:

*"Mbiti yagamba runcini ringi nku! Yagwa runcini. Yambiria gukiriria tuguru, "Ndutani rutaani ntantubite wega. Ti niu. Ti niu. Ti niu. Ndutani ntatubite weega."*
*Mbiti ri, yerwa yerwa ni mbiti i cingi atiri, "tutikuruta ni weu wiaga kabare. Mbiti ikinatwarwa ni runci.*

("Alipoanguka majini akaanza kuinua miguu, "Nitoeni tafadhali. Sikuruka vyema." Fisi wengine wakamwambia, "Hatutakutoa. Ni wewe huiba kunde za kindi." Fisi akasombwa na maji*.")*

Sifa mbaya za fisi kama mhusika mui zinaichochea hadhira kuchukia kuwa mwovu katika jamii na kupenda kuwa mwandilifu na mwema. Muhusika mui katika hadithi hii anaipamba hadithi kwa kuonyesha nguvu za matambiko ya jamii kama ala kamili ya kupata haki. Fisi anashindwa na nguvu za tambiko la kuruka mto kisha haki na ukweli kupatikana. Hatima ya mhusika mui ni maangamizi. Fisi anatumbukia mtoni na kufa maji huku wenzake wakimkashifu

### 5.2.2 Wahusika Wema

Wahusika wema wanajitokeza kama wahusika bapa. Wanadumisha umbo lile lile la kimienendo kuanzia uatangulizi hadi kwenye sehemu ya hukumu. Wao ndio wanahujumiwa na wahusika wawi. Kwa mfano katika hadithi hii ya fisi na kindi. Kindi anachukua nafasi ya muhusika mwema. Analaghaiwa na fisi *“Thoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na Mbiti. Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria kabare gatuire.”* Kindi alikuwa mwaminifu. Alikuwa akichuma mbaazi kwake bila kutamani za mwenzake “*Mbiti nitua gwa Kabare. Kabare nako nigatua gwake, Gwatwika riu cia mbiti itigukomwa, na tintue.*” Kindi alijitokeza kama mjinga. Hang’amui kwa haraka kubadilika kwa tabia ya fisi. Hatambui mapema hujuma na ulaghai wa fisi hadi pale mbaazi zinaelekea kuisha shambani

> “*Riu wa ntuku kabare gakithii mbele gagitua. Mbiti ikiuma thuuba. Magitungana. mbiti ikithii, igitua. Kabare ntuku ingi kakithii kethiria kethiria nthoroko ciako iri bakubi guthira, kamiuria “mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga na ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?”*
> Akamuuliza, “Fisi eti huwa unaniambia huwa humwoni mtu ambaye huiba kwangu n ani wewe tu huwa nakutana nawe? Hujawahi kumwona mtu akizichuma hizi mbaazi zangu ambazo zaelekea kuisha?

Kindi alikuwa mwenye busara. Fisi alipokana kuwa hajawahi kumwona aliyekuwa akichuma kunde za kindi, kindi hakuzozana naye. Alitumia mbinu rahisi na faafu ya kukabili mzozo baina yake na fisi. Alipendekeza tambiko la kuruka mto ili kutambua mwizi bila maonevu.

> *Amwira, “riu, nitutue kiatho na auke. Withiranie mbiti cionthe nan mbithiranie tubare tuunthe. Tuthi muburoni witagwa Ginci kiiru. Tuthii tutube. Uria ukagwa ku, niwe ukamenyeka niwe wiaga nhtoroko cia uria wingi.”*

> (Akamwambia, "Sasa, tupange miadi ya kesho kutwa uwalete Pamoja Fisi wote,nami niwalete kindi wote. Twende katika mto wa Ginci kiiri .Twende turuke. Yule atakayeanguka majini ndiye mwizi aibaye kunde za mwenziwe.")

Kindi alikuwa mpole. Baada ya kugundua kuwa fisi alikuwa akichuma kunde kwake hazua urugu wala fitina. Alimhoji fisi kwa upole.

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Kindi aliruka mto Ginci Kiiru mara tatu mbila kutumbukia. Wema wake unamwepushia adhabu na kuangamizwa na nguvu za tambiko. Muhusika mwema anaipamba hadithi kwa kuonyesha kuwa haki inaweza kupatikana bila hiana katika jamii. Anaonyesha kuwa mbinu za matambiko jadi zinaendeleza usawa na kupatikana kwa ridhaa kamili baada ya kuhujumiwa. Fisi ananaswa huku kindi akapata uwezo wa kuepushiwa adhabu.

### 5.3 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Ngongoana na Gacinci

Wahusika katika hadithi hii walikuwa Pamoja na Ngongoana, Gacinci, kaka yao, zimwi na wacheza ngoma. Wahusika hao waligawika katika mikabala miwili. Wawi na wema.

#### 5.3.1 Wahusika Wawi

Wahusika wote wanatanguliza hadithi hasa kwa habari njema. Wahusika wawawi wanajitokeza katika katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Wahusika hao ni wale wanaosambaratisha mshikamano wa jamii. Mwanzoni Ngongoana na Gacinci wanaishi kwa ushirikiano mkubwa ingawa ni mayatima "*Kwari na Ngongoana na Gacinci. Muntu na muru wa ng'ina."* Wanakaa pamoja kule nyumbani na kuepuka kushiriki ngoma za densi ili zimwi lisiingie nyumbani na kuwaangaisha. Wanaheshimiana. Gacinci alikuwa akitii tahadhari ya Ngongoana dhidi ya kwenda densi za usiku "*Riu nyimbo cia tene nuntu niciainagwa, Gacinci akera Ngongoana, "kanthii rwimbo." Ngongoana akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkariwa ni marimarimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua akerega kuthii.*

Gacinci na zimwi walichukua nafasi ya wahusika wawi. Gacinci alikuwa mkaidi. Aliacha kutii ushauri wa Ngongoana na kwenda kushiriki densi za usiku "*Ntuku i ingi rwainwa bakubi muno. Amwira, "Ari nee, gankegue baba ii ngakuthikagiriria ii nkegucaga irimarimu rikigita atia? rigiigica." ...Athii. Akinya rwimboni"*. Gacinci

alikuwa mwenye tamaa. Alitamani sana kwenda kusikiliza densi za usiku "*Amwira, "Ari nee, gankegue baba ii….".* Alikuwa msaliti. Alidhamini sana kujiburudisha kuliko kukaa na dadake na kumlinda dhidi ya zimwi "*Athii. Akinya rwimboni. Irimarimo nario riari wa baba ruriini rikinathungira.*"

Zimwi linapochukua usukani na kuendelea na uovu, Gacinci anajigundua na kuchukua hatua ya kurudia wema. Aliposikia sauti ya dadake akiteswa na zimwi alikumbuka wajibu wake wa kushirikiana na dadake. Alichukua hatua na kuanzisha harakati za ukombozi.

> *Gacinci akinegua mwang'ina akina. Akinela antu, "Takirani mbigueni." Egua …Akimera, "riu ncuni ii, mumbile nuntu riu ni irimarimu rikuthinia mwana wetu*

Zimwi badala ya kumwadhibu Gacinci kwa uovu wake, linakuwa katili na kumhangaisha Ngongoana. Linaingia chumbani kwa ulafi na kutaka maziwa yote.

> *Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua, riathiria…Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi." Arira, niriathira."*

Zimwi lina tamaa iliyozidi. Linapokamilisha kunywa maziwa linapania kumla Ngongoana. Linamtaka alibebe ili likamle "*Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria*". Zimwi lilikuwa sumbufu. Lilimsumbua Ngongoana lilipoingia chumbani na kumtaka alibebe kwa kamba kama kuni mgongoni ingawa lilikuwa na uzito uliomzidi Ngongoana. Alilibeba huku akilia "*Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikuribota. Arikua akigucaga atikuribota.*

Sifa mbaya za zimwi zinachochea hadhira kulichukia na kuchukia tabia kama hizo katika jamii. Hatima ya muhusika mui ni maangamizi. Zimwi linauawa kwa kuchomwa mishale na mkuki. "*Irimarimu riauma. Riambilia kurathwa na migwi, kumutangwa na matumo, riakua.*

### 5.3.2 Wahusika Wema

Wahusika wema ni wale wanaodumisha umbo la uzuri wa mienendo katika hadithi. Katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci, muhusika Ngongoana anashikilia mienendo inayodumisha mshikamano wa jamii. Ngongoana ni mshauri mwema. Kila mara

anamshauri dadake kukaa nyumbani na kukoma kwenda ngoma za usiku ili kusitiza zimwi kuingia nyumbani. Kwa mfano,

> *Gacinci akera Ngongoana, "kanthii rwimbo." Ngongoano akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkariwa ni marimarimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua akerega kuthii.*
>
> Gacinci akamwambia Ngongoana, "Ebu niende kwenye wimbo."Akamkanya .Akamwamwabia , "Usiende .Nitaliwa na mzimwi ."Kwa kuwa mazimwi yalikuepo .Akasikia akakosa kwenda .

Ngongoana ni mpole na mtiifu.

> Zimwi linapoingia chumbani likamwita na kudai kupewa maziwa, allitika kwa upole na kulipa maziwa yote mbila ubishi. Zimwi lilipomtaka achukue kamba alibebe, alifanya hivyo bila ubisha ingawa hakuwa na nguvu ya kulibeba. Kwa mfano,
>
> *Irimarimo nario riari wa baba ruriini rikinathungira. Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria.*
> *Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi." Amwira, " niriathira."Amwira , "Ngua. Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria. Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikuribota. Arikua akigucaga atikulibota.*

Ngongoana alikuwa mwenye hekima. Alifahamu na kutumia mbinu ya kumtaarifu dadake bila kuhatarisha maisha. Alitumia kiitikio cha wimbo kuwasiliana na dadake na kuomba msaada wa ukombozi. Dadake aliposikia kiitikio cha wimbo, alitambua kuwa Ngongoana alikuwa hatarinikisha kuwaombo wacheza ngoma kumsaidia kumwokoa. Kwa mfano,

> *Ngongoana akiriraga muno. Akiinaga:*
> *(Gacinci ii Gacinci mwile ndagukanilie wathi*
> *Wa utuku Gacinci mwile) x3*
> *Akamwila, "Ngongoana ii ndwaa njia ya mumbu, ndugandwae njia ya mugumo."*
> *Rikaina: Gacinci ii Gacinci mwile*
> *Ndagukanirie wathii wa utuku*
> *Gacinci mwile*

*Gacinci akinegua mwang'ina akina.*

Wakaenda.Wakaenda. Wakaenda. Naye Ngongoanga alikuwa akilia sana. Aliimba:

> (Gacinci ii Gacinci mwambie
> Nlikuonya nyaimbo za usiku
> Gacinci mwambie )x3

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Ngongoana alikombolewa na kakake pamoja na wacheza ngoma waliokuwa pamoja na Gacinci. Zimwi linapouawa, wanaamana yeye na dadake kurudi nyumbani kwa amani. Ngongoana alifanikiwa kurejesha umoja wao na dadake kwa kurudi nyumbani pamoja. Kwa mfano,

*Riakua nirio Gacinci menukile na mwang'ina.*

## 5.4 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Wasichana Wanne wa Ukambani

Wahusika katika hadithi hii walikuwa wasichana watatu, Mweru, Nyaga, Babu na wazazi wa Nyaga na Mweru. Wasichana watatu wanachukua nafasi ya wahusika wawi huku Mweru akitawala nafasi ya wahusika wema.

### 5.4.1 Wahusika Wawi

Wahusika wawi wanajitokeza katika sehemu ya hadithi ya mabadiliko ya mienendo. Wahusika hao walikuwa kiini cha kuvurugika kwa wema wa jamii. Wahusika wawi katika hadithi hii walikuwa wasichana watatu. Hadithi ilipotangulizwa wahusika wote wanaanza kwa kushirikiana na kuwa na mshikamano. Wasichana wote wanne wanakubali kwa pamoja kushiriki mradi wa urembeshwaji. Wanakubali kwa pamoja wakatiwe mwanya.

> "*Airitu mana ma Ikamba meerwa ni magacawe njarumi. Mathii gucawa magego. Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii…."*
> Wasichana wane kutoka Ukambani waliambiwa wangechongwa meno kuyatia mwanya wa Urembo. Wakaenda kuchongwa Meno. Baada ya shughuli hiyo kukamilika, waliambiana "Twendeni mtoni…

Wasichana watatu wenzake Mweru wanajitokeza kuwa wahusika wawi baada ya kushindwa na Mweru. Ni wasichana wenye kinyongo. Walimwonea Mweru wivu baada ya kuwa na mwanya mzuri kisha kupanga njama ya kumuua badala ya kumpongeza.

> *Mathii kuri antu monete irima iraca muno muntu akibingirwa ku akaurira ku. Mathii ri, mathiuba mbele ya Mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku, na twekira mweru ku agakuira kuu.*
> Wakaambiana, "Twendeni tufunue shimo kwa kuondoa lile jiwe tumrushe Mweru ndani. Na tukimtia mle, atafia humo.

Kutokana na kinyongo watatu hao wanakuwa wenye chuki. Wanamchukia Mwenru na kuanza kumtenga katika ushiraka wao. Walipiga hatua mbele kwa haraka ili kumwacha Mweru kwa nia ya kumpangia njama ya kumwangamiza.

> *Mathii ri, mathiuba mbele ya Mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku…*
> Walipoenda, wakaharakisha hatua mbele ya Mweru kisha wakakubaliana wakiwa watatu, "twendeni tuinue jiwe tumtumbukize Mweru mle.."

Watatu hao waliacha kuwa waaminifu na kuwa wasaliti. Wanakubaliana kuuingia shimoni na kwa zamu kisha kutoana kwa kwamba ila Mweru alipofikiwa na kuingia shimoni walikosa kuvuta kamba na kumwacha mle. Badala yake wanamfunikia mle ndani kwa jiwe.

> *Makinerana, "nitumuthairirie ii, turume mukanda, twaruma mukanda, muntu athungira akaburutwa ni antu mathatu akauma. Indi muntu wa cietu ambe athungire ari wa mbele, kenda mweru akarigia akiugaga akarutwa turege kumuruta."*
> Wakasemezana, "Tumdanganye. Tuchukue Kamba. Mtu mmoja akiingia, anavutwa na wale watatu anatoka. Mmoja wetu atangulie ili Mweru aingie akiwa wa mwisho. Halafu tukatae kumwondoa mle.

Wasichana wale watatu walibadillika na kuwa watu waongo. Walikubaliana kwa pamoja kundanganya kuwa Mweru aliliwa na fisi ambao walikuwa wengi katika eneo hilo kipindi hicho.

> *Na twinukange na karugi muno, twathii tuge atiri, nuntu kwina mbiti, twaurua tuge nimbuga karirwe ni mbiti nuntu niwe enukire mbele yetu".*
>
> Kisha turejee nyumbani haraka sana. Tukiulizwa kuhusu habari yake, tuseme alitangulia na huenda alililiwa na fisi."

Hatima ya mhusika muwi ni maangamizi huku ukweli ukibainika na wenye haki kuipata. Wasichana watatu wawi wanaangamia kwa kubadilika kuwa vipepeo baada ya Mweru kuandaa tambiko la kinywaji kilichotiwa ghudi ya kunasia ndege. Ukweli ulibainika baada ya uvumbuzi wa Nyaga ndugu yake Mweru na Mweru kuokolewa na wanajamii.

> *Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urembo.*
> *Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugaga*

*makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe.* ,"

(Mweru alikuwa amekasirika. Alitaka kulipiza kisasi kwa kuwaliga. Akabaki. Akatafuta rojorojo ya kutengeneza gundi ya kuwanasa ndege kutoka kwenye miti ya kila nui. Angeitia rojorojo hiyo kwenye maziwa ambayo angewapa. Siku ikafika. Wakaja Mweru akawapokelea tena. Akawapa maziwa yenye rojorojo sumu naye akayanywa yale salama wasijue. Wakanywa. Baadaye akawaambia, "Twendeni niwasindikize." Akawasindikiza. Walipofika njiani, wote wakageukan kuwa vipepeo isipokuwa Mweru.)

### 5.4.2 Wahusika Wema

Wahusika wema ni wale wanaodumisha wema wa kijamii pamoja na kuendeleza mshikamano wa mfumo wa jamii. Katika hadithi ya Wasichana wanne wa Ukambani, wahusika Mweru, Nyaga, babu na wanajamii walikuwa kiwakilishi cha wahusika wema. Mweru alikuwa mpole na mshirika mwema. Baada ya kuwashinda wenzake na Mwanya wake kubainika kuwa mzuri hakuwatenga wala kuwadharau wenzake watatu. Aliendelea kushirikiana nao kama walivyozoea.

*Mweru we atacawa riingi nuntu we niamacindite. Maca riu merana "Riu ni gutua ringi". Mambiriria kugera munyiri ringi. Magera magera magera matikubetukia nwaka makugwithia runcini mari mathatu ringi. Mweru atua aringia ringi.*

(Wakarudi na kuchongwa tena. Mweru hakuchongwa tena kwa kuwa alikuwa amewashinda. Wakaenda mtoni na kuanza kushindana tena. Wote watatu wakashindwa tena. Mweru akafanikiwa.)

Mweru ni mwepesi wa kuwaamini wenzake. Yeye na wenzake walipokubaliana kuingia shimoni kisha kila mmoja kutolewa na wengine kwa kuvuta kamba hakuwa na ubishi kuwa wa mwisho kuingia. Alipowaamini na kuingia wakakosa kumtoa ingawa alifanya hivyo kwa kuwaamini.

*Mabanga ugu. Mathungira ria mbele makirutanaga makirutanaga makirutanaga. Marutana monthe kinya ona mweru maruta. Macokera ria kairi. Mathii mathatu akirutagwa. Mweru arigia. Arigia ri, akiinamia mukanda arutwa ri, akunikirwa na ibari (ibiga)*

(Wakaingia kwa awamu ya kwanza kila mtu akiviutwa na kutoka. Hata Mweru akatolewa. Wakarudia mara ya pili. Wa kwanza watatu wakatolewa. Mwerru akaingia wa mwisho. Akatikisha Kamba wamwondoe lakini wakamfunikia mle ndani kwa jiwe kubwa.)

Mweru pia, alikuwa karimu. Wasichana wenzake walitambuakuwa aliokolewa waliamua Kwenda kusalimia hata hivyo Mweru aliwakaribisha na ku Wakasemezana, "Tumdanganye. Tuchukue Kamba. Mtu mmoja akiingia, anavutwa na wale watatu anatoka. Mmoja wetu atangulie ili Mweru aingie akiwa wa mwisho. Halafu tukatae kumwondoa mle. Wakapanga hivyo.

Wakaingia kwa awamu ya kwanza kila mtu akiviutwa na kutoka. Hata Mweru akatolewa. Wakarudia mara ya pili. Wa kwanza watatu wakatolewa. Mwerru akaingia wa mwisho. Akatikisha Kamba wamwondoe lakini wakamfunikia mle ndani kwa jiwe kubwa. Akabaki humo. Akakaa mle, wakirimia kinywaji bila kujali walivyomtenda uhayawani.

> *Mathii Kumukethia ntuku ya mbele, Mweru amamukiira wega muno na nkinya amakundia iria manunyanira weega muno.*
>
> (Wakaenda kumsabahi siku ya kwanza. Mwertu akawapokelea vizuri sana. Akawapa maziwa wakanywa pamoja)

Mweru ni mpambanaji na mstahimilivu. Alipambana na hali ngumu mle shimoni pamoja na kustahimulili uozo kwenye mguubila kukata tamaa. Alipoitambua sauti ya Nyaga aling'ang'ana hadi kuhakikisha Nyaga amemtambua na kumsaidia. Aliimba kwa sauti ili Nyaga asikie na kumwokoa. Hatimaye anafaulu na kuokolewa na wanajamii.

> *Nawe kaana karia gekaririte ibaari riri, gatikumenya kana ni ibiga rikunikanie.*
> *Gekarite o baria Mweru ari. Mweru egua akinaina: ...*
> *Nyaga abanga "ari kambire mburi iria bu ringi"*
> *Amiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*
> *Akinegua:*
>
> *Nkanga ii nkanga cia Maindi*
> *Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
> *Wana riu nwa tutwire*
> *Nkanga cia maindi*
> *NItwarire nguo cia mwili*
> *Nkanga cia Maindi*
> *Tukinora mugwanja umwe*
> *Nkanga cia Maindi.*
>
> (Kulipopambazuka, Nyaga akaambiwa, "Utaenda useme hivyo ulivyosema ili tumsikie Mweru akizungumza." Wakaamka mapema na kusanzuka. Wakafika Malishoni Nyaga akakalia jiwe lile. Watu wakatega masikio yao nchi! Nyaga akasema, Ewe mbuzi potrelea pote kama yule mweru wetu aliyetokomea toko!"
>
> Wakasikia: Kanga I Kanga wa mifupa
> Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,

Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Watu wale waliposikia hivyo, wakaondosha jiwe. Walikuwa na Kamba mbili. Mtu mmoja akaingia humo na Kamba moja. Mweu akavutwa akafika nje. Yule mtu aliyekuwa ndani naye akavutwa akatoka.)

Hatima ya wahusika wema ni kupata ushindi na ukombozi kama haki. Mweru alikombolewa na wanajamii na kurudia hali yake ya kawaida baada ya kutunzwa na kupona uozo. Ukweli unabainika kuwa hakufa bali alitupwa shimoni. Wenzake wanabadilika kuwa vipepeo huku Mweru akibaki kufurahia mwanya wake mzuri.

> *…makinegua Mweru ri, niarabwire. Niaronire wa kumuruta kuu irimani. Makinandika kamakamukethie. Mathii Kumukethia ntuku ya mbele, Mweru amamukiira wega muno na nkinya amakundia iria manunyanira weega muno. Riu ri, amakinyia menuka. Akinamatwira kiatho na auke. "Muce na nkegua nimukuirite ii, wana iria ni mukethira riri bo." Amera "nibe tugaca gugukethia Mweru."*
> *Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urembo.*
> *Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugaga makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe. Mweru atigwa na mwanya wawe.*
>
> (Akabaki. Akatafuta rojorojo ya kutengeneza gundi ya kuwanasa ndege kutoka kwenye miti ya kila nui. Angeitia rojorojo hiyo kwenye maziwa ambayo angewapa. Siku ikafika. Wakaja Mweru akawapokelea tena. Akawapa maziwa yenye rojorojo sumu naye akayanywa yale salama wasijue. Wakanywa. Baadaye akawaambia, "Twendeni niwasindikize." Akawasindikiza. Walipofika njiani, wote wakageukan kuwa vipepeo isipokuwa Mweru.)

### 5.5 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi katika Hadithi ya Chura na Mbuni

Wahusika katika hadithi hii walikuwa Pamoja na chura, mbni na wanyama wengine na wanachoma nyama na kula pamoja. Wahusika hao waligawika katika mikabala miwili. Wawi na wema.

### 5.5.1 Wahusika Wawi

Wahusika wote wanatanguliza hadithi hasa kwa habari njema. Wahusika wawawi wanajitokeza katika katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Wahusika hao ni wale wanaosambaratisha mshikamano wa jamii. Mwanzoni chura, mbuni na wanyama wengine wanaishi kwa ushirikiano mkubwa. Chura na mbuni walichukua nafasi ya wahusika wawi. chura alikuwa mkaidi na mbinafsi.

Mbuni anapochukua usukani na kuendeleza na uovu kwa kulaani vikembe wa chura chura anajigundua na kuchukua hatua ya kurudia wema. Chura anaamua kumtafuta mbuni ilikuomba msamaha kwa kumbembeleza na kuamuru maji yarejee kwenye mito. Alichukua hatua na kuanzisha harakati za ukombozi. Badala ya mbunikuendelea kuwaangamiza vikembe wa chura na churakukausha mito wanasameheana na kurejessha Amani miongoni mwao. Hatima ya muhusika mui ni maangamizi lakini katika hadithi hii tunapata kuwa msamaha unatumika kuondoa uovu wa wahusika wawi. Hata hivyo chura anasemehewa kwa masharti kwani ilimbidi alete mafuta kwenye vijiti maalum saba!

> *Nyaga kithimilite ikunda runci icioke imane nyama. Riria Nyaga yaculithililie yoona taka Kaura gatimicuite ri,yakuamiriria igikunda runci ugu,Kaura karuma ibiga kamiringa rugoci rukinaguuka.Nyaga yacioka yaciokia rugoci rwao ringi.Ai!ikinathuura ikinenuka. Ikinakeera, " Negwe kaura woona ni kitheru kiu giakwa wakura , ugakileta na nkuniko mugwaanja cia maguta ma mbariki."Kaura gatigwa nako ri, gakurumwa ni Nyaga.Gatigwa runcini nuntu nigekaraga runcini ri, twana twa kaura twambiriria gukua.*
>
> *Kaura nako kambiriria kwimba maguru. Kaura kamenya nkugwatwa ni kirumi kia Nyaga kauga, "riu ninthii nkiuragiriria kwa Nyaga na nina nkuniko mugwanja cia maguta ma mbariki."*
>
> (Alipoona kama chura hamuoni, akainama akapiga tundu la maji. Chura akaokota jiwe, akampiga upembe ikang'oka. Mbuni akalejesha upembe tena. Akakasilika.Akaenda kwake. Akamwambia cura, "nawe chura kwa vile umenigonga umening'oa upembe, utanirejeshea kwa vizibo saba vya mafuta ya karafuu." Chura akaachiwa lahana na mbuni. Vikembe vya chura vikaanza kufa. Chura naye akaanza kufura miguu. Chura akafahamu kuywa lahana ya mbuni ilikuwa imemfika. Akasema, "Sasa nitaenda nikiulizia aishiko mbuni nikiwa na vizibo saba vya mafuta ya karafuu." Chura alikata vijiti vya karafuu na kutia yale mafuta humo. Akaunganisha hadi vikafika saba.)

Baada ya tambiko hili la kusameheana mbuni alimwondolea chura laana ya kufa kwa wanawe naye chura akamruhusu kuwa anayanywa maji.

Sifa mbaya za chura kama mhusika mui zinaichochea hadhira kuchukia kuwa mwovu katika jamii na kupenda kuwa mwadilifu na mwema. Mhusika mui katika hadithi hii anaipamba hadithi kwa kuonyesha nguvu za matambiko ya jamii kama njia nzuri ya kupata haki. Baada ya tambiko la kusameheana chura na mbuni pamoja na familia zao waliishi kwa Amani.

### 5.5.2 Wahusika Wema

Wahusika wema ni wale wanaodumisha umbo la uzuri wa mienendo katika hadithi. Hatima ya muhusika mwema ni ushindi.

## 5.6 Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Fisi na Ndovu

Wahusika katika hadithi hii walikuwa fisi na ndovu. Wahusika hao waligawika katika mikabala miwili. Wawi na wema.

### 5.6.1 Wahusika Wawi

Wahusika wote wanatanguliza hadithi hasa kwa habari njema. Wahusika wawawi wanajitokeza katika katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Wahusika hao ni wale wanaosambaratisha mshikamano wa jamii.  Mwanzoni fisi na ndovu wanaishi kwa ushirikiano mkubwa.

> *Njogu na mbiti ni ciatumite urata. Cierana, riu niilalage irimani rimwe. Ciatua kuraraga irimani rimwe. Njogu yari na twana twayo na mbiti yari na twana twayo.*
> Ndovu na fisi walikuwa marafiki wakubwa, wakakubaliana wawe wanalala na kuishi kwenye shimo moja. kila mmoja alikuwa na wanawe lakini wote waliishi kwa Amani.

Hatima ya muhusika mui ni maangamizi. katika hadithi tunapata kuwa mhusika fisi na wanawe ambao ni wawi wanaangamizwa kwa kupigwa mateke na kukanyagwa na ndovu.

> *Mbiti yakira. Mbiti yambatwa. Yakinyithanua ni njogu yakua. Twana twambatwa. Twakinyithanua twakua.*
> Fisi akanyamaza. Akashikwa na tembo. Akakanyangwa akafa. Wanawe wakashikwa. Wakakanyangwa wakafa

### 5.6.2 Wahusika Wema

Wahusika wema ni wale wanaodumisha umbo la uzuri wa mienendo katika hadithi. Katika hadithi ya fisi na ndovu tunapata kuwa wana wa tembo wana sifa za mhusika mwema kwani tunapata ya kuwa hawakuwadhulumu wana wa fisi hata kama walishambulia ndugu zao.pia tunapata kuona mwana mmoja wa tembo anaamua kwenda kumuarifu mama yake waliyokuwa wanapitia mikononi mwa rafikiye fisi na vikembe wake. Alifunga safari hadi alikokuwa malishoni.

> Mwandovu aliyekuwa na chongo akatanabahi kuwa wamebaki wawili tu. Akasema, "tutaenda malishoni kula na wana wa fisi. Lakini, kwa kuwa sijui iwapo ni mie au ndugu yangu ataliwa na fisi nitatoroka. Sitasubiri tuliwe sote. Nitaenda kumsaka mama aishiko. Nitakua nikila mbali na fisi pale kichakani. Sitawafuata wakirejea pangoni. watamla ndugu yangu ila mimi watanifuata wanikose. "akaamua.
> Wakaenda malishoni kama ilivyokuwa mazoea. Yule chongo akasafiri mchana kutwa. Ndugu yake akarejea pangoni na kuliwa na wana wa fisi. Fisi na wanawe walidhani kwamba yule chongo angerudi. Lakini alikua ameapa, "sasa ni kwenda bila kuangallia nyuma."
> Akasafiri hadi akakutana na fisi. Akaimba:
> fisi mnaokula huku, mnaokula huku,
> mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
> Alituacha katika nyumba ya fisi.
> Mwanafisi akasema, *m…m…m…m…*
> Akaulizwa nini kinachokuliza?
> Akasema nalilia mwana yembo.
> Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

> *Riu, kaana ga kari na nthoongo, kona matigara mari mairi. Kandika riu, "gatuthii tutigare na ciana ino, indi untu twathii kuria, nuntu ninkumenya narega kuriwa, nig aka kangi gakaliwa nuntu turi mairi, na tucioke tuthire, niu nintoroka, ngacerie ku maitu ekaraga. Na tukathii kuria wega muno kithakani, indi niu, nkaricaga ni kuraja muno. Ikinuka, tinicuma thuuba. Riu gaka gakinya kariwa, niu, maganceria mbure. Metere minuka, timinunka."*

> *Kana karia ka nthongo kabanga ugu. Ciathi kuria. Kibwai gigikinya ri, cionthe ciice ciinukite cionthe ri, cienuka ciici kari wabo. Karia nako gatinda kuthii. Cienuka, ciathii. Kana karia na kathii karira, " m…m..m…m…!" "ni indu ukulilila?" "Ni rutende rwa njogu nkulilila." "kutha na utigakuthe wica." Kaana karia kaliwa.*

> *Riu mamenya karia nika gatikenuku, nigaguca. Kau gakuriwa. Kau nako kandika, "riu nikuthii gutigocoka." Ri cienukire nako kambiriria kuthii riu. Kathii kathii kathii kathii.*

> *Gatungana na mbiti kaina, "mbiti mukuria guku, mukuria guku, mwanamwonera njogu ya cianyaga yatutigire nyomba na mbiti, kana*

*ka mbiti gakauga m…m….m…m…, gakaurua ni indu ukulilila, gakauga ni rutende rwa njogu nkuririra, kutha na utigakuthe wica, kuthu!"*

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Fisi anaangamizwa nakuleta ushindi katika familia ya ndovu na wanawe wawili kwani waliweza kuokoa maisha yao.

Kutokana na hadithi hizi , ni bayana kuwa mhusika mwema humalizia kwa ushindi. Hili ni funzo kwa jamii kuwa wema hulipa kwa wema. Inabainika kuwa wachuka wana imani kwamba ukiwa mwenye haki utatetewa na hali za kimaumbile na wema utaendelea kutawala dhidi ya uovu. Inavutia kuona ukweli na wema hubainika na kutawala dhidi ya uovu.

# SURA YA SITA

# MBINU ZA KIMTINDO KATIKA NGANO ZA WACHUKA

## 6.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu za kimtindo zilizotumika kuleta ujumi katima ngano za wachuka. Mtafiti alitanguliza sehemu hii kwa kuchanganua mbinu za kisanaa na mbinu za lugha mtawalia.

## 6.2 Mbinu za Kimtindo

Kwa mujibu wa Mehmood na wenzake (2014), dhana ya kimtindo ni taaluma ya uchanganuzi na ufasiri wa matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo mbinu za kimtindo ni mbinu zinazohusiana na matumizi ya lugha kiufundi na kiisimu. Matumizi ya lugha kiufundi ni pamoja na mbinu za kisanaa na mbinu za lugha au tamathali za usemi. Mawazo ya Wamitila (2003), yanatilia uhusiano wa dhana ya mtindo na kimtindo kwa kufafanua mtindo kama mazoea ya mtunzi wa kazi ya Sanaa kuteua msamiati, mbinu za kisanaa na mbinu za lugha ili kubainisha upekee wa kazi yake. Kimsingi kutokana na mawazo ya wataalamu hao dhana mbili za mbinuza kimtindo zinabainika: dhana ya mbinu za kisanaa na dhana ya mbinu za lugha. Dhana hizi zilikuwa muhimu kuangaziwa kama mbinu za kimtindo katika ngano za Wachuka na namna zinavyotumika kuendeleza ujumi.

Baadhi ya mihimili ya nadharia ya ujumi wa kinudhuma huelekeza kuwa mistari na aya hazipangwi tu kwa mujibu wa sheria za kishairi, lakini pia hutumiwa kuwasilisha ujumi na tajiriba ya pamoja ya jamii husika kwa kutumia takriri, mianzo maalumu na jazanda miongoni mwa vipengele vingine vya kimtindo. Mawazo haya yalibainika kusisitiza umuhimu wa vipengele vya kimtindo katika dira ya ujumi wa kazi za faisihi. Mitindo mbalimbali ya takriri ilibainika katika ngano simulizi za Wachuka miongoni mwa mbinu nyingine. Mbinu hizi zilihakikiwa kupitia kitengo cha mbinu za kisan ana mbinu za lugha.

### 6.2.1 Mbinu za Kisanaa

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mbinu za kisanaa ni mbinu za kiufundi anazotumia mwanafashi kama ala ya kuwasilishia maudhui na ujumbe mkuu. Huwa mbinu za kimtido anazoziteua mtunzi ili kuimarisha ubunifu wa kazi yake. Wamitila(mtaje)

aliziorodhesha baadhi ya mbiu izo kama vile jazanda, taharuki, ndoto, nyimbo miongoni mwa nyingine. Mbinu hizi pia ziliweza kujitokeza katika ngano za Wachuka. Baadhi ya mbinu za Sanaa zilizotambuliwa ni pamoja na matumizi ya nyimbo, taswira, taharuki, dayalojia, antorojia ya kiafrika na ubuntu.

#### 6.2.1.1 Nyimbo

Wimbo ni utungo wa kishairi ambao huwasilishwa kwa njia ya kuimbwa. Katika ngano simulizi za Wachuka nyimbo zilijumuishwa katika uttunzi na uwasilishaji. Nyimbo hizo ziliambatana na muktadha wa matukio pamoja na dhima. Kwa mfano, wimbo ufuatao wa kiitikadi unaojitokeza katika hadithi ya kindi na fisi kama kiungo cha tambiko.

> *Tubare na mbiti cia tirimana Ginci kiiru ciathii riu, riu cierana, "riu ni kwina ii kenda muntu atuba." Riu ciaina:*
>
> *"Ntarumaa ntarumaa muthoroko."*
> *Kabare kaina;*
> *Ntarumaa x2*
> *muthoroko x2*
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*
>
> *Mbiti nayo yerwa niine. yaina:*
>
> *Ntarumaax2*
> *muthorokox2*
> *wa muru wa kabare Ginci kiiru ntwara*
>
> *Mbiti yagamba runcini butu! Yauga, "Ruutana ndutani ii, gantatubite wege*
>
> *Kabare kerwa, "ruuga ringi riu nuntu mbiti yauga nika itarugite weega, iruge weega." Kaina;*
> *Ntarumaa x2*
> *Muthororoko x2*
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwaara.*
> *Kabare ri, karuga gakinya rugongo ruria.*
>
> *Mbiti yambiria gutantaura;*
>
> *Ntauma x2*
> *muthooko x2*
> *wa muu wa kabare Giinci kiiru ntwara*
>
> *Yagamba runcini nku! Yerwa riu mbiti i cingi,*
> *"Ai nee riu ni weu wiite." Yauga ari rutaana ndutani ii gantatubite weega ri, tingwa ku."*
>
> *Kabare kauga, "gantube ria kathatu." … Kaina:*
>
> *Ntaruma x2*
> *muthorokox2*
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*
>
> *Kabare gatuba gakinya naa rugongo ruru rungi. Mbiti yambiriria riu;*
>
> *Ntauma x2*
> *Muthooko x2*

*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

Siku hiyo ikafika. Kindi na Fisi wakakutana Ginci kiiru. Wakaafikiana waimbe ili kila mmoja aruke mto ule. Wakaimba:

sikula x2
kunde x2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nisombe

Kindi akaimba,

sikula x2
kunde x2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nisombe

Kindi akachupa akafika ng'ambo ya pili. Fisi naye akaambiwa aimbe. Akaimba:

Sikua x2
kunde x2
Za ndugu kindi Ginci kiiru nisombe

…Kindi akaimba:

Sikula x2
kunde x2
Za ndugu fisi Ginci kiiru nisombe

Kindi akaruka akafika upande wa pili.

Fisi akaanza kugugumiza:

Sikuax2
kundex2
Za ndugu kindi Ginci kiiru nisombe

…Kindi akaimba akiwa ng'ambo ile:

Sikulax2
kundex2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nsombe

Kindi akarupa akafika upande mwingine

Fisi naye akaanza:

Sikuax2
kundex2
Za ndugu fisi Ginci kiiru nsombe

Wimbo huu ni wa kishirikina unaotilia uzito nguvu za ushirikina kama nyenzo ya kupata haki. Wimbo unajenga ujumi wa kiimani na maadili ya jamii ya Wachuka. Maneno katika wimbo wa tambiko yanakuwa Ushahidi wa matendo ya mtu husika na ambao unamtolea hukumu. Hukumu inategemea ukweli wa msemaji. Kama anayosema ni ya uongo nguvu za maumbile zinamwadhibu na kumwondolea mwenye haki lawama. Fisi na kindi wanaimba wimbo huo kama njia ya kukukili kisha nguvu za maumbile hasa mto Ginci kutoa hukumu. Fisi kwa kuwa mwongo na nafiki anasombwa na mto Ginci hivyokutambulika kama mwiziwa kunde za kindi. Wimbo huu unaimarisha kilele cha hadithi na kuwa ya kuvutia kimaadili na kufanikisha dhamira ya ngano kama ala ya kuonya na kutahadharisha. Nguvu za matambiko zinapigiwa upatu

na kuwafanya wanajamii kuogopa nguvu hizo na kuchagua kukili makosa kuomba msamaha kuliko kupitishiwa matambiko. Wimbo huo pia unafanikisha taharuki na kufanikisha kufifisha mgogoro kiujumi.

Wimbo mwingine ni ule wa Ngongoana na zimwi katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci. Wimbo huo ulikuwa wimbo-mbiu kwa Gacinci. Tazama wimbo ufuatao wa Ngongoana na Gacinci:

*Ngongoanga akiriraga muno. Akiinaga:*
*(Gacinci ii Gacinci mwile ndagukanilie wathi*
*Wa utuku Gacinci mwile) x3*
*Akamwila, "Ngongoanga ii ndwaa njia ya mumbu, ndugandwae njia ya mugumo."*
*Rikaina: Gacinci ii Gacinci mwile*
*Ndagukanirie wathii wa utuku*
*Gacinci mwile*
*Gacinci akinegua mwang'ina akina. Akinela antu, "Takirani mbigueni." Egua,*
*Gacinci ii Gacinci mwile*
*Ndagukanirie wathi wa utuku*
*Gacinci mwile*
Naye Ngongoanga alikuwa akilia sana. Aliimba:
(Gacinci ii Gacinci mwambie
Nlikuonya nyaimbo za usiku
Gacinci mwambie) x3
Likamwambia, "Ngongoanga, nipeleke njia ya mumbu usinipeleke njia ya magumo." Likaimba: Gacinci Gacinci mwambie
Nilikukanya nyimbo za usiku
Gacinci mwambie
Gacinci akasikia dada ake akiimba akaambia watu, "Ebu nyamazeni nisikie." Akasikia:
Gacinci Gacinci mwambie
Nilikukanya nyimbo za usiku
Gacinci mwambie

Wimbo huu unamjenga mhusika mwema kiujumi kwa kumfisha taji ya hekima na upevu wa akili. Unawasilisha fikra za pevu za Ngongoana kumtaarifu dadake hali tata aliyomo bila kugadhabisha zimwi na kumshambulia. Unafanya hadithi kuvutia kila inasumuliwa kwa vijana wachanga huku wakijionakuwa na uwezo wa kiakiri na tajriba ya mbinuishi. Hekima ya mhusika Ngongoana kuwa mbunifu na kuweza kulishinda zimwi kwa akili kwa kutumia wimbo kifumbo unaifanya hadithi kuwa nzuri ya kusimuliwa mara kwa mara. Wimbo huu unazua dhima nyimbo kama ala ya kupitisha ujumbe kama nyenzo ya mawasiliano. Ngongoana alitumia wimbo kijanja kumfikishia

dadake ujumbe wa kuja kumkomboa dhidi ya zimwi lililokusudia kumla. Wimbo huo pia unakaribisha kilele cha hadithi kwa njia ya mnato pamoja na kujenga taharuki. Wimbo umetumika pia katika hadithi ya Wasichana Wanne wa Ikamba kama mbinu ya kimtindo. Kwa mfano wimbo ufautao wa Mweru:

*…Mweru egua akinaina:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*NItwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

*Nyaga aabnga "ari kambire mburi iria bu ringi"*
*Amiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*
*Akinegua:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*Nitwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

Mweru akaimba:

Kanga I Kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Nyaga akaamua, "Ebu nimwambie mbuzi yule hivyo tena." Akamwambia, "Ewe mbuzi potelea pote kama yule Mweru wetu aliyetokomea toko!"
Akasikia:

Kanga I Kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Wimbo huu pia ni wimbo-mbiu au taarifu. Wimbo huu unaonyesha ujuzi wa hali ya juu wa kufufua mtiririko wa hadithi baada ya kuzama kwa mhusika mkuu. Wimbo unadumisha mandhari ya Mweru katika ulimwengu ndani ya jamii kiujumi. Mweru alipoimba aliweza kufufua ushirikiano wake na Nyaga nduguye. Inakuwa hatua ya kwanza ya safari ya kurejea kwenye jamii na kuendelea tena na maisha ya kawaida huku hadithi ikipata nafasi ya kuendelea. Ujumbe kwenye wimbo unamfanya Mweru kuonekana kuwa mwenye nguvu na mshindi. Wimbo huo unakuwa ala ya kufufua imani kuwa wahusika wema hawaangamii. Ufufuo huu huifanya hadithi kuwa tamu na nzuri ya kusimuliwa mara kwa mara. Unachangia pia mbinuishi katika jamii kama kiwakilishi cha hekima. Mweru kuimba wimbo huu kunamfanya kuwa mtu anafikiria sana na kwa hekima.

Katika hadithi ya chura na mbuni tuna wimbo wa chura anaoimba ili kuwauliza wanyama wenzake njia ya kwennda kwa mbuni,

> *Kathii gatema tumiti twa miariki nuntu turi karima. Gagikagira maguta ma mbariki ku, twakinya mugwanja. Kamuntithania kamuntithania kamuntithania kathii tang'u! tang'u! tang'u! kathii gakinya guntu nau gatunga wegua ni mbiti, gakaina,*
>
> *"Muthurithuri muthunthuiga, kwa Nyaga ninaku muthunthuiga. mbile mbu ya Nyaga muthunthuiga. Ciana cianathira muthunthuiga ni rwagi na mbebo muthunthuiga."*

Akaanza safari. Alipokutana na Wanyama njiani akaimba. *Muthunthuri muthunthuiga, kwa mbuni ni wapi? Muthunthuiga, nipeleke vyombo vya mbuni, muthunthuiga wanangu wamekwisha, muthunthuiga, wameugua baridi na homa ya malaria, muthunthuiga.*

Wanyama wengine akiwemo fisi walikuwa wamechukizwa na chura kwa tendo lake la kukausha mito lakini chura kwa ujanja wake anatumia wimbo ili kuyeyusha moyo wa fisi, hivyo kuwa nyenzo ya uridhiano. Kwani angetumia lugha ya kawaida ingemuwia vigumu kufanikisha mawasiliano yao hivyo hangesaidika.katika fasihi jukumu moja la nyimbo ni kuburudisha na kwa njia hii mawazo maovu hupunguzwa a hata kuondolewa kabisa kupitia nyimbo.wimbo wa chura ulimsaidia kupata usaidizi.wimbo huu umetumika kumjenga mhusika chura kama mhusika mwema kwani anaona haja ya kwenda kuomba msamaha pia anapomwita Fisi *muthuri muthumnhuiga* kwani ni jina

lenye maana ya mzee mheshimika inaarifu kuwa chura alikuwa mnyenyekevi.hivyo kuendeleza dhana ya ujumi.

Pia katika hadithi ya ndovu na fisi tuna wimbo ulioimbwa na mwana wa Tembo alipokuwa anamtafuta mamake. Msimulizi wa hadithi hii anaonekana kutumia huu wimbo ili kuwavutia hasa watoto kwani tunaona kuwa mwimbaji ni motto wa ndovu. Kwa njia hiimvuto unapatikana.pia tunapata huu wimbo unarahisisha mawasiliano kwani kupitia huu wimbo huyu mwana tembo aliweza kupata habari za mahali alimokuwa mamake. Wimbo huu umetumika kuwajenga wahusika wadogo wadogo kama vile paa, swara na ndovu wengine ambao hatukuwaona hapo awali.

Akasafiri hadi akakutana na fisi. Akaimba:

fisi mnaokula huku, mnaokula huku,
mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Mwanatembo huyo alisafiri hadi akakutana na ndovu. Akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Ndovu wakamwambia? Unaona kule ng'ambo ile, ndiko aishiko ndovu wa Cianyaga."

Akasafiri hadi alipokutana n ap aa. Akaimba

Paa mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Akaambiwa, "unaona kule, ndiko aishiko mama yako."

Akaendelea na safari. Akakutana na swara wakiwa malishoni. Akaimba:

Swara mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana tembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Akaambiwa, "kule ndiko anakoishi mamaku."

Alipokuwa karibu kufika, aliwaona ndovu wachache pahali. Akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Wakamwambia, "Ndovu wa Cianyaga ndiye yule. Angalia. Pale palipo na ndovu wengi. Ushafika. Tembea kidogo tu. Hapo ndipo mama yako huishi. Utampata." Yule chongo akafurahi mno alipowaona hao tembo. Alipofika pale lakini hakuweza kumtambua mama yake miongoni mwa wale ndovu wengi. Akaona wimbo ungemsaidia akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema, *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Ndovu hao wengine hawakuwa na mwao na kile kilichokuwa kikiendelea. Waliendelea kula tu.  Mama yake akaskia ni kama alikuwa akiitwa. Akawaambia wenzake, "Ebu nyamazeni. Tusikilize. Kuna jambo nimeskikia." Ndovu wakanyamaza ji!

Yule mwanandovu akaanza wimbo:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema, *m…m…m…m…*
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

#### 6.2.1.2 Taswira

Msokile (1993), anaeleza taswira kama mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya mtunzi katika kazi yake ya fasihi. Taswira humpa hadhira hisi mbalimbali kama vile kunusa, kuona, kugusa, kuonja na kusikia. Katika ngano za Wachuka taswira mbalimbali zilibainika kutumika ili kuendeleza ujumi. Kwa mfano katika hadithi ya kindi na fisi mtunzi anatanguliza hadithi kwa taswira ya umoja na ushirikiano pamoja na kuzua picha ya usalama fisi na kindi wapofanya urafiki na kushirikiana kulima. Kifungu kifuatacho kinathibitisha taswira hiyo:

> *"Mbiti na kabare ciatumire urata cierana niciunge itema, ciauga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko."*
> (Fisi na kindi walifanya urafiki kisha wakakubaliana wapalilie shamba ili wapande mbaazi.)

Wakapalilia na wapanda mbaazi. Kufanya urafiki kati ya fisi na kindi ni taswira ya hakikisho ya usalama kwa kuwa katika maisha ya kawaida ya porini, fisi huwa tishio la usalama wa kindi. Fisi huwala wanyama wandogo kama vile kindi. Mpango wao wa kupalilia shamba na kupanda mbaazi pamoja ni taswira ya umoja na ushirikiano unaojengeka juu ya urafiki wao. Kwa jumla maelezo ya kifungu hicho yanaleta taswira ya maisha mema ya urafiki. Taswira hii katika utangulizi wa hadithi inaendeleza ujumi wa masimulizi unaokiuka uhalisia. Katika hali halisi, fisi huchukiwa kwa tabia zake za ulafi lakini katika hadithi hii anapendeza kwa kuwa ajenti wa usalama, umoja na ushirikiano. Taswira hii inafanya maisha ya urafiki kama huo kuwa ya kutamanika.

Taswira kama hiyo pia inajitokeza katika utangulizi wa hadithi ya Ngongoana na Gacinci. Mtunzi anatanguliza hadithi kwa taswira ya umoja ushirikiano na usalama. Ngongano na Gacinci ni ndugu mayatima wanaotegeana kwa ushirikiano dhidi ya mashambulizi ya zimwi. Tazama dondoo ifuatayo kutoka kwa hadithi ya Ngongoano na Gacinci:

> *Kwari na Ngongoana na Gacinci. Muntu na muru wa ng'ina. Aciari mao makua. Indi, maari ma ikamba. Matigwa mari mairi.*
> *Riu nyimbo cia tene nuntu niciainagwa, Gacinci akera ngongoana, "kanthii rwimbo. "Akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkaliwa ni malimalimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua, akerega kuthii.*

Ngongoana na Gacinci alikuwa mtu na ndugu yake. Wazazi wao wakafa na kuwaacha peke yao wakiwa wawili. Walikuwa wa Ukambani. Maelezo hayo ya mtunzi yanajenga

taswira umoja kama ndugu na kutegemeana kama mayatima. Kadhalika mtunzi anapanua taswira yake na kujumuisha suala la usalama na ushirikiano. Kuwepo kwa mazimwi ni picha ya hatari inayowakabili Ngongoana na Gacinci kiusalama. Gacinci alitii ushauri wa dadake kila alimrai asihudhurie ngoma ya usiku ili wawe pamoja na kujikinga zimwi. Kutii kwa Gacinci ni taswira ya heshima na ushirikiano. Taswira hii inazima hisia za masikitiko na huruma kiujumi kisha kusisitiza uwezo walio nao wahusika Ngongoano na Gacinci kukabiliana na maisha mradi tu watadumisha umoja kama ndugu na kushirikia kila jambo. Taswira hii inaifanya hadithi kuwa nzuri ya kuhadithi hata mayatima mara kwa mara na kuwatia nguvu.

Taswira ya umoja na ushirikiano pia inatumika kiujumi kutanguliza hadithi ya wasichana wanne wa Ukambani. Kifungu kifuatacho kutoka kwa hadithi ya Wasichana Wanne wa Ukambani ni thibitisho la taswira hiyo:

> *Airitu mana ma Ikamba meerwa ni magacawe njarumi. Mathii gucawa magego. Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii, u ukaringia munyiri rugongo ruria atuike niwe ena njarumi I mbega.*

Wasichana hao wanne kutoka Ukambani waliambiwa wakachongwe meno kuyatia mwanya wa urembo. Wakaenda wakachongwa meno na baada ya shuguli hiyo kukamilika, wakakubaliana kwenda mtoni waone ni nani angeweza kutema mate kupitia kwa mwanya wa meno hadi ng'ambo ya pili, ili kubainisha mwenye mwanya mzuri. Wanashirikiana na kukubaliana kufanya shughuli zote kama kikundi. Hakuna anayepinga kutoka mwanzo. Maelezo hayo yanasawiri umoja na ushirikiano. Taswira hii inatanguliza ulimwengu wa wanawake kiujumi na kupendeza kuona namna wanashirikia bila wivu.

Katika hadithi ya fisi na ndovu mtunzi anatanguliza hadithi pia kwa taswira ya umoja na ushirikiano pamoja na kuzua picha ya usalama fisi na ndovu na wanawe wanapofanya urafiki na kushirikiana katika shughuli za malazi na malezi. Kifungu kifuatacho kinathibitisha taswira hiyo:

> *Njogu na mbiti ni ciatumite urata. Cierana, riu niilalage irimani rimwe. Ciatua kuraraga irimani rimwe. Njogu yari na twana twayo na mbiti yari na twana twayo.*
>
> *Riu, ciekara muno muno muno ikilalaga ilimani rimwe. Ciikarite muno, ntuku imwe njogu niyerire mbiti nuntu numendanite muno,*

*"Ntigirwa na ciana. Nthii bantu nkwenda kuthii." Mbiti yamira, "nibu."*
Tembo na fisi walikua marafiki. Wakaafikiana wawe wakilala katika pango moja. Tembo alikua na wanawe na fisi vivyo hivyo.
Wakaishi kwa muda mrefu kwa lile pango moja. Walikua marafiki wa kufa kuzikana. Siku moja, tembo akamwambia fisi, "baki na wanangu niende mahali Fulani." Fisi akakubali. Tembo akaenda mahali, huko mbali walikoishi tembo wengine wengi.

Katika hadithi hii mtunzi amethihirisha ushirikiano na urafiki mkubwa kati ya fisi na ndovu kwani walilala katika pango moja na pia kuwalea wanao kwa pamoja. Hata ndovu alipopata shughuli za kwenda mahali tunapata kuwa fisi alilichukua jukumu la kuwatunza wana we ndovu bila pingamizi. Ule wimbo wa mwanatembo unatuchorea taswira ya jinsi watoto wa fisi walivyoweza kuangamizwa kwani walitumiwa kama kitoweo cha kuwatuliza wana wa fisi. Huyu mwanatembo anaenda akiradidi huuu wimbo kila anapokutana na wanyanyama njiani kuonyesha kuwa yale maelezo yake alitaka wanyama wamuonee huruma ili wamweleze alipokuwa mamake.kwa hivyo huu wimbo unazua taswira hisi.

*Gatungana na mbiti kaina,*
*"mbiti mukuria guku, mukuria guku*
*, mwanamwonera njogu ya cianyaga yatutigire nyomba na mbiti,*
*kana ka mbiti gakauga m…m….m…m…,*
*gakaurua ni indu ukulilila,*
*gakauga ni rutende rwa njogu nkuririra,*
*kutha na utigakuthe wica, kuthu!"*

(Akasafiri hadi akakutana na fisi. Akaimba:
"fisi mnaokula huku, mnaokula huku,
mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu"

Wanyama wanamwelekeza upande anakoishi mamake ndovu wa cianyaga. Maelezo ya wanyama yanazua taswia oni wanapomwambia;

*Unaona kule ng'ambo ile, ndiko aishiko ndovu wa Cianyaga."*
*…Akaambiwa, "unaona kule, ndiko aishiko mama yako."*

Taswira hii ni dhana inayoendeleza ujumi katika hadithi hii kwani kwa kupitia hizi picha za mawazo msikilizji anavutiwa na usimulizi vilivyo. Katika hadithi ya chura na

mbuni tunapata kuwa wanyama wote walikua na ushirikiano mkubwa kwani wanaamua kuchoma nyama pamoja. Wote walileta kuni na kisha wakachinja. Walipomaliza kuchinja wanachoma zile nyama na kuzila kwa pamoja.

> *Nyamu cionthe ni ciatirimanite bamwe. Cierana wa nyamu ice na tuku. Nyamu ciothe ciakua nku, Mathinja matwika nyamu ino nikaigwokia nyama. Ciokia nyama gwokia gwokia gwokia. Ciokia ciambiria kuria.*
> Wanyama wote walijumuika Pamoja. Wakakubaliana kila mnyama aje kuni. Wanyama wote wakabeba kuni. Wakachinja.Walipochinja wakaamua wachome nyama. Wakazichoma nyama wakaanza kuzila.

Mpango wao wa kuwinda, kuleta kuni, kuchoma na kuzila nyama pamoja ni taswira ya umoja na ushirikiano unaojengeka juu ya urafiki wao. Kwa jumla maelezo ya kifungu hicho yanaleta taswira ya maisha mema ya urafiki. Taswira hii katika utangulizi wa hadithi inaendeleza ujumi wa masimulizi unaokiuka uhalisia. Katika hali halisi, fisi huchukiwa kwa tabia zake za ulafi lakini katika hadithi hii anapendeza kwa kuwa ajenti wa umoja na ushirikiano ilhali tunamuona chura asiyetajwa kwa maovu yeye sasa ndiye ajenti wa uovu katika hii jamii. Taswira hii inafanya maisha ya urafiki kama huo kuwa ya kutamanika

#### 6.2.1.3 Dayalojia

Kwa mujibu wa tuki (1998), dayalojia ni mazungumzo ya ana kwa ana baina ya watu wawili. Katika ngano za Wachuka dayalojia ilibainika kutumika na kuendeleza hadithi. Wahusika katika hadithi waliweza kuwa na nafasi ya kuzungumza ana kwa ana na kusemezana mara kwa mara. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi kunatokea mazungumzo baina yao ndani ya hadithi wakati kindi aligundua kuwa mbaazi zake zinavunwa. Kindi wanazungumza na fisi ana kwa ana baada ya kindi kumwendea fisi na kumsaili kuhusu tukio hilo. Mathalan,

> *Riu kabare gakithii gakiuria Mbiti, "Mbiti' nuntu ni gweu urigirie ri, nuwonire uria untwirire nthoroko?" "Aari, aari cianjeru cianjeru ntageria kwona, ari ntamwona ntamwona.*
>
> ( "Fisi eti huwa unaniambia huwa humwoni mtu ambaye huiba kwangu na ni wewe tu huwa nakutana nawe?Hujawahi kumwona mtu akizichuma hizi mbaazi zangu ambazo zaelekea kuisha?"

"La! La! La! Sijamwona. Sijamwona. Sijamwona." Akamwambia.)

Kifungu hiki ni mazungumzo baina ya kindi na fisi. Kindi alitaka kujua endapo fisi alimwona aliyekuwa akiiba mbaazi zake. Fisi alimujibu moja kwa moja kuwa hajawahi kumwona mtu yeyote.

Mazungumzo mengine ya ana kwa ana yalitokea wakati kindi alimwendea fisi ili kuthibitisha tena endapo fisi humwona aliyekuwa akiiba mbaazi zake. Mazungumzo yafuatayo pia ni ithibati ya dayalojia katika hadithi ya fisi na kindi.

> *kamiuria "mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga na ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?"*
> *Aari aari ntamwona. Ntamwona, ntamwona."*
>
> akamuuliza"Fisi eti huwa unaniambia huwa humwoni mtu ambaye huiba kwangu na ni wewe tu huwa nakutana nawe?Hujawahi kumwona mtu akizichuma hizi mbaazi zangu ambazo zaelekea kuisha?"
>
> "La! La! La! Sijamwona. Sijamwona. Sijamwona." Akamwambia,

Kindi alimshuku fisi na kuamua kumsaili ana kwa ana. Kindi alilazimika kumuuliza fisi maswali huku fisi akijibu kwa kujitetea kuwa hajawahi kushuhudia mtu yeyote akiiba mbaazi za kindi. Dayalojia katika hadithi hii ziliweza kuwapa wahusika uhai wa kujismea na kuendeleza usimulizi na kuwa wamiliki wa tajiriba za matukio katika hadithi. Mtunzi anaanza kusimulia kisha wahusika wanachukua usukani na kuwa watendaji hai. Ingawa ni wahusika wa msimulizi wazua ujumi wa kimimesia kwa kuonyesha matukio halisi na kuyatenda. Dayalojia pia inatumika kuendeleza ujumi katika hadithi ya Ngongaoana na Gacinci. Ngongoana anzungumza na dadake ana kwa ana wakatia alikuwa akimkanya kuhudhuria ngoma za usiku. Yafutayo ni mazungumzo kati ya Ngongoana na dadake.

> *Gacinci akera Ngongoana, "kanthii rwimbo." Akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkaliwa ni malimalimu,"*
>
> (Gacinci akamwambia Ngongoana, "Ebu niende kwenye wimbo." Akamkanya .Akamwamwabia , "Usiende .Nitaliwa na mzimwi ."Kwa kuwa mazimwi yalikuepo .Akasikia akakosa kwenda .)

Ngongoana na zimwi waliendeleza mazungumzo ya ana kwa ana wakati zimwi lilifaulu kuingia chumbambani. Mazungumzo yafuatayo yalithibitisha yalikuwa ya Ngongoana na zimwi.

> *Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria.*

*Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi."Amwira, "niriathira."Amwira , "Ngua. Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria.*

(Zimwi lililokuwa karibu na lango likaingia . Likamwita, "Ngongoanga ," akaitika, "wuu." "Nipe maziwa." Akalipatia maziwa kwenye dundu likatisa, likanywa yote. Likamwambia, "Nipe mengine ."Likapewa maziwa mengine likanywa yakaisha.Likamwambia tena , "Ngongoanga ,nipe mengine."Akaliambia yameisha." Likamwambia, "Nibebe kama kuni ni mle nitakula ."Ngongoanga akachukua Kamba akalifunga zimwi huku akiwa haliwezi.)

Matumizi zaidi ya dayalojia yalibainika katika hadithi ya wasichana wanna wa Ukambani. Katika utangulizi wa hadithi, wasichana wote wanne wanapanga mazozezi kwa kuzungumziana ana kwa ana. Mipango yote inaandaliwa kwa maongezi ya moja kwa moja. Yafuatayo ni maongezi ya wasichana hao wakikubaliana kwenda mtoni kushindana.

*Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii, u ukaringia munyiri rugongo ruria atuike niwe ena njarumi I mbega. Na ururia akaguithia runciini atuike njarumi yawe ti mbega tucoke tugacawe riingi."*

(Wakaenda Kuchongwa Meno. Baada ya shuguli hiyo kukamilika, waliambiana "Twendeni mtoni tuone nani ataweza kutema maji kupitia kwa mwanya wa meno hadi ng'ambo ya pili. Atakayefanya hivyo ndiye atakayesemekana kuwa na mwanya mzuri zaidi. Atakayeshindwa kufanya hivyo, asemekane kuwa na mwanya duni, hivyo arudi akachongwe tena.")

Mazungumzo mengine yanayoendelea katika hadithi iyo hiyo ni baina ya Nyaga na wazazi wake na nyanyake akiwafahamisha kuwa Mweru angali hai na ametupwa kwenye shimo moja huko marishoni. Yafuatayo ni mazungumzo hayo:

*Kathii kera ng'ina, "Umenye, Mweru ari bo ii?" Ng'ina akaringa na mwiko "niuu ucite kuririkania kiriro ki naririre ngica gugakira?" Kathii kiri ithe, ithe akaringa na muthambicho. Nyaga ri kathi gakiriraga wa gwa icue. Kathii kamwita, "cucu" etika amwira "Umenye, umenye Mweru ari bo ii? Tiga ugu twiragwa niarirwe ii? Ari kuu nthi, mbikarire ibiga negwa akina kuu nthi maita megana? Mairi cucu, Indi nkiira aciari makwa mambiriria kundumia. Riu ni tuma nkurira. Era "guti na thiina ii, ni niu nkameera."*

( Yule kijana akaamua kuwarejesha mbuzi nyumbani. Alipofika, akamwambia mama yake, "Wajua Mweru angalipo." Mama akampiga kwa mwiko. Akamwuliza "Kwa nini unanitonesha kidonda?"

> Akaenda alipokuwa babake. Baba mtu akampiga kwa mpini. Akaenda huku akilia. Akafika kwa babu yake. Akamwita, "Babu,"akaitikia. Akamwambia, "wajua, Mweru angalipo, Japo huwa tunaambiwa kuwa aliliwa. Yumo humo chini. Nilikalia jiwe nikaskia akiimba huko chini. Aliimba mara mbili babu. Nilipowaambia wazazi wangu wakaanza kunipiga. Ndiyo maana ninalia."
>
> Babu akamwambia, "Hakuna tashwishi. Binafsi nitamwambia," Wakaenda hadi nyumbani. Babu akawauliza, "Eti mmemwadhibu Nyaga kwa nini?" "Ametwambia mambo ya kishetani; eti Mweru angalipo hali twajua vyema kuwa alikufa." Baba akajibu. Mama yake alipoulizwa, alijibu, "anatutonesha kidonda kwa kutuambia kuwa Mweru angali hai nasi tunajua kuwa aliaga dunia kitambo.")

Katika hadithi ya chura na mbuni tunapata kuwa kuna mazungumzo ya ana kwa ana kati ya chura na wanyama wenzake; *Riu kaura gakinamenererua ni nyamu cionthe gakinaurwa, "Nee kaura muntu ati matina ubirite nku cia miboru ku? Ana nyama cietu tutikurumia." Kaura kauga ambikare aa nkoona."* (Chura akadharauliwa na Wanyama wote akaulizwa, "Nawe chura uso makalio umepeleka hizo kuni zako wapi?" Hatutakupatia nyama zetu. Chura akasema, "Nitakaa hapa nione.")

Mazumngumzo yao yaliendelea;

> *Kaura nako ri, gatikurumwa. Nikerwa, "Kaura muntu ati matina ucite aa kurutha atia bo?" Kaura kathura gaciuria, "Tauntu mukumbira ugu, mukanyua runci mwaruta ku?" "Tukanyua muburoni" "Indabwethia?" "Gukabwethia miburo yonthe ?" "ii" Niu nindi mbwethie runci, namwi timwona gia kunyua. Mone kana nyama inu cienu ikamutethia mutinywite runci."*
>
> Chura naye hakupewa akaambiwa, "Chura aso na makalio amekuja hapa kufanya nini?" Chura akakasilika. Akawauliza, "Hivi, mnaponiambia hivyo mtatoa wapi maji ya kunywa?" "Tutakunywa mtoni." "Na nikiikausha?" "Kwani utakausha mito yote?" "Na hivyo mimi nitaenda nikaushe mito, nanyi hamtapata ya kunywa. Nione iwapo nyama hizo zenu zitamfaa bila kuyanywa maji.

Wanyama wanapoondoka kutafutata maji mitoni baada ya kula nyama na kushiba walipata kuwa kweli mito haikuwa na maji bali matope yalijaa. walikuwa na kiukikubwa nandipo walipoona watakufa kiu walisemezana na kukubaliana wamwite chura wampe nyama ili arejeshe maji, hivyo tunapata mazungumzo kati ya wanyama; *Wa mbiti imwe yaaciira, "Untu tukwona baba nibo kaura kari. Nitugakaire muno i, tukarumie nyama i, nitugukua ni inonta." Riu ciambiriria guitana, kaura kaura," Kaura kaumira "Bai titukwima nyama ringi ii, tukwenda gukua wa bu utwirire ii,*

*tukundie runci i, natwi ri tukurumie nyama. Nuntu nituthigia kunywa tukona ni mutonto.”*

*Nyamu yetagwa nyaga yauga, “Niu runci rwa kaura, ntirukunda. Na nyama ciakwqa ntirumia kaura”.Nyamu iria cingi cionthe ciambiria kurumia kaura. Kaura karia kegua nikaremirwe ni kuria nuntu nikarumwa ni nyamu cionthe indi nyaga niregire.*

*Nyaga yakairwa ni nyamu inu ciingi yerwa, “Nyaga, i rumia kaura nyama nugukua ni inonta.” “U? Niu ntikunda runci rukuthambwa ni kaura na nthonjo ikiangaga ku. Ntirukunda na ntirukunda. Nani, ana mwarutirwa nyinci ni mwiu mukanyua niu ntinyua indi,ntilukunda na ntikalumia nyama niu ntikarumia* (Fisi mmoja akamwambia, “chura huyu hapa. Tumbembeleze mno, tumpe nyama ili tusife kiu.” Wakaanza kumuita chura. Chura akatokea. “Tafadhali hatutakunyima nyama tena. Tu karibu kufa kama ulivyotuambia. Tupe maji nasi tukupe nyama. Kwa kuwa tumeshindwa kuyanywa haya.

Mnyama mmoja kwa jina mbuni akasema, “mimi sitayanywa maji ya chura. Na nyama zangu sitampatia.” Wanyama hao wengine wote wakaanza kumpa chura. Chura akala akashiba. Alipewa nyama na Wanyama wote isipokuwa mbuni. Mbuni alibembelezwa na Wanyama hao wengine akaambiwa, “Mbuni mpe chura nyama. Utakufa kiu.” “Nani? Mimi sitayanywa maji anayooga chura tena yenye nongo. Sitayanywa. Hata mkipewa maji nyie mtayanywa. Mie sitayanywa wala kumpa chura nyama).

Nyamu yetagwa nyaga yauga, “Niu runci rwa kaura, ntirukunda. Na nyama ciakwa ntirumia kaura”. kupitia haya mazungumzo tunapata mgogoro kati ya chura na wanyama wenzake unaanza kukua. Mazungumzo haya yalileta uadui mkubwa kwani chura alihisi kuwa amedharauliwa kwa kutusiwa na pia kunyimwa nyama na wenzake. Baada ya hapa tunamwona chura kama mwenye kisasi kwani alilaani mito yote ikauke. Tendo hili lilikuwa la kuwadhulumu wenzake kwani maji ni uhai hasa baada ya kula nyama wanyama wangehitaji maji ya kunywa kwa wingi lakini chura alikuwa amekausha mito. Mazungumzo haya yametumika kumjenga mhusika mbuni na kuonyesha mbuni kama mwenye hasira na fisi kupewa sifa ya mwenye kupenda uridhiano, hivyo kuleta ujumi katika hadithi hii.

Vifungu hivi ni ishara ya matumizi mapana ya dayalojia katika ngano za Wachuka. Mazungumzo haya yalikuwa yakiendelea katikati ya hadithi kama sehemu ya kuendeleza usimulizi. Dayalojia inatumika kiujumi kujenga uhai wa wahusika na kuibua mandhari halisi ya kijamii katika ngano za Wachuka. Wahusika wanakuwa si vinyago bali ni wenye pumzi na wenye kutenda kwa uhai.

### 6.3 Mbinu za Lugha

Kwa mujibu wa Senkoro (1980), mbinu za lugha aghalabu huwa tamathali za usemi ambazo huwa maneno, sentensi au misemo na hutumika kiupamba kazi ya fasihi simulizi. Tamathali za usemi ni maneno kama vile tashibihi, tashihisi, takriri, chuku na kadhalika (Wamitila, 2000). Katika ngano za Wachuka tamathali mbili kuu ziliweza kudhihirika kimatumizi na kuendeleza ujumi. Tamathali hizo ni takriri na chuku.

#### 6.3.1 Takriri

Kulingana na misingi ya nadharia ya ujumi wa kinudhuma, mistari na aya hazipangwi tu kwa mujibu wa sheria za kishairi, lakini pia hutumiwa kuwasilisha ujumi na tajiriba ya pamoja ya jamii husika kwa kutumia takriri. Mawazo hayo ya nadharia iliyorejelewa yanasisitiza nafasi maalumu ya takriri kiujumi katika matini za fasihi. Kwa mujibu wa Wikipedia (2021), takriri ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani. Takriri kama mbinu ya kimtindo ilibainika kutumika katika ngano za Wachuka. Kwa mfano, kauli zifuatazo katika hadithi ya fisi na kindi:

> *…cierana niciunge itema, ciaunga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko.*
> Wakakubaliana wapalilie konde wapande mbaazi. Wakapanda mbaazi.Mbaazi zilipokomaa,kindi akawa akienda kuchuma zake.

Fisi na kindi baada ya kufanya urafiki walikubaliana wapalilie shamba ili wapande kunde. Kifungu hiki kinarudiaudia mawazo na matendo ya uamuzi wa fisi na kindi kama marafiki. Uradidi pia unajitokeza katika maneno ya fisi akikana kuwa hakuwahi kumwona mtu yeyote akiiba mbaazi za kindi. Tazama kauli ifuatayo ya fisi:

> *"Aari, aari cianjeru cianjeru ntageria kwona, ari ntamwona ntamwona.*
>
> "La! La! Cheupe cheupe, sikumwona."

Fisi anarudiarudia karibu kila neno katika kifungu hiki alipokuwa anajitetea. Uradidi huu unabainisha unafiki wa fisi wa kujaribu kujifanya mwema ilhali yeye ndiye mwizi wa mbaazi. Fisi alirudiarudia maneno hayo kama mbinu ya kumshawishi kindi na kujaribu kujiondolea lawama.

Kadhalika, takriri ilijitokeza katika mishororo ya nyimbo. Kwa mfano katika wimbo ufuatao wa tambiko:

*Kabare kaina;*
*Ntarumaa x2*
*muthoroko x2*
*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

Mshororo wa kwanza na wa pili unaimbwa ukirudiwarudiwa mara mbili. Takriri katika hadithi hii ilitumika kiujumi kubainisha silka za wahusika wema na wawi katika hadithi. Takriri pia inajitokeza katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci. Matendo ya wahusika yanarudiwarudiwa. Kwa mfano kurudiwa kwa hatua za Gacinci Kwenda ngoma ya usiku:

*Athii. Athi. Akinya rwimboni*
(Akaenda, akaenda akafika kwenye ngoma)

Gacinci anafululiza hadi kufika kwenye ngoma. Mfulilizo huo unaonyeshwa kwa uradidi wa mwendo wa safari.

Mfano zaidi wa takriri unabainika katika kifungu kifuatacho kutoka kwa hadithi ya Ngongoana na Gacinci:

*Athii akiriraga. Athii akiriraga,*
(Akaenda akilia, akaenda akilia)

Matendo ya mwendo na kulia kwa Ngongoana alipokuwa amelibeba zimwi yanarudiwarudiwa. Ngongoana akaenda akilia. Takriri zaidi inadhihirika katika uradidi wa maneno katika mishoro ya wimbo. Kwa mfano katika wimbo wa Ngongoana ufuatao;

*Gacinci ii Gacinci mwile ndagukanilie wathi*
*(Wa utuku Gacinci mwile) x3*

Kidokezo hiki cha wimbo kinaonyesha urudiaji wa jina la Gacinci.

Mtindo huu wa urudiaji wa maneno na vifungu uliunduliwa katika hadithi ya Wasichana wanne wa Ukambani. Mtunzi alirudiarudia kutendeka kwa matukio kama ilivyo katika mfano ufuatao kutoka kwa haadithi:

*Macoka ringi gucawa, mathii macawa ringi.*

Wasichana wengine waliposhindwa na Mweru kuvusha mate kwenda ng'ambo ya pili kupitia mwanya wa meno, walikubaliana kwenda kuchongwa tena. Kadhalika takriri katikamhadithi hiyo iliendelezwa kwa kurudia maneno na mishoro katika wimbo. Tazama mfano ufutao wa wimbo wa Mweru akiwa shimoni:

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*Nitwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

Mshororo '*Nkanga cia Maindi'* unarudiwarudiwa katika wimbo huo. Matumzi takriri katika hadithi hii yalibanika kuwa ya kutilia mkazo matukio na na ujumbe. Katika hadithi ya chura na mbuni takriri imetumika kusisitiza suala linayoloathiri wahusika, kwa mfano tunapata kuwa chura anaposema kuwa atakausha mito suala hili ni kuu kwani wanyama wanahitaji maji hasa baada ya kula nyama. Wanatia shaka kuwa chura anuwezo wa kunyausha mito.

*Nyamu iria ciambiriria kuthekera kaura igikeraga, "Ana* ***ukabwethia utibwethia*** *yonthe, tukanyua runci, runci tukanyua. Gutibu* ***ubota kubwethia*** *miburo yonthe.* ***Thii ubwethie*** *ni."*

Tishio la kufanya mito inyauke lilitiliwa shaka na wanyama wote kwani waliona kama jambo lisilowezekana. Katika mazungumzo ya wanyama tunapata jina Kaura limerudiwarudiwa sana.

*Nitugakaire muno i, tukarumie nyama i, nitugukua ni inonta." Riu ciambiriria guitana,* ***kaura kaura," Kaura*** *kaumira*

Hii ni kwa sababu ni mhusika aliyekuwa na nafasi kubwa sana katika ufumaji wa hii hadithi. Ametumika kuendeleza maudhui ya ubinafsi na dhuluma, pia amewajenga wahusika wengine kama vile mbuni. Wanapomuita kwa kurudia rudia jina lake, ilikuwa ni mbinu ya kumbembeleza ili kutuliza hasira zake.kwa njia hii wema unashinda uovu

kwani anakubali kurejesha maji na wanyama wakanywa. Mbuni alisisitizakuwa hangeyanywa maji ya chura kwa kurdia neon kuwa; sitayanywa sitanywa maji ya chura. Kifungu hiki kinaonyesha kauli hiyo;

> "***Niu ntikunda*** *runci rukuthambwa ni kaura na nthonjo ikiangaga ku.* ***Ntirukunda*** *na* ***ntirukunda.*** *Nani, ana mwarutirwa nyinci ni mwiu mukanyua niu ntinyua indi****, ntilukunda*** *na ntikalumia nyama niu ntikarumia*."

Takriri imetumikakusisitiza utaratibu wa mwendo wa chura kama ifuatavyo;

> *Kaura niko kau.* ***Kathii, Kathii, kathii*** *gakinya bantu kethiriria mbiti kairi. Kaina muthunthuri….."*

Katika ngano ya fisi na ndovu takriri imetumika kuonyesha uhusiano na urafiki wa karibu kati ya ndovu na fisi. Wametumia neno 'muno' (sana) mara mingi. Tunapata maelezo haya;

> *Riu,* ***ciekara muno muno muno*** *ikilalaga irimani rimwe. Ciikarite muno, ntuku imwe njogu niyerire mbiti nuntu numendanite muno*,

Pia neno hili limerudiwa kuonyesha muda walioishi na kulala katika pango moja ulikuwa mrefu. Hii ni kinyume na uhalisia kwani fisi na ndovu hawatangamani porini. Ushirikiano umeendeleza ujumi katika ufumaji wa ngano hii.

Takriri katika kifungu kifuatacho imetumika kusisitiza muda aliokaa mama ndovu*;*

> *Riu njogu* ***yekara*** *njoguni****. Yekara yekara yekara yekara*** *itikwinuka nabo ikalala nabo*

Maneno ya mwanawe fisi aliyotoa akilia kumla mwanatembo yamerudiwarudiwa katika usimulizi na wimmbo wa mwana tembo, mfano

> *"m..m..m..m..!" "Ni indu ukulilila?" "Ni rutende rwa njogu nkulilila." "Kutha na utigakuthe wica."*

Takriri hii imetumika kuendeleza usimulizi na pia kusisitiza dhuluma walizopitia watoto wa ndovu. Pia uradidi huu unasisitiza sifa mbovu ya fisi na wanawe ya ulafi na ubinafsi.

Mwana wa ndovu anafululiza hadi kufika malishoni alipokuwa mamake. Mfululizo huo unaonyeshwa kwa uradidi wa mwendo wa safari. Kifungu hiki kinaonyesha huo mwendo;

*Kaana **kathii kathii kathii kathii** .... Kethira nthuni. ""Auuuu! **Tituthii! Tuthii** tukonane na mbiti." "Ari, niu ntikinya nau ringi. Nkariwa ni mbiti ugu twana twetu turaririrwe... Kaana karumirira ng'ina. **Ciathii ciathii ciathii**... Ciakinya kibwai.*

Katika hadithi hii takriri imetumika kusisitiza mwendo, uhusiano wa wahusika na ujumbe.

### 6.3.2 Chuku

Chuku ni maelezo yaliyotiliwa chumvi. Jambo la kawaida hufanywa kuwa si la kawaida huku lisilo la kawaida kufanywa kuwa la kawaida (Kuhenga, 1977). Katika ngano za Wachuka, chuku ilijengeka kwa kuyafanya mambo yasiyo ya kawaida kuwa ya kawaida. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi Wanyama wanapea uwezo wa kuendeleza ya kawaida kama vile kufanya urafiki na kulima. Kwa mfano,

> *Mbiti na kabare ciatumire urata cierana niciuge itema, ciauga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko.*
> ( Fisi na Kindi walikuwa marafiki. Wakakubaliana wapalilie konde wapande kunde. Wakapanda kunde).

Fisi na kindi wanafanya mambo ya kawaida kama wenye tajiriba kama binadamu. Uwezo huu wa kuwa na tajiriba ya kawaida unatilia chumvi jambo lisilo la kawaida kuweza kuwa la kawaida. Matukio mengine yaliyotiliwa chumvi ni pamoja na kindi kumoji fisi kisha kuandaa tambiko la kuamua ni nani mwizi wa mbaazi za mwingine.

Mktadha mwingine wa matumizi ya chuku katika ngano za Wachuka ulidhirika kwenye ujenzi wa hadithi ya Ngongoana na Gacinci. Gacinci wanaelewana kilugha na zimwi. Kuelewana kilugha baina ya binadamu na zimwi si jambo la kawaida ila katika hadithi hiyo linafanywa kua la kawaida. Zimwi liliingia chumbani na kumwita Ngongoana kisha wanaanza mazungumzo.

> *Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria.*
> *Riamwira, "ngundia ingi" Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi." Amwira, "niriathira." Amwira, "Ngua. Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria.*
>
> ( Zimwi lililokuwa karibu na lango likaingia .Likamwita, "Ngongoanga ," akaitika, "wuu." "Nipe maziwa." Akalipatia maziwa kwenye dundu likatisa, likanywa yote .Likamwambia, "Nipe mengine ."Likapewa maziwa mengine likanywa yakaisha.Likamwambia tena , "Ngongoanga

,nipe mengine.”Akaliambia yameisha.”  Likamwambia, “Nibebe kama kuni ni mle nitakula .”Ngongoanga akachukua Kamba akalifunga zimwi huku akiwa haliwezi .Akalibeba kwa kujitahidi .Akaenda akilia .)

Haya ni mazungumzo yaliyofanywa ya kawaida baina ya Ngongoana na zimwi mle chumbani. Tukio hilo ni la chuku kwani zimwi si kiumbe chenye tajiriba ya mawasiliano na binadamu. Chuku katika hadithi ya wasichana wanne wa ukambani inaibuliwa katika hitimiso ya hadithi. Hadithi inaisha kwa wasichana kubadilika na kuwa vipepeo wakiwa njiani isipokuwa Mweru.
*Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe.*

Mweru alipokuwa akiwasindikiza wasichana wenzake walibadilika wote na kuwa vipepeo kwa sababu ya kumhujumu Mweru.

Hatima ya wasichana hao inatiliwa chumvi. Katika hadithi ya chura na mbuni chuku inaibuliwa tunapomwona chura akiendeleza chuki kwa kukanyausha mito yote hivyo wanyama waliomdharau kukosa maji. Chura amepewa uwezo wa kufanya miujiza yaani mambo yasiyo ya kawaida kwani wanyama wanapomuomba msamaha anarejesha maji.

*Kaura kauma au kathurite mono nuntu wabu gakwimwa nyama ti mathe, kathii gakibwethagia miburo Kabwethia kabwethia kabwethia, miburo yathira*

( Chura akaondoka hapo akiwa amekasilika sana kwa kuwa alinyimwa nyama kama mzaha. Akaenda akakausha mito yote. )

Pia tunamwona mbuni akiwa na uwezo wa kulaani chura na wanawe kwa sababu ya tendo alilotenda na laana inashika chura anafura miguuna vikembe vyake vikaanza kuaga.

*“Kaura gatigwa nako ri, gakurumwa ni Nyaga.Gatigwa runcini nuntu nigekaraga runcini ri, twana twa kaura twambiriria gukua.*
*Kaura nako kambiriria kwimba maguru. Kaura kamenya nkugwatwa ni kirumi kia Nyaga”*

(Chura akaachiwa laana na mbuni. Vikembe vya chura vikaanza kufa. Chura naye akaanza kufura miguu. Chura akafahamu kuwa laana ya mbuni ilikuwa imemfika.)

Chuku imetumika kuelezea ulafi wa motto wa fisi kwani tunapata kuwa alilia kumla mwa ndovu kila siku bila kutosheka.

*Riu riria mbiti nayo yatigirwe twana, wa kibwai giakinya, kaana ka mbiti gakambililia kulila. Gakauga , “m..m..m..m..!” mbiti igakauria, “*

*Ni indu ukulilila?" Gakauga, "Ni rutende rwa njogu nkulilila." Gakerwa, "kutha na utigakuthe wica."*

(Kila jioni,kikembe cha fisi kingeanza kulia na kusema, "m…m…m…m… ninalilia mwana wa ndovu." Fisi angemwambia, "ng'ata ila usimg'ate kwa nguvu." Papo hapo, mwanatembo angeliwa bila kusazwa na vikembe vya fisi. )

Chuku katika ngano hizi ilibainika kuwa na matumizi ya kiujumi kujenga fantasia na ulimwengu wa masimulizi kutenganishwa na ulimwengu halisi wa hadhira.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Utangulizi

Sehemu hii ilishughulikia muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Mtafiti alitanguliza kwa muhtasari uliozingatia malengo yote matatu ya utafiti. Sehemu ya pili iliangazia matokeo ya utafiti. Kitengo cha tatu kilishughulikia hitimisho kisha kufuatwa na mapendekezo ya utafiti wa usoni.

## 7.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa wa uhakiki mwega wa ujumi katika ngano simulizi za wachuka. Madhumuni yalikuwa kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka, kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka na kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa kuchangia maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ya Wachuka, kufanikisha uhifadhi wa ngano za Wachuka kama kipera muhimu cha fasihi simulizi ya kiafrika na fasihi kwa jumla. Utafiti huu umechangia katika kukuza hadhi ya ujumi wa fasihi simulizi ya kiafrika. Umekuwa nyenzo ya kuhifadhi utamaduni mila na desturi za Wachuka kama jamii mahususi. Pia, utafiti huu umekuwa na umuhimu kwa wahakiki wa masuala ya fasihi na walimu watafiti.

Utafiti huu ulifanyiwa nyanjani kwa kukusanya ngano kutoka kwa watambaji wa ngano katika tarafa ya Chuka. Mtafiti alichanganua vipengele msingi vya ngano za wachuka kiujumi kwa kuongozwa na nadharia ya ujumi wa kinudhuma.

Utafiti huu ulipangiliwa katika sura saba. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, vikwazo vya utafiti kisha maelezo ya istilahi. Suala la utafiti likuwa kuchunguza na kubainisha mwega wa ujumi katika ngano za Wachuka ili kuonyesha ufasaha wake kisanaa na kiufundi uliofikiwa katika utunzi na uwasilihaji wake kiujumi.

Malengo na maswali ya utafiti yalikuwa matatu: kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka, kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka na kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Utafiti huu ulikuwa na umuhimu wa kuchangia maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ya Wachuka, kufanikisha uhifadhi wa ngano za Wachuka kama kipera muhimu cha fasihi simulizi ya kiafrika na fasihi kwa jumla. Utafiti huu umechangia katika kukuza hadhi ya ujumi wa fasihi simulizi ya kiafrika. Umekuwa nyenzo ya kuhifadhi utamaduni mila na desturi za Wachuka kama jamii mahususi. Pia, utafiti huu umekuwa na umuhimu kwa wahakiki wa masuala ya fasihi na walimu watafiti. Utafiti huu ulishughulikia mwega wa ujumi pekee katika ngano za Wachuka.

Sura ya pili ilishughulikia mapitio ya maandishi na misingi ya nadharia. Sura hii ilishughulikia maandishi yaliyohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti alirejelea na kuhakiki maandishi muhimu yaliyoendana na malengo ya mada ya utafiti. Katika utangulizi mtafiti alishughulikia jamii ya Wachuka na fasihi simulizi yao. Kadhalika mtafiti alipitia maandishi yaliyoandikwa kuhusu utafiti wa fasihi simulizi, utafiti katika suala la ujumi, kipera cha ngano, lugha ya kimasimulizi na mguso tamthali za usemi na wahusika wa kisimulizi.  Sehemu hii ilihitimisha kwa kubainisha misingi ya nadharia ya ujumi wa kinudhuma.

Sura ya tatu iliangazia mbinu za utafiti na mbinu za uchanganuzi wa data. Sehemu hiyo ililenga kujadili mbinu ambazo mtafiti alitumia katika ukusanyaji, uanishaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu. Sura ilitangulia kwa kudahali muundo wa utafiti huu utafiti huu ukikuwa wa kithamano. Sehemu hii ilishughulikia pia mahali pa utafiti. Utafiti ulikuwa nyanjani uliondelezewa katika tarafa ya Chuka. Sura hii iliangazia uzingatiaji wa maadili ya kitafiti. Uteuzi wa sampuli wa kimakusudi na ule wa kimarejeleo ulitumiwa. Njia ya ushuhudiaji ilitumika kama kifaa cha kukusanya data. Kadhalika mtafiti alifafanua mbinu ambazo zilitumiwa kuchanganua data na kuwasilisha matokeo.

Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu ya utafiti: Kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka, kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka na kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Sura ya nne ilihusu uchanganuzi wa mtiririko wa matukio katika ngano za Wachuka kwa nia ya kujibu swali la kwanza la utafiti. Mtiririko wa matukio kiujumi uliweza kuchanganuliwa na kufafanuliwa. Sehemu hii iliweza kubaini kuwa mtiririko wa matukio kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka hufuata utaratibu wa ngazi tatu za matukio. Utangulizi kuchukua nafasi ya tukio la wema, kati kuwa sehemu ya msukosuko wa mwenendo na hitimisho kuwa harakati za kupata haki au ukombozi. Kwa jumla, mtitiriko wa matukio kiujumi uliweza kubainishwa na kuthibitishwa.

Sura ya tano ilishughulikia wahusika wa kisimulizi katika ngano za Wachuka ili kujibu swali la pili la utafiti la kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Mtafiti aliangazia sifa za wahusika wa kisimulizi katika katika ngazi mbili: Wahusika wema na wahusika wawi. Mtafiti aliweza kuthibitisha kuwa wahusika wema na wawi huendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

Sura ya sita ilinuia kujibu swali la tatu la utafiti kwa kuchanganua mbinu za kimtindo katika ngano simulizi za Wachuka. Mbinu za kimtindo zilizochanganuliwa ni pamoja na mbinu za kisaana na mbinu za lugha. Utafiti ulibanisha kuwa mbinuza kisanaa hasa nyimbo, taswira na dayalojia zilitumika kuendeleza ujumi katika nagano simulizi za Wachuka. Kadhalika, mbinu za hasa takriri na chuku zilitumika kuendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Kwa jumla sehemu hii iliweza kubainisha kikamilifu mbinu za kimtindo zilivyotumika kuendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Sura ya saba ilihitimisha kwa muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

### 7.3 Hitimisho

Utafiti huu ulitarajiwa kutimiza malengo matatu ya utafiti: Lengo la kwanza lilikuwa kuchunguza kuchunguza jinsi mtiririko wa matukio huendelezwa kiujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka, Kutokana na matokeo ya utafiti iligunduliwa kwamba mtiririko wa matukio huendeleza ujumi katika ngano simulzi za wachuka.

Matukio hufuata ruwaza maalumu kwa ngano kutangulizwa kwa tukio la wema kisha msukosuko wa mienendo na kuhitimishwa kwa tukio la kupata haki au ukombozi. Mtiririko wa matukio kiujumi ulibainika kuwa kiini cha mwega wa ujumi katika ngano simulizi za wachuka.

Lengo la pili la utafiti lilikuwa kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Matokeo yalithibitisha kuwa wahusika hugawika mara mbili kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Wahusika wema na wawi ambao sifa zao hutumika kuendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

Lengo la tatu la utafiti lilihusu kuchanganua mbinu za kimtindo zilivyotumika kuleta ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa mbinu za kisanaa na za lugha hutumika kuendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Mbinu za kisanaa kama vile nyimbo, taswira na takriri zijumuika katika muundo wa kila ngano na kuwa na uamilifu wa kuipa ngano ufaafu wa kimasimulizi kidhima katika jamii ya wachuka. Mbinu za lugha hasa takriri na chuku zilibainika kuwa mwega wa ujumi katika ngano simulzi za Wachuka kwa kuimarisha uhalisia wa matukio na kutimiza dhimay katika funzo Imani za jamii ya Wachuka.

Kwa jumla, imeafikiwa kuwa mwega wa ujimi katika ngano simulizi za Wachuka huendelezwa na mtririkao wa matukio kiujumi, sifa za wahusika kisimulizi na mbinu za kimtindo hasa mbinu za kisanaa na za lugha.

### 7.4 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu umeweza kuthibitisha kuwa kuna mwega wa ujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Hata hivyo, utafiti zaidi wa ngano pamoja na tanzu nyingine za fasihi simulizi unahitajika. Utafiti huo unafaa kuegemea kukuza fasihi simulizi jadi ya Kiafrika pamoja na fasihi simulzi ya kisasa. Pia, pana haja ya ngano simulizi za Wachuka kuenziwa kama fasihi simulizi asilia, jadi na Kiafrika.

Matokeo ya utafiti yalionyesha haja ya kuwepo kwa utafiti wa usoni. Ilitambulika kuwa mwega wa ujumi katika ngano simulizi za jamii husika. Masuala mengine ya ujumi

kama vile ujumi mweusi hayakuangaziwa ingawa yanaweza kuwa na nafasi katika ngano za Wachuka. Mtafiti anapendekeza:

i) Utafiti kufanyika ili kuabainisha visakale katika ufumaji wa ngano za Wachuka.
ii) Utafiti wa kiontolojia kuendelezewa ngano za Wachuka.
iii) Utafiti zaidi wa motivu katika ngano za Wachuka unafaa kufanywa.
iv) Kuchunguza jinsi kanuni za mawasiliano zilivyokiukwa katika ufumaji wa ngano za Wachuka.

## MAREJELEO


Alembi, E. (2002). *The Construction of Abanyore on Death through Oral Funeral Poetry* (Doctoral Dissertation, PhD Thesis. Helsinki University Press).

Bakhtin, M. (1981). The Dialogic Imagination (C. Emerson & M. Holquist, Trans.).

Chacha, M. (1997). *Majigambo ya Kikuria.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Hymes, D.H. (1970). Linguistic method in ethnography: Its development in the United States. In P. Garvin (Ed.), *Method and theory in linguistics*. The Hague: Mouton.

Eagleton, T. (2011). *Literary Theory: An Introduction*. John Wiley & Sons.

Finnegan, R. (1977). *Oral Traditions and Verbal Arts; Guide to Research.* London: Routledge.

Guthrie, M. (1976). *The Classifications of Bantu Languages.* London: Dawsons of Pall mall.

Hammermeister, K. (2002). *The German Aesthetic Tradition;* Cambridge University Press, U.k

Harmon W., & Holman, H. (2000). *A Handbook of Literature ( 8th Edition)* . Upper Saddle River: Prentice Hall.

Hegel, G. (1997). *Introduction to Aesthetics.* London: Oxford University Press.

Jacobson, R. (1960). Linguistics and Poetics, Style in Language, 350–77. *New York, N*

Kabira, W., & Mutahi, H. (1988). *African Oral Literature.* Nairobi: Longman Kenya.

Kiganza, P. ( 2011 ) . *Ujumi katka ushairi wa mnyampala*: The University of Dodoma press, Dodoma

Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers.

Kuhenga, C. (1977). Tamathali Za Usemi.*Y: Ed. Th. Sebeok.*

M` imanyara, A. (1992). *The Restatement of Bantu Origin and Meru History.* Nairobi: Longman Publishers.

M‟Ngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Madumulla, J. (2011). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi.* Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.

Mathooko, P. (2006). Fasihi Simulizi: Chombo Hifadhi cha Lugha za Kiafrika. Katika K. Njogu, Momanyi C & Mathooko P.M (wah), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications.

Matti, G. (1993). *Sanaa za Maonyesho za Kiafrika za jadi: Mfano wa Tohara ya Watharaka*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili(Haijachapishwa ) Chuo Kikuu cha Moi.

Mbaabu, I. (1978). *Methali, Vitendawili na Mashairi ya Kimeru.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni Wa Waswahili.* Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing.

Miruka, O. (1994). *Encounter With oral Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mitambo, E. (2018 ). Taswira za Mtoto wa Kiume katika Ngano za Watharaka.Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Chuka, kenya .

Mlacha, S. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mohamed, S. (1995). *Kunga za Nathari. Katika Kiswahili.* Nairobi: East African Educational .

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki Wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O., & Mugenda A. (2003). *Research Methods. Quantitative Approaches and Qaulitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mugenda, O., & Mugenda, A. (1999). *Research Methods. Quantitative Approaches and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mulokozi, M. (1983). Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamhuri Inayobadilika. *Semina ya Fasihi Simulizi* (pp. Uk 21-33). Dar es Salaam: Jarida la 184 Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. (2003). Utafiti wa fasihi simulizi. *makala ya semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.* (pp. 18-26). Dar es Salaam: TUKI.

Mutegi, (2012). *Taswira ya Mwanamke katika Ngano za Wamuthambi*, Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka, Kenya.

Mutegi, L. (2010). *Maigizo Katika Fasihi Simulizi : Mfano wa Kirarie katika Nyimbo za Tohara ya Wameru.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili(Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mutiso, K. (2005). Utenzi wa Hamziyyah (The Hamziyyah Epic. A Detailed Analysis of a Swahili Islamic Epic). *Institute of Kiswahili Research, University of Dar-es-Salaam, Dar-es-Salaam, 2005; 360+ 15 pp*.

Mwaniki, H. (2004). *Chuka Historical Texts.* Nakuru: Nakuru Media Document Supplies

Ndege, M. (2003). Gender and The Oral Narrative among The Ameru. In Kabira, *Contesting Social Death* (pp. 153- 156). Nairobi: Kenya oral literature Association.

Ndimofor, N. (2011). *Oral Literature of the Akum People: A Study of the Folksong and Cultural Elements* (Doctoral Dissertation, Ecole Normale Superieure).

Ndungo, C. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Ndungo, C. (1997). *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Nairobi: University of Nairobi.

Ngure, A. (2007). *Fasihi Simulizi kwa Shule Za Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation .

Ntarangwi, G. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Rock Island: Augustana College.

Oyoyo, J. (2013). *Uhakiki wa Fani Katika Ngano za Kiswahili.* Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Simala, I. (2006). Fasihi Simulizi Katika Enzi za Utandawazi katika. In Njogu et al, *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* (pp. 11-18). Nairobi: Nairobi Twaweza Communications.

Steere, E. (1970). *Swahili Tales and as Told by Natives of Zanzibar.* London: Harvard College Library.

Timmamy, R. (1990). *Uhakiki wa Ngano za Kiswahili.* Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics.( 2nd ed).* England: pearson education ltd.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi : Istilahi na Nadharia* . Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books.

Wellek, R. (1965). *Theory of Literature.* Harcourt: Penguin Books.

Zirimu, P. (1971). An Approach to Black Aesthetics. *Nairobi, Kampala and Dar es Salaam: East African Literature Bureau in Black Aesthetics (Eds) Pio Zirimu and Andrew Cur*.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Ngano za Wachuka kutoka kwa Watambaji

### HADITHI YA KWANZA

*Mbiti na kabare ciatumire urata cierana niciuge itema, ciauga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko. Thoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na Mbiti.Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria Kabare gatuire.*

*Riu, Mbiti yathii yatua baria kabare gatuire ri, kabare gakithii kathiite gutua ri, gakiona Mbiti itatua kwayo, itwire gwako. Riu kabare gakithii gakiuria Mbiti," Mbiti' nuntu ni gweu urigirie ri, nuwonire uria untwirire nthoroko?" "Aari, aari cianjeru cianjeru ntageria kwona, ari ntamwona ntamwona.*

*Wa ntuku, Kabare kathii gagatua, Mbiti ikauma thuba ikathii igatua. Kwa Mbiti gutigutwiwa. Mbiti nitua gwa Kabare, Kabare nako nigatua gwa kabare, gwatwika riu cia mbiti itigukomwa, na tintue.*

*Riu wa ntuku kabare gakithii mbele gagitua. Mbiti ikiuma thuuba. Magitungana. mbiti ikithii, igitua. Kabare ntuku ingi kakithii kethiria kethiria nthoroko ciako iri bakubi guthira, kamiuria "mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga n ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?"*

*Aari aari ntamwona. Ntamwona, ntamwona." Amwira," riu, nitutue kiatho na auke. Withiranie mbiti cionthe nan mbithiranie tubare tuunthe. Tuthi muburoni witagwa Ginci kiiru. Tuthii tutube. Uria ukagwa ku, niwe ukamenyeka niwe wiaga nhtoroko cia uria wingi."*

*Mbiti yera Kabare, "nibu." Cierana bu, riu ntuku inu yakinya. Tubare na mbiti cia tirimana Ginci kiiru ciathii riu, riu cierana, "riu ni kwina ii kenda muntu atuba." Riu ciaina:*

> *"ntarumaa ntarumaa muthoroko."*
> *Kabare kaina;*
> *Ntarumaa x2*
> *muthoroko x2*
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

*Kabare gatuba gakinya rugongo ruria Mbiti nayo yerwa niine. yaina:*

> *Ntarumaax2*
> *muthorokox2*
> *wa muru wa kabare Ginci kiiru ntwara*

*Mbiti yagamba runcini butu! Yauga, "Ruutana ndutani ii, gantatubite wege*

*Mbiti cietikira ciaruta Mbiti. Aya! yarutwa ri, Kabare kerwa, "ruuga ringi riu nuntu mbiti yauga nika itarugite weega, iruge weega." Kaina;*

> *Ntarumaa x2*
> *Muthororoko x2*
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwaara.*
> *Kabare ri, karuga gakinya rugongo ruria.*

*Mbiti yambiria gutantaura;*

> *Ntauma x2*
> *muthooko x2*
> *wa muu wa kabare Giinci kiiru ntwara*

*Yagamba runcini nku! Yerwa riu mbiti i cingi,*

*"Ai nee riu ni weu wiite." Yauga ari rutaana ndutani ii gantatubite weega ri,tingwa ku."*
*Mbiti yarutwa ria kairi. Kabare kauga, "gantube ria kathatu." Kenda kauma rugongo ruria gakinya rugongo ruria. Kaina:*

*Ntaruma x2*
*muthorokox2*
*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

*Kabare gatuba gakinya naa rugongo ruru rungi. Mbiti yambiriria riu;*

*Ntauma x2*
*Muthooko x2*
*wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwara*

*Mbiti yagamba runcini ringi nku! Yagwa runcini. Yambiria gukiriria tuguru, "Ndutani rutaani ntantubite wega. Ti niu. Ti niu. Ti niu. Ndutani ntatubite weega."*
*Mbiti ri, yerwa yerwa ni mbiti i cingi atiri, "tutikuruta ni weu wiaga kabare. Mbiti ikinatwarwa ni runci.*
*Rugono na ntai.*

## TAFSIRI YA HADITHI YA KWANZA
## HADITHI YA FISI NA KINDI

Fisi na Kindi walikuwa marafiki. Wakakubaliana wapalilie konde wapande mbaazi. Wakapanda mbaazi. Mbaazi zilipokomaa, kindi akawa akienda kuchuma zake. Kila akirejelea alikutana na fisi.

Fisi naye alizoea kuchuma mbaazi palepale alipochuma kindi. Kindi alipoelekea kuchuma tena, akagundua kuwa fisi hakuchuma kwake bali katika shamba la kindi.

Kindi akaenda akamuuliza fisi, "fisi, maadamu ni wewe ulienda shambani mwisho, ulimwona aliyechuma mbaazi zangu?" "La! La! Cheupe cheupe, sikumwona."

Kila siku, kindi alipochuma mbaazi zake, fisi akamfuata, naye akazichuma. Kwa fisi mbaazi hazikuchumwa; ni kwa kindi tu za fisi hazikuguswa kamwe Hazikuchumwa.

Ikawa mazoea. Kila kindi alichuma, fisi naye akamfuata, akachuma. Siku moja wakakutana Fisi akaenda akachuma.

Kindi alipoelekea kwake siku nyingine, akagundua mbaazi zake zi karibu kwisha. Akamuuliza, "Fisi eti huwa unaniambia huwa humwoni mtu ambaye huiba kwangu n ani wewe tu huwa nakutana nawe? Hujawahi kumwona mtu akizichuma hizi mbaazi zangu ambazo zaelekea kuisha?"

"La! La! La! Sijamwona. Sijamwona. Sijamwona." Akamwambia, "Sasa, tupange miadi ya kesho kutwa uwalete Pamoja Fisi wote, nami niwalete kindi wote. Twende katika mto wa Ginci kiiri. Twende turuke. Yule atakayeanguka majini ndiye mwizi aibaye mbaazi za mwenziwe." Fisi akamwa mbia kindi, "sawa."

Wakakubaliana. Siku hiyo ikafika. Kindi na Fisi wakakutana Ginci kiiru. Wakaafikiana waimbe ili kila mmoja aruke mto ule. Wakaimba:

sikula x2
mbaazi x2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nisombe

Kindi akaimba,

sikula x2
mbaazi x2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nisombe

Kindi akachupa akafika ng'ambo ya pili. Fisi naye akaambiwa aimbe.

Akaimba:

Sikua x2
mbaazi x2
Za ndugu kindi Ginci kiiru nsombe

Fisi akaanguka majini chubwi! Akasema, “Tafadhali niondoeni. Sikuruka vizuri.” Fisi wengine wakakubaliana wakamnyanyua. Alipotolewa, Kindi akaambiwa aruke tena kwa vile fisi alikuwa amedai hakuwa ameruka vyema, ili aruke vizuri.

Kindi akaimba:

Sikula x2
mbaazi x2
Za ndugu fisi Ginci kiiru nsombe

Kindi akaruka akafika upande wa pili.

Fisi akaanza kugugumiza:

Sikuax2
mbazix2
Za ndugu kindi Ginci kiiru nombe

Akaanguka majini tena, chubwi!

Fisi wengine wakamwambia, “Hivi ni wewe mwizi wa mbaazi,” Akasema, “Hapana.Tafadhli nitoeni sikuruka vizuri. Nikichupa vizuri, sitaanguka mtoni.”

Fisi akatolewa mara ya pili, kindi akasema, “Ebu niruke mara ya tatu.” Ili atoke ng’ambo ile afike upande huo wa kwao.

Kindi akaimba akiwa ng’ambo ile:

Sikulax2
mbaazix2
Za ndugu Fisi Ginci kiiru nsombe

Kindi akarupa akafika upande mwingine

Fisi naye akaanza:

Sikuax2
mbaazix2
Za ndugu fisi Ginci kiiru nsombe

Fisi akakaanguka tena mtoni chubwi!

Alipoanguka majini akaanza kuinua miguu, “Nitoeni tafadhali. Sikuruka vyema.” Fisi wengine wakamwambia Fisi, “Hatutakutoa. Ni wewe huiba mbaazi za kindi.”

Fisi akasombwa na maji.

Hadithi inakamilika hapo.

## HADITHI YA PILI
## NGONGOANA NA GACINCI

*Kwari na Ngongoana na Gacinci. Muntu na muru wa ng’ina. Aciari mao makua. Indi, maari ma ikamba. Matigwa mari mairi.*

*Riu nyimbo cia tene nuntu niciainagwa, Gacinci akera ngongoana, “kanthii rwimbo.” Akamukania akamwira, “tiga kuthii, nkaliwa ni malimalimu,” nuntu kwari na marimarimu. Akegua akerega kuthii.*

*Atua kumwiraga bi wa rionthe akigucaga. Ntuku i ingi rwainwa bakubi muno.Amwira, “Ari nee , gankegue baba ii ngakuthikagiriria ii nkegucaga irimarimu rikigita atia?rigiigica.”*

*Athii. Athii. Akinya rwimboni. Irimarimo nario riari wa baba rurini rikinathungira. Riamwita, “Ngongoana,” arira, “wuu,” “Nkundia iia.” Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria.*

*Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria.Riu rikinamwira atiri , "Ngongoana, nkundia ingi."Amwira, " niriathira."Amwira , "Ngua. Ngua ta ngu, nwa riu ngakugia. Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikulibota. Arikua akigucaga atikulibota.*

*Athii akiriraga. Athii akiriraga, mainaga, "Njira ya mugumo"nawe riu akamwila, "Ngongoanga , ndwaa njia ya mumbu, ndungandwae njia ya mugumo." Akamwira, " nibu."*

*Akamwira, "Ngua nwa niu ngakugia. Ndaa njia ya mumbu ndugandwae njia ya mugumo.nwa niu ngakugia." Mathii mathii mathii. Ngongoanga akiligala muno. Akiinaga:*

*(Gacinci ii Gacinci mwile ndagukanilie wathi*
*Wa utuku Gacinci mwile) x3*

*Akamwila, "Ngongoanga ii ndwaa njia ya mumbu, ndugandwae njia ya mugumo."*
*Rikaina: Gacinci ii Gacinci mwile*
*Ndagukanirie wathii wa utuku*
*Gacinci mwile*

*Gacinci akinegua mwang'ina akina. Akinela antu, "Takirani mbigueni." Egua,*
*Gacinci ii Gacinci mwile*
*Ndagukanirie wathi wa utuku*
*Gacinci mwile*

*Akimera, "riu ncuni ii, mumbile nuntu riu ni irimarimu rikuthinia mwana wetu," Makiria rwimbo muruang'ina aca arumirirwa ni antu mau maingi. Magikinya methiriria ni irimarimu rikuitwe ni mwang'ina akiriraga.*

*Mauga, "unu ukuite niakinye nthi." Irimarimu riauma. Riambilia kurathwa na migwi, kumutangwa na matumo, riakua. Riakua nirio Gacinci menukile na mwang'ina. Rogono rukinathira.*

## TAFSIRI YA HADITHI YA PILI
## HADITHI YA NGONGOANA NA GACINCI

Paliondoka Ngongoanga na Nduguye Gacinci kutoka ukambani, wazazi wao wakaaga dunia wakabaki wawili tu.

Kwa sababu nyimbo za zamani zilikuwa zikiimbwa, Gacinci akamwambia Ngongoana, "Ebu niende kwenye wimbo." Akamkanya. Akamwamwabia, "Usiende. Nitaliwa na mzimwi." Kwa kuwa mazimwi yalikuepo. Akasikia akakosa kwenda.

Akawa akimwambia ivo kila wakati akisikiliza. Siku nyingine, wimbo ukaimbwa karibu na pua na mdomo .Akamwambia, "Ebu nikasikilize apa .Nitakuwa macho zimwi likija."

Akaenda akafika kwenye wimbo. Zimwi lililokuwa karibu na lango likaingia. Likamwita, "Ngongoanga," akaitika, "wuu." "Nipe maziwa." Akalipatia maziwa kwenye dundu likatisa, likanywa yote. Likamwambia, "Nipe mengine." Likapewa maziwa mengine likanywa yakaisha. Likamwambia tena, "Ngongoanga, nipe mengine." Akaliambia yameisha."

Likamwambia, "Nibebe kama kuni ni mle nitakula." Ngongoanga akachukua Kamba akalifunga zimwi huku akiwa haliwezi. Akalibeba kwa kujitahidi. Akaenda akilia. Walienda wakiimba kuhusu njia ya mugumo

Nalo zimwi likamwambia, "Ngongoanga, nipeleke njia ya mumbu, usinipeleke ya mugumo." Akakubali. Likamwambia, "Nibebe ni mie nitakula. Nipeleke njia ya mumbu, usipeleke ya mugumo.

Wakaenda.Wakaenda. Wakaenda. Naye Ngongoanga alikuwa akilia sana. Aliimba:

(Gacinci ii Gacinci mwambie

Nlikuonya nyaimbo za usiku
Gacinci mwambie) x3

Likamwambia, "Ngongoanga, nipeleke njia ya mumbu usinipeleke njia ya magumo."

Likaimba: Gacinci Gacinci mwambie
Nilikukanya nyimbo za usiku
Gacinci mwambie

Gacinci akasikia dada ake akiimba akaambia watu, "Ebu nyamazeni nisikie." Akasikia:

Gacinci Gacinci mwambie
Nilikukanya nyimbo za usiku
Gacinci mwambie

Akawaambia, "Sasa njooni mnipeleke kwa kuwa hilo ni zimwi linalomsumbua msichana wetu." Wimbo ukatulia. kakake akaja akifuatwa na hao watu wengine.

Walipofika wakapata zimwi lilikuwa limebebwa na dadake akilia. Wakase, "Huyo aliyebebwa akanyange chini." Zimwi likashuka likashambuliwa kwa mishale na kuchomwa kwa mikuki, likafa.

Lilipokufa, Gacinci na dadake wakarejelea nyumbani

Hadidhi imekamilika hapo

## HADITHI YA TATU
## AIRITU MANA MA IKAMBA

*Airitu mana ma Ikamba meerwa ni magacawe njarumi. Mathii gucawa magego. Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii, u ukaringia munyiri rugongo ruria atuike niwe ena njarumi I mbega. Na ururia akaguithia runciini atuike njarumi yawe ti mbega tucoke tugacawe riingi."*

*Mathii riu macawa maca riu mathii muburoni uria meranite, makinmbiriria gutua munyiri. Mau monthe matua matua airitu mathatu ukigwicaga runcini. Muiritu umwe wetagwa Mweru, agera wawe wakinya rugongo ruuria.*

*Meerana, "Riu, nwatuthiire gucawa riingi ii, tutiumba gucindwa ni muntu umwe." Macoka ringi gucawa, mathii macawa riingi. Mweru we atacawa riingi nuntu we niamacindite. Maca riu merana "Riu ni gutua ringi". Mambiriria kugera munyiri ringi. Magera magera magera matikubetukia nwaka makugwithia runcini mari mathatu ringi. Mweru atua aringia ringi.*

*Mathii mathii merana "Tuthii na tutikuria gucawa ringi". Mathii kuri antu monete irima iraca munomuntu arikibingirwa ku akaurira ku. Mathii ri, mathiuba mbele ya mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku, na twekira mweru ku agakuira kuu. Na twinukange na karugi muno, twathii tuge atiri, nuntu kwina mbiti, twaurua tuge nimbuga karirwe ni mbiti nuntu niwe enukire mbele yetu".*

*MAkinerana, "nitumuthairirie ii, turume mukanda, twaruma mukanda, muntu athgungira akaburutwa ni antu mathatu akauma. Indi muntu wa cietu ambe athungire ari wa mbele, kenda mweru akarigia akiugaga akarutwa turege kumuruta."*

*Mabanga ugu. Matgungira ria mbele makirutanaga makirutanaga makirutanaga. Marutana monthe kinya ona mweru maruta. Macekera ria kairi. Mathii mathatu akirutagwa Mweru arigia. Arigia ri, akiinamia mukanda arutwa ri, akunikirwa na ibari (ibiga)*

*Mweru atigwa kuu, atuura ku. Atuura ku ri, makinya mucii, maurua mauga "Mweru niwe winukire mbele yetu ii, nwakigua atunganire na mbiti ariwa" nuntu mbiti ciari ku*

*nkinya muthenya. Ingi aciari mamenya unu mwana ka arikire agite kwirukira ma mangi.*

*Riu mekara ugu maici Mweru ni wakwire. Kwari na muruagina Mweru wetagwa Nyaga. Myaga ri, ni gakurithia, Gatuura Nyaga karithagia karithagia karithagia, Wagakirithagia wogu, Nyaga ri, kathuura muno ni mburi kamiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*

*Nawe kaana karia gekaririte ibaari riri, gatikumenya kana ni ibiga rikunikanie. Gekarite o baria Mweru ari. Mweru egua akinaina:*

> *Nkanga ii nkanga cia Maindi*
> *Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
> *Wana riu nwa tutwire*
> *Nkanga cia maindi*
> *NItwarire nguo cia mwili*
> *Nkanga cia Maindi*
> *Tukinora mugwanja umwe*
> *Nkanga cia Maindi.*

*Nyaga abnga "ari kambire mburi iria bu ringi"*
*Amiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*
*Akinegua:*

> *Nkanga ii nkanga cia Maindi*
> *Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
> *Wana riu nwa tutwire*
> *Nkanga cia maindi*
> *NItwarire nguo cia mwili*
> *Nkanga cia Maindi*
> *Tukinora mugwanja umwe*
> *Nkanga cia Maindi.*

*Kana karia ri, kabanga ni kwinukia mburi. Kathii kera ng'ina, Umenye, Mweru ari bo ii?"*

*Ng'ina akaringa na mwiko "niuu ucite kuririkania kiriro ki naririre ngica gugakira?" Kathii kiri ithe, ithe akaringa na muthambicho. Nyaga ri kathi gakiriraga wa gwa icue. Kathh kamwita, "cucu" etika amwira "Umenye, umenye Mweru ari bo ii? Tiga ugu twiragwa niarirwe ii? Ari kuu nthi, mbikarire ibiga negwa akina kuu nthi maita megana? Mairi cucu, Indi nkiira aciari makwa mambiriria kundumia. Riu ni tuma nkurira. Era "guti na thiina ii, ni niu nkameera."*

*Maca maca mauria, "Ntikumuria, ai mwaburira nyaga ki?"" Agitwira* nteto cia *nkoma. Agitwira Mweru ari bon a ni uria wakwire." Ni ithe akuragia riu. Athii kiri Ngina amuria bu. Ngiina amucokeria wa bu. Amuria, "Niaturirikania kiriiro gi twaririre twakira; agica gutwira Mweru ari bo, Mweru u wakwire wa tene?"*

*Icue akinamera "Taciani nimwireni, ruyu ruyu ruyu, mwithiranie antu ma mena binyama gutegatekia ibari riu negua nirio akunikiritwe nario. Nuntu Nyaga tiika atikumenya baria ibari ririkunikire na niwe urithagia. Athii atwonie, indi untu tukathii, nuntu mwana unu niaina akauga niathiritie nguo, urume anwa rucuka kana nguo yaku ukamwikirira ii? Na ukie gakie wikire katheguni na uthii na gakuniko ga gukuniika nag a kumukundia nako. Nuntu mwana unu, ari bo ugu nyaga ambira. Tigani kuukagia untu na karugi ugu. Mwana, atirigwa ni untu. Na mwana niwe uririkanaga."*

*Merana, "nibu tukathii kirauko."*

*Ng'ina auga, "ana ngakia tene muno. Wegua nibu ri, tukathii na ngaceria antu. Antu matiura.*
*Riu mabanga ugu na icue. Riu Nyaga ana ataringwa ringi. Akumama cacawa. Gwakia kirauko erwa "Nyag tuthiiugu uraugire kenda umwigua akiaria" Maukira tene mathii. Mathii makinya nabo, nau Nyaga arithagia, Nyaga athii ekarira ibiga riria. Antu mati au? MAthikiritie muno megua kana ka Nyaga amabenagia Nyaga auga "Tui Mburi iria uroura ukaura ta Mweru wetu uria waurire."*
*Makithikiriria bu makwaragianteto megua:*

*Nkanga ii nkanga cia Maindi*
*Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
*Wana riu nwa tutwire*
*Nkanga cia maindi*
*NItwarire nguo cia mwili*
*Nkanga cia Maindi*
*Tukinora mugwanja umwe*
*Nkanga cia Maindi.*

*Antu kugaa na kwigua ugu, makunura ibari mari na mikanda iri. Muntu umwe athungirua kun a mukanda, obereretwe mbaru. Athii, oberera Mweru, anenkererwa erwa "riu twitithirie we."*
*Ambiriria kumurutha weega, ameera "Nkumuthaika weega muruteni riu,"*
*Mweru arutwa akinya nthi nawe ekirwa mukanda nawe athaikwa arutwa. Ibari riakunikwa wa buria ingi bari bakunike. Akunika, Magicua mweru, Mweru orete mwena umwe uuthe. Aana ekarire ta Karigi ni Kubuuta. Mweru ameera "Niu ndiicaga Muthetu. Ana nguo ninarire. Riu on ninatigaritie gukua cua ninorire mwena umwe."*
*"Natia gwekarire?" Amera, "Ui, twathiire gucawa magego, natwika ni niu nkubetukiamuburo munyiri, riu mankinankunikira guku ntikumenya na tweranagatuthungire wa muntu akarutwa. Niu mankunikira ria mwico. Nkinatuura guku nuntu riu nimathurire muno ni niu."*
*"Guti na thina. Matwirire kawarirwe ni mbiti natwi twetikia." Riu Ng'ina amwoba rucuka nathiite naru. Ekara nti kaboora amukundia gacuru agatabika, Wakundua agatabika. Atabika Muthetu, atabika Muthetu. Nuntu indi ya tene antu nimekagira ciuma, atabika ciuma, atabika maguo, atabika nkuruki. Wa akinyunyaga wa akinyunyaga wa akinyunyaga. Ri atigire gutabika ri, mamenya riu into ikuthira mwili. Mamenya riu kamakwinuka na mwana wao makinenuka.*
*Menuka, mathii, ithe auga riu gakuthinja nturume, mwana unu ebakage maguta nau barware na akiagirwe wa rionthe ni kenda abota kubua.*
*Ambiriria gutumbirua, abua. abua bururu. Anambiriria riu kugendaga. Riu airitu maria mathatu makinegua Mweru ri, niarabwire. Niaronire wa kumuruta kuu irimani. Makinandika kamakamukethie. Mathii Kumukethia ntuku ya mbele, Mweru amamukiira wega muno na nkinya amakundia iria manunyanira weega muno. Riu ri, amakinyia menuka. Akinamatwira kiatho na auke. "Muce na nkegua nimukuirite ii, wana iria ni mukethira riri bo." Amera "nibe tugaca gugukethia Mweru."*
*Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urembo.*
*Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugag makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe. Rugano rukinathira.*

## TAFSIRI YA HADITHI YA TATU
## HADITHI YA WASICHANA WANNE WA UKAMBANI

Wasichana wane kutoka Ukambani waliambiwa wangechongwa meno kuyatia mwanya wa Urembo. Wakaenda Kuchongwa Meno. Baada ya shuguli hiyo kukamilika, waliambiana “Twendeni mtoni tuone nani ataweza kutema maji kupitia kwa mwanya wa meno hadi ng’ambo ya pili. Atakayefanya hivyo ndiye atakayesemekana kuwa na mwanya mzuri zaidi. Atakayeshindwa kufanya hivyo, asemekane kuwa na mwanya duni, hivyo arudi akachongwe tena.”

Walielekea katika ule mto waliokuwa wameafikiana wakaanza kushindana kuvusha mchirizi kwenye mto. Wasichana watatu wakajaribu ila hawakuvusha. Msichana mmoja aliyeitwa Mweru ndiye aliyeweza kuvusha had upande wa pili wa mto huo. Hao watatu wakasema “Lazima turudi kuchongwa tena. Hatuwezi kushindwa na mtu mmoja.

Wakarudi na kuchongwa tena. Mweru hakuchongwa tena kwa kuwa alikuwa amewashinda. Wakaenda mtoni na kuanza kushindana tena. Wote watatu wakashindwa tena. Mweru akafanikiwa.

Wakaambiana, “Twendeni tufunue shimo kwa kuondosha lile jiwe tumrushe Mweru ndani. Na tukimtia mle, atafia humo. Kisha turejee nyumbani haraka sana. Tukiulizwa kuhusu habari yake, tuseme alitangulia na huenda alililiwa na fisi.”

Wakasemezana, “Tumdanganye. Tuchukue Kamba. Mtu mmoja akiingia, anavutwa na wale watatu anatoka. Mmoja wetu atangulie ili Mweru aingie akiwa wa mwisho. Halafu tukatae kumwondoa mle. Wakapanga hivyo.

Wakaingia kwa awamu ya kwanza kila mtu akiviutwa na kutoka. Hata Mweru akatolewa. Wakarudia mara ya pili. Wa kwanza watatu wakatolewa. Mwerru akaingia wa mwisho. Akatikisha Kamba wamwondoe lakini wakamfunikia mle ndani kwa jiwe kubwa. Akabaki humo. Akakaa mle,

Wali[pofika nyumbani, wakaulizwa aliko Mweru wakasema “Mweru ndiye alitangulia kuelekea nyumbani. Huenda alikutana na fisi akaliwa.”

Zama hizo kulikuwako na fisi wengi. Wazazi wakasadiki kuwa huyo mtoto aliliwa na fisi kwa vile aliamua kuacha wenzake akatembea peke yake. Wakaishi wakijua kuwa Mweru alifariki. Mweru alikuwa na kakake aliyefahamika kama Nyaga. Alikuwa akichunga mifugo malishoni. Siku moja akiwa anawachunga mifugo, mbuzi mmoja akamkasirisha mno. Akamwambia, “ewe mbuzi potelea pote kama yule Mweru wetu aliyetokomea toko!” Kijana huyu alikuwa amekalia jiwe pasi kung’amua kuwa chini ya jiwe hilo palikuwa na shimo. Humo ndimo alimokuwa Mweu. Akasikia Nyaga akimfokea mbuzi yule.

Mweru akaimba:

> Kanga I Kanga wa mifupa
> Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
> Hata sasa tunaishi,
> Kanga wa mifupa.
> Tulikula nguo za mwili,
> Kanga wa mifupa.
> Tukanona pande mmoja,
> Kanga wa mifupa.

Nyaga akaamua, “Ebu nimwambie mbuzi yule hivyo tena.” Akamwambia, “Ewe mbuzi potelea pote kama yule Mweru wetu aliyetokomea toko!”

Akasikia:

> Kanga I Kanga wa mifupa
> Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,

Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Yule kijana akaamua kuwarejesha mbuzi nyumbani. Alipofika, akamwambia mama yake, "Wajua Mweru angalipo." Mama akampiga kwa mwiko. Akamwuliza "Kwa nini unanitonesha kidonda?"

Akaenda alipokuwa babake. Baba mtu akampiga kwa mpini. Akaenda huku akilia. Akafika kwa babu yake. Akamwita, "Babu,"akaitikia. Akamwambia, "wajua, Mweru angalipo, Japo huwa tunaambiwa kuwa aliliwa. Yumo humo chini. Nilikalia jiwe nikaskia akiimba huko chini. Aliimba mara mbili babu. Nilipowaambia wazazi wangu wakaanza kunipiga. Ndiyo maana ninalia."

Babu akamwambia, "Hakuna tashwishi. Binafsi nitamwambia," Wakaenda hadi nyumbani. Babu akawauliza, "Eti mmemwadhibu Nyaga kwa nini?" "Ametwambia mambo ya kishetani; eti Mweru angalipo hali twajua vyema kuwa alikufa." Baba akajibu. Mama yake alipoulizwa, alijibu, "anatutonesha kidonda kwa kutuambia kuwa Mweru angali hai nasi tunajua kuwa aliaga dunia kitambo."

Babu akawaambia, "Ebu niwaambieni, kesho, tafuteni watu wenye nguvu wa kusongeza jiwe hilo nililoskia Mweru amefunikiwa nalo. Nyaga anafahamu lilipofunikwa shimo. Yeye ndiye hupeleka mifugo malishoni. Aende atuonyeshe. Mtoto huyu anaimba akisema kuwa nguo zimemwishia, Beba angalau nguo ya kumvisha. Saga uji utie katika dundu. Beba kizibo cha kumnywesha uji nacho, Maadamu Mweu angalipo kama alivyoniambia huyu kijana. Mtoto ndiye ajuaye, ndiye akumbukaye. Wakakubaliana kuwa wangeenda asubuhi.

Mama akasema, "Nitasaga uji mapema mno. Nitawatafuta watu. Watapatikana."

Wakakubaliana hivyo. Nyaga hakupigwa tena. Alilala vizuri. Kulipopambazuka, Nyaga akaambiwa, "Utaenda useme hivyo ulivyosema ili tumsikie Mweru akizungumza." Wakaamka mapema na kusanzuka. Wakafika Malishoni Nyaga akakalia jiwe lile. Watu wakatega masikio yao nchi! Nyaga akasema, Ewe mbuzi potrelea pote kama yule mweru wetu aliyetokomea toko!"

Wakasikia: Kanga I Kanga wa mifupa
Gacirici Nyaga wetu kanga wa mifupa,
Hata sasa tunaishi,
Kanga wa mifupa.
Tulikula nguo za mwili,
Kanga wa mifupa.
Tukanona pande mmoja,
Kanga wa mifupa.

Watu wale waliposikia hivyo, wakaondosha jiwe. Walikuwa na Kamba mbili. Mtu mmoja akaingia humo na Kamba moja. Akamfunga Mweru huku naye amefungwa kifuani. Baada ya kumtayarisha vizuri, aliwaambia, "Tayari nimemfunga vizuri. Mvuteni sasa."

Mweu akavutwa akafika nje. Yule mtu aliyekuwa ndani naye akavutwa akatoka. Jiwe nalo likarejeshwa pale lilipokuwa. Mweru alikuwa ameoza upande mmoja. Alikuwa amekonda kama sindano kwa sababu ya njaa. Akawaambia, "mim hula mchanga. Hata nguo nilizokuwa nimezivalia nilizila. Nilikuwa nachungulia kaburi. Angalieni hata nishaoza upande mmoja.

"Nini kilichotokea?" Akawaambia, "Tulienda kuchongwa meno, mien a wenzangu. Nikawapiku katika kuvusha mchirizi pale mtoni. Wakanifungia huku bila kutarajia. Tulikuwa tumeafikiana kuwa kila mmoja angeondolewa humu kwa awamu ila wakanihadhaa na kunifungia humo. Walikasirika sana nilipowashinda. Nimekuwa humo tangu siku hiyo."

"Si kitu, Walitwambia kuwa uliliwa na fisi nasi tukakubali." Mama yake akamfunga kwa kanga aliyoibeba. Akaketi taratibu. Akamnywisha uji akatapika. Kila alipopiga tugu la uji akatapika mchanga, nguo na shanga za nakshi alizokuwa amemeza. Akaendelea kunywa. Alipoacha kutapika wakajua kuwa vyote alivyokuwa amevimeza vishatoka. Wakaamua kurejelea nyumbani na mwanao.

Walipofika nyumbani, nbabake Mweru akasema kuwa angemchinjia kondoo wa kiume. Mwanawe angejipaka mafuta ya kondoo huko alikougua. Awe pia akisagiwa uji kila leo ili awezw kupata shufaa. Akaanza kulishwa vizuri. Akashugulikiwa hadi akaponakabisa. Akaanza kutembea vizuri. Wale wasichana watatu wakasikia habari za mweru kwamba alipata nafuu kabisa baada ya kuokolewa kutoka mle walimomtttumbukiza. Wakaamua kumtembelea wamjulishe hali. Wakaenda kumsabahi siku ya kwanza. Mwertu akwapokelea vizuri sana. Akawapa maziwa wakanywa pamoja.

Mweru akawasindikiza warejee makwao. Akawakaribisha tena kwa mwaliko wa siku mbili ambazo zingefuata. Akawaambia, "Karibuni, Nitawaandalia maziwa na uji wa kusagwa." Nao wakasema, "Tutakuja tukusalimie Mweru," Mweru alikuwa amekasirika. Alitaka kulipiza kisasi kwa kuwaliga.

Akabaki. Akatafuta rojorojo ya kutengeneza gundi ya kuwanasa ndege kutoka kwenye miti ya kila nui. Angeitia rojorojo hiyo kwenye maziwa ambayo angewapa. Siku ikafika. Wakaja Mweru akawapokelea tena. Akawapa maziwa yenye rojorojo sumu naye akayanywa yale salama wasijue. Wakanywa. Baadaye akawaambia, "Twendeni niwasindikize." Akawasindikiza. Walipofika njiani, wote wakageukan kuwa vipepeo isipokuwa Mweru.

Hadithi imeishia hapo.

## HADITHI YA NNE
## KAURA NA NYAGA

*Nyamu cionthe ni ciatirimanite bamwe. Cierana wa nyamu ice na tuku. Nyamu ciothe ciakua nku, riu, nako kaura gakinauna tuku twa miboru. kathii nabo. Kathii ri, mathinja. Mathinja matwika nyamu ino nikaigwokia nyama. Ciokia nyama gwokia gwokia gwokia. Ciokia ciambiria kuria.*

*Riu kaura gakinamenererua ni nyamu cionthe gakinaurwa, "Nee kaura muntu ati matina ubirite nku cia miboru ku? Ana nyama cietu tutikurumia." Kaura kauga ambikare aa nkoona." Kaura gekara bo. Nyamu ciokia nyama ciambiriria kuria. Ciaria cionthe, ciabaa ciambiria kumuntira mitini. Nibu ibairwe riu niiremirwe.*

*Kaura nako ri, gatikurumwa. Nikerwa, "Kaura muntu ati matina ucite aa kurutha atia bo?" Kaura kathura gaciuria, "Tauntu mukumbira ugu, mukanyua runci mwaruta ku?" "Tukanyua muburoni" "Indabwethia?" "Gukabwethia miburo yonthe?" "ii" Niu nindi mbwethie runci, namwi timwona gia kunyua. Mone kana nyama inu cienu ikamutethia mutinywite runci."*

*Nyamu iria ciambiriria kuthekera kaura igikeraga, "Ana ukabwethia utibwethia yonthe, tukanyua runci, runci tukanyua. Gutibu ubota kubwethia miburo yonthe. Thii ubwethie ni."*

*Kaura kauma au kathurite mono nuntu wabu gakwimwa nyama ti mathe, kathii gakibwethagia miburo Kabwethia kabwethia kabwethia, miburo yathira. Gakinatigaria umwe win a tunci tunini muno nuntu ni twa mutonto.*

*Nyamu ciathire miburoni yonthe cierana runci rwaura.Nacio inontire unanimaligwa nimalicaga nyama ciaki nuntu mbiti inontire niciigua taka ingikua. Ciathi ciathi ciethiriria mutonto. Ciathigia kunyua mtonto ri, ti gitaka. Gitikunywika.*

*Wa mbiti imwe yaaciira, "Untu tukwona baba nibo kaura kari. Nitugakaire muno i, tukarumie nyama i, nitugukua ni inonta."Riu ciambiriria guitana, kaura kaura," Kaura kaumira "Bai titukwima nyama ringi ii, tukwenda gukua wa bu utwirire ii, tukundie runci i, natwi ri tukurumie nyama.Nuntu nituthigia kunywa tukona ni mutonto."*

*Nyamu yetagwa nyaga yauga, "Niu runci rwa kaura, ntirukunda.Na nyama ciakwa ntirumia kaura".Nyamu iria cingi cionthe ciambiria kurumia kaura. Kaura karia kegua nikaremirwe ni kuria nuntu nikarumwa ni nyamu cionthe indi nyaga niregire.*

*Nyaga yakairwa ni nyamu inu ciingi yerwa, "Nyaga, i rumia kaura nyama nugukua ni inonta." "U? Niu ntikunda runci rukuthambwa ni kaura na nthonjo ikiangaga ku. Ntirukunda na ntirukunda.Nani, ana mwarutirwa nyinci ni mwiu mukanyua niu ntinyua indi,ntilukunda na ntikalumia nyama niu ntikarumia."*

*Kaura nako kamenya negwe warukunda, ningukwonia.Ai! Nyaga kithimilite ikunda runci icioke imane nyama.Riria Nyaga yaculithililie yoona taka Kaura gatimicuite ri,yakuamiriria igikunda runci ugu,Kaura karuma ibiga kamiringa rugoci rukinaguuka.Nyaga yacioka yaciokia rugoci rwao ringi.Ai!ikinathuura ikinenuka. Ikinakeera, " Negwe kaura woona ni kitheru kiu giakwa wakura , ugakileta na nkuniko mugwaanja cia maguta ma mbariki."Kaura gatigwa nako ri, gakurumwa ni Nyaga.Gatigwa runcini nuntu nigekaraga runcini ri, twana twa kaura twambiriria gukua.*

*Kaura nako kambiriria kwimba maguru. Kaura kamenya nkugwatwa ni kirumi kia Nyaga kauga, "riu ninthii nkiuragiriria kwa Nyaga na nina nkuniko mugwanja cia maguta ma mbariki."*

*Kathii gatema tumiti twa miariki nuntu turi karima. Gagikagira maguta ma mbariki ku,twakinya mugwanja.Kamuntithania kamuntithania kamuntithania kathii tang'u! tang'u! tang'u! kathii gakinya guntu nau gatunga wegua ni mbiti,gakaina ,*

> *"muthurithuri muthunthuiga, kwa Nyaga ninaku muthunthuiga. mbile mbu ya Nyaga muthunthuiga.Ciana cianathira muthunthuiga ni rwagi na mbebo muthunthuiga."*

*Mbiti igikeera, "nukwona rugongo ruuria, niku kwa Nyag7]7]." Kaura gakiambiririria kuthii ringi. Gakithie gagitungana na tuthuni. "Muthunthuri……."*

*Kaura niko kau. Kathii Kathii kathii gakinya bantu kethiriria mbiti kairi.Kaina muthunthuri….."*

*Keerwa, "kwa Nyaga ni baaria." Kathii.Gakinya kwa Nyaga.Nyaga yari kuu nyomba. Kaura kaina, "munthunthuri….."*

*Nyaga yakirira kaura yauga itikambukura, nuntu nako nikamithukirie. Nyaga yekara ikirite. Kaura kauria, "nuntu mbirirwe aa nibo kwa Nyaga ii,tika Nyaga igunkirira?" Gankairirie mine kairi."*

*Kaura kaina, "muthunthuri…….?"Nyaga yauma.Yamuria, "ni indu ucirite gwakwa anga tutabitanirie?"Amwira, "Ari ii,nika ndauga nkubuce ii twikanirie mata."*

*Amuria, "Anga tutabitanirie?" Amwira, "Ari ii, ana antu mabitania nimaciokaga makabitanukia." "Riu Nyaga ri, nitubitanukie."Amuria, "tukibitanukia negwe ri,nkuniko iria nakwirire mugwanja winacio?" "ii ino" "ooh! Ari riu nkwigua tukabitanukia. Amwira, "riu ri takura rugoci ruru."kaura gakuura.kerwa, " igirira nthi."kaigirira nthi.kerwa, "ikira nkuniko imwe ," gekira. Kiginyo kiauma. "ikira inu ingi."kiginyo kiauma. "ikira inu ingi." kiginyu kiauma. "ikira inu ingi." kiginyu kiauma*

*Kaura gekira nkuniko mugwanja.ya mugwanja ikithira ugu ,kiginyu kia mwico kiauma.Nyaga ikinabora. Riu akinamwira , "riu ri tukugwatanira ciokia kithegu giakwa."*

*Yaciokia. Merana, "ii tu! Tu! Tu! wa twana twaku, ukithii utwithire bo. Nuntu onani nkubua."Nako kaura gakinamira, "i tu! tu! tu! Anagwe, unyunyage unyunyage runci." Rugono rukinathira.*

**TAFSIRI YA HADITHI YA NNE**

**HADITHI YA CHURA NA MBUNI**

Wanyama wote walijumuika Pamoja. Wakakubaliana kila mnyama aje kuni. Wanyama wote wakabeba kuni. Naye chura akabeba kuni za mti wa 'muboru" .Akaenda huko. Wakachinja.Walipochinja wakaamua wachome nyama. Wakazichoma nyama wakaanza kuzila.

Chura akadharauliwa na Wanyama wote akaulizwa, "Nawe chura uso makalio umepeleka hizo kuni zako wapi?" Hatutakupatia nyama zetu.

Chura akasema, " Nitakaa hapa nione." Chura akakaa hapo. Wanyama wakachoma nyama. Wakaanza kula. Wakala. Wakashiba. Wakaanza kupachika vijiti kwenye nyama zingine kutokana na shibe.

Chura naye hakupewa akaambiwa, "Chura aso na makalio amekuja hapa kufanya nini?"Chura akakasilika. Akawauliza, " Hivi, mnaponiambia hivyo mtatoa wapi maji ya kunywa?" "Tutakunywa mtoni." "Na nikiikausha?" "Kwani utakausha mito yote?" "Na hivyo mimi nitaenda nikaushe mito, nanyi hamtapata ya kunywa. Nione iwapo nyama hizo zenu zitamfaa bila kuyanywa maji.

Wanyama wale wakaanza kumcheka chura wakimwambia, "ata ukaushe, utakausha yote. Tutayanywa maji. Huwezi kuikausha mito yote. Nenda uikaushe basi."

Chura akaondoka hapo akiwa amekasilika sana kwa kuwa alinyimwa nyama kama mzaha. Akaenda akakausha mito yote. Akabakiza mto mmoja wenye maji kiasi kidogo sana, maji yaliyokuwa na ndongo.

Wanyama walienda katika mito yote kutafuta maji wakakosa. Walikuwa wamekabwa na kiu hata wakajuta kuzila nyama zile. Nusura wafe kutokana na kiu. Walipata maji yale yenye dongo, hayakunyweka.

Fisi mmoja akamwambia, "chur ayu hapa. Tumbembeleze mno, tumpe nyama ili tusife kiu." Wakaanza kumuita chura. Chura akatokea. "Tafadhali hatutakunyima nyama tena. Tu karibu kufa kama ulivyotuambia. Tupe maji nasi tukupe nyama. Kwa kuwa tumeshindwa kuyanywa haya.

Mnyama mmoja kwa jina mbuni akasema, "mimi sitayanywa maji ya chura. Na nyama zangu sitampatia." Wanyama hao wengine wote wakaanza kumpa chura.
Chura akala akashiba. Alipewa nyama na Wanyama wote isipokuwa mbuni.

Mbuni alibembelezwa na Wanyama hao wengine akaambiwa, "Mbuni mpe chura nyama. Utakufa kiu." "Nani? Mimi sitayanywa maji anayooga chura tena yenye nongo. Sitayanywa. Hata mkipewa maji nyie mtayanywa. Mie sitayanywa wala kumpa chura nyama.

Chura akaapa kumwadhibu mbuni iwapoangeyanywa. Mbuni alikuwa na mpango wa kunywa maji na nyama asipeane. Alipoona kama chura hamuoni, akainama akapiga tundu la maji. Chura akaokota jiwe, akampiga upembe ikang'oka.Mbuni akalejesha upembe tena . Akakasilika.Akaenda kwake. Akamwambia cura, "nawe chura kwa vile umenigonga umening'oa upembe, utanirejeshea kwa vizibo saba vya mafuta ya karafuu." Chura akaachiwa lahana na mbuni. Vikembe vya chura vikaanza kufa. Chura naye akaanza kufura miguu. Chura akafahamu kuywa lahana ya mbuni ilikuwa

imemfika. Akasema, “Sasa nitaenda nikiulizia aishiko mbuni nikiwa na vizibo saba vya mafuta ya karafuu.”

Chura alikata vijiti vya karafuu na kutia yale mafuta humo. Akaunganisha hadi vikafika saba.

Akaanza safari. Alipokutana na Wanyama njiani akaimba. Muthunthuri muthunthuiga, kwa mbuni ni wapi? Muthunthuiga, nipeleke vyombo vya mbuni, muthunthuiga wanangu wamekwisha , muthunthuiga, wameugua baridi na homa ya malaria, muthunthuiga.

Fisi akamwambia , “waona kule, ng’ambo ile, ndiko kwa mbuni.” Chura akaendelea na safari. Akakutana na swala na paa akawambia, “Muthunthuri….”

Akakutana na fisi tena akaimba, “muthunthuri…..” Akaambiwa, “kwa mbuni ni pale. Mbuni alikuwa humo ndani.Chura akaimba, “muthunthuri….”

Mbuni alinyamaza kwanza. Alikuwa amekasirika na chura.Chura akauliza, “kwa kuwa niliambiwa hap ani kwa mbuni huenda ananinyamazia au nini? Nitaimba tena.”

Chura akaimba, “muthunthuri….” Mbuni akatoka. Akamuliza, “umekuja kwangu kufanyani na tulikosana?”

## HADITHI YA TANO
## NJOGU NA MBITI

*Njogu na mbiti ni ciatumite urata. Cierana, riu niilalage irimani rimwe. Ciatua kuraraga irimani rimwe. Njogu yari na twana twayo na mbiti yari na twana twayo.*

*Riu, ciekara muno muno muno ikilalaga ilimani rimwe. Ciikarite muno, ntuku imwe njogu niyerire mbiti nuntu numendanite muno, “Ntigirwa na ciana. Nthii bantu nkwenda kuthii.”Mbiti yamira, “nibu.”*

*Njogu yathii. Guntu kuraca. Guntu ku njogu i mingi muno ciekaraga. Riu ri yathiire, yathii yambiriria gwikarania na njogu, itacoka. Yaandika, “Riu nuntu ciana ciina mbiti n ani murata wakwa ri, ngaciithira wabo. Niiricage na twana twa mbiti.”*

*Riu njogu yekara njoguni. Yekara yekara yekara yekara itikwinuka nabo ikalala nabo. Riu riria mbiti nayo yatigirwe twana, wa kibwai giakinya, kaana ka mbiti gakambililia kulila. Gakauga , “m..m..m..m..!” mbiti igakauria, “ Ni indu ukulilila?” Gakauga, “ Ni rutende rwa njogu nkulilila.” Gakerwa, “kutha na utigakuthe wica.”*

*(Kuthu! Kaanaka njogu gakaliwa ni twana twa mbiti gakathira.) ikaathi kuria wega muno. Kibwai giakinya, kana ka mbiti kau kangi gakauga, “m..m..m..m!” Ni indu ukulilila?” “Ni rutende rwa njogu nkulilila.” “Kutha na utigakuthe wica.” (kuthu! Aya! Kau gakiliwa.)Ikithii kuria ruyuni. Igitinda githakani. Ikinuka kibwai, “m..m..m..m..!” “Ni indu ukulilila?” “Ni rutende rwa njogu nkulilila .” “kutha na utigakuthe wica.” Kuthu! Kau gagikua gakiliwa ni twana twa mbiti.*

*Ikithii kuria ringi kibwai giakinya, “m..m..m..m..!” “Ni indu ukulilila?” “Ni rutende rwa njogu nkulilila.” “Kutha na utigakuthe wica.” Kau kana ka njogu gakiliwa ni twana twa mbiti.*

*Riu, kaana ga kari na nthoongo, kona matigara mari mairi. Kandika riu, “gatuthii tutigare na ciana ino, indi untu twathii kuria, nuntu ninkumenya narega kuriwa, nig aka kangi gakaliwa nuntu turi mairi, na tucioke tuthire, niu nintoroka, ngacerie ku maitu ekaraga. Na tukathii kuria wega muno kithakani, indi niu, nkaricaga ni kuraja muno. Ikinuka, tinicuma thuuba. Riu gaka gakinya kariwa, niu, maganceria mbure. Metere minuka, timinunka.”*

*Kana karia ka nthongo kabanga ugu. Ciathi kuria. Kibwai gigikinya ri, cionthe ciice ciinukite cionthe ri, cienuka ciici kari wabo. Karia nako gatinda kuthii. Cienuka,*

*ciathii. Kana karia na kathii karira, " m…m..m…m…!" "ni indu ukulilila?" "Ni rutende rwa njogu nkulilila." "kutha na utigakuthe wica." Kaana karia kaliwa.*

*Riu mamenya karia nika gatikenuku, nigaguca. Kau gakuriwa. Kau nako kandika, "riu nikuthii gutigocoka." Ri cienukire nako kambiriria kuthii riu. Kathii kathii kathii kathii.*

*Gatungana na mbiti kaina, "mbiti mukuria guku, mukuria guku, mwanamwonera njogu ya cianyaga yatutigire nyomba na mbiti, kana ka mbiti gakauga m…m….m…m…, gakaurua ni indu ukulilila, gakauga ni rutende rwa njogu nkuririra, kutha na utigakuthe wica, kuthu!"*

*Kaana karia gakithii gakithii gagitungana na njogu. "njogu mukuria guku ……wica." Mbiti ciakera, "nukwona kuria rugongo ruria? Niku njogu ya cianyaga ikaraga."*

*Kaana kathii kathii kathii kathii …. Kethira nthuni. "Nthuni mukuria guku ……kuthu?" Kerwa, "weu nuthii kuria, niku nyukwe ekaraga."*

*Kathii kathii kathii….. kethiria guntu nthia ikuria. Kaina, "Nthia…kuthu!" kerwa nukwona kuria niku nyukwe ekaraga."*

*Kathii kathii kathii….. riu kari bakubi gukinya. Kathii kethiria njogu iti mingi bantu. Kaina, "njogu…….kuthu!"*

*"Aii! Njogu ya cianyaga iiria. Cuthiriria ino. Nikwona njogu ino mingi muno ukwona baba, ino, wana nika ukinyire, nugendaga banini, ukinakinya. Baaria nibo nyukwe ekaraga. Njogu ya cianyaga nitumwene.njogu ya cianyaga u uru baria. Nukwonaa njogu inu cionthe? Njogu wa cianyaga uri bo."*

*Kaana gakena!kamenya riu nkwambiriria guciona. Kathi, kathii ri, gakinakinya bo. Gakinya bo ri, gatikumenya ng'ina ni iriku nuntu njogu ni nyingi. Kona ngatethua ni kwina. Kaina, "njogu…..kuthu!"*

*Njogu ino ciingi gutibu ikwigua nwa ka ikuria. Ng'ina ikinegua ta njogu ya cianyaga ikugwetwa. Akinaciira atiri, "takirani ii, ki ii, tuthikiririeni kuri gauntu negua. " Njogu ciakira ki!*

*Kna karia kmbiriria rwimbo, "njogu….. kuthu!"N jogu ikinathi baria kana kayo kari. Yakauria, "Ai natia ukuuga? Na mwaca nau guku kuunthe kuraca u?"*

*"Tiga kumburia i, amba umonkie." "Ari taina ogu ukwinaga." "Ari ntikwinira bu ringi i, utiambite kumonkia."*

*Njogu ya cianyaga yekara nthii yonkia kana, kabaa. Yakera, " mbira riu."*

*Kaana kaamira "Nukumenya, ri watutigire nyomba ya mbiti, twathii kuria na ciana cia mbiti, tukinuka kibwai, kaana ka mbiti gakambiririe kurira gakiugaga m…m…m…, karira mbiti ikauria "Nimbi ukuririra?" kaana kauga, "Ni rutende rwa njogu nkuririra." Gakinerwa "Kutha na utigakuthe wica." Kaana gaku gakikua, gakiriwa gakithira, riu wa ntuku cionthe. Riu nikandiciririe muno namenya kau kangi niko gakuthii kariwe, nani nkariwa ruyu. Ndona riu, ninthii na kithaka. Natunga mbiti nicinire bu. Natunga njogu niciniire.*

*Riu naca nkinaga ugu ukwigucaga nkiina, nirio nonua nkinya baria uri."*

*"Auuuu! Tituthii! Tuthii tukonane na mbiti." "Ari, niu ntikinya nau ringi. Nkariwa ni mbiti ugu twana twetu turaririrwe.*

*"Ari Tuthii." " Aari, niu guntu mbiti iri, ntikinyikia i, nintigwa naa njogu iri." "Ari, tuthii."*

*Kaana karumirira ng'ina. Ciathii ciathii ciathii… Ciakinya kibwai. Nuntu ni kuraca. Ciakinya kibwai ciathii, nuntu ni kibwai ri, njogu nikwona twana twa mbiti.*

*"Ambu Njogu ciana ciakwa ri, ciiku?"*

*"Niciicite, kaikuria." Mekara mekara mekara.*

*"Mbiti, ciana ciakwa ciiku?"*

*“Nimacite. Tia cu. Mari nau kithakani i, indi nimacite.”*
*Njogu yekara yekara yekara. Yona gutukire, kwabetukania.*
*“Ntigukuria mbiti, ciana cia ri, ciiku?”*
*“Nimacite metaetarere.” Mbiti ni ciana ciakwa nkwenda n aguti gwetaeterera ringi. Guti mwana unkigua ari kithakani thaa ino. Cionthe niciinukire. Ga ciaku ciinukire ciakwa ciatigwa ku?| |Wegua nukwenda wega, ciana ciakwa lete.”*
*Mbiti yakira. Mbiti yambatwa. Yakinyithanua ni njogu yakua. Twana twambatwa. Twakinyithanua twakua. Rugono rukinathira.*

## TAFSIRI YA HADITHI YA TANO
## HADITHI YA FISI NA TEMBO

Tembo na fisi walikua marafiki. Wakaafikiana wawe wakilala katika pango moja. Tembo alikua na wanawe na fisi vivyo hivyo. Wakaishi kwa muda mrefu kwa lile pango moja.

Walikua marafiki wa kufa kuzikana. Siku moja, tembo akamwambia fisi, “baki na wanangu niende mahali Fulani.” Fisi akakubali. Tembo akaenda mahali, huko mbali walikoishi tembo wengine wengi.

Tembo alipoenda, alianza kuishi na tembo wengine. Hakurudi. Alijiambia, “maadamu wanangu wako mikononi mwa fisi ambaye ni sahibu yangu nitawapata nikirejea. Watakua wakila Pamoja na wana wa fisi.” Aliishi na tembo wengine siku ayami bila kurejea pangoni.

Kila jioni, kikembe cha fisi kingeanza kulia na kusema, “m…m…m…m… ninalilia mwana wa ndovu.” Fisi angemwambia, “ng’ata ila usimg’ate kwa nguvu.” Papo hapo, mwanatembo angeliwa bila kusazwa na vikembe vya fisi.

Mchana, walishinda vizuri wakila pale malishoni. Kila magharibi waliporejea pangoni, mwanafisi angelia ili aruhusiwe kumla mtoto wa ndovu. Wakazoea kufanya hivyo kila uchao.

Mwandovu aliyekuwa na chongo akatanabahi kuwa wamebaki wawili tu. Akasema, “tutaenda malishoni kula na wana wa fisi. Lakini, kwa kuwa sijui iwapo ni mie au ndugu yangu ataliwa na fisi nitatoroka. Sitasubiri tuliwe sote. Nitaenda kumsaka mama aishiko. Nitakua nikila mbali na fisi pale kichakani. Sitawafuata wakirejea pangoni. watamla ndugu yangu ila mimi watanifuata wanikose. “akaamua.

Wakaenda malishoni kama ilivyokuwa mazoea. Yule chongo akasafiri mchana kutwa. Ndugu yake akarejea pangoni na kuliwa na wana wa fisi. Fisi na wanawe walidhani kwamba yule chongo angerudi. Lakini alikua ameapa, “sasa ni kwenda bila kuangallia nyuma.”

Akasafiri hadi akakutana na fisi. Akaimba:

fisi mnaokula huku, mnaokula huku,
mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Mwanatembo huyo alisafiri hadi akakutana na ndovu. Akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?

Akasema nalilia mwana yembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Ndovu wakamwambia ?Unaona kule ng’ambo ile, ndiko aishiko ndovu wa Cianyaga.”
Akasafiri hadi alipokutana nap aa. Akaimba

Paa mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Akaambiwa , “unaona kule, ndiko aishiko mama yako.”
Akaendelea na safari. Akakutana na swara wakiwa malishoni. Akaimba:

Swara mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana tembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Akaambiwa, “kule ndiko anakoishi mamaku.”
Alipokuwa karibu kufika, aliwaona ndovu wachache pahali. Akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Wakamwambia, “Ndovu wa Cianyaga ndiye yule. Angalia. Pale palipo na ndovu wengi. Ushafika. Tembea kidogo tu. Hapo ndipo mama yako huishi. Utampata.” Yule chongo akafurahi mno alipowaona hao tembo.
Alipofika pale lakini hakuweza kumtambua mama yake miongoni mwa wale ndovu wengi. Akaona wimbo ungemsaidia akaimba:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?
Akasema nalilia mwana yembo.
Ng’ata ila using’ate kwa nguvu.

Ndovu hao wengine hawakuwa na mwao na kile kilichokuwa kikiendelea. Waliendelea kula tu. Mama yake akaskia ni kama alikuwa akiitwa. Akawaambia wenzake, “Ebu nyamazeni. Tusikilize. Kuna jambo nimeskikia.” Ndovu wakanyamaza ji!
Yule mwanandovu akaanza wimbo:

Ndovu mnaokula huku, mnaokula huku,
Mumemwona tembo aitwaye cianyaga?
Alituacha katika nyumba ya fisi.
Mwanafisi akasema,m…m…m…m…
Akaulizwa nini kinachokuliza?

Akasema nalilia mwana yembo.
Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.

Mama akaenda pale alipokuwa mwanawe. Akamwuliza, "Eti unasemaje? Mmekuja nan ani huku mbali hivi?" "Usiniulize. Ninyonyeshe kwanza."

"Ebu imba hivyo ulivyoimba."

"Sitaimba tena hadi utakaponinyonyesha."

Mama yule akaketi chini na kunyonyesha mwaanawe. Mwanandovu akashiba . Mamake akamwambia, "Niambie sasa" Mwanawe akamwambia, "Wajua ulipotuacha katika nyumba ya fisi, mmoja wa hao wana angelia. Mamake angemwambia ale mmoja wetu. Hivyo ndivyo wanao walianza kuliwa. Kila siku. Nilifikiria mno nikamaizi mwenzangu angeliwa leo nami kesho. Nikaamua kufunga safari nikutafute kwa kuimba hadi nifike ulipo."

"Mawe! Twende nikakabiliana na fisi." La mimi sitafika huko tena. Nitaliwa na fisi kama ndugu zangu walivyoliwa." "hapana twende." "La. Kwiko na fisi siendi. Nitabaki huku waliko ndovu wengine." "La. Twende."

Mwanandovu akamfuata mama yake wakafika huko machweo kwa kuwa kulikuwa mbali. Ndovu akawaona wana wa fisi. "Kwani wanangu wako wapi?" "Wanakuja wanakula."

"Wanakuja. Hawajarejea. Wako malishoni lakini wanakuja."

Ndovu alisubiri hadi usiku. "Fisi, niambie waliko wanangu." "Subiri kidogo wanakuja."

"Ninataka wanangu. Sitasubiri tena. Hakuna mwana awezaye kuwa kichakani wakati huu. Wote washarejea. Nipe wanangu kabla ya mambo kwenda mrama."

Fisi akanyamaza. Akashikwa na tembo. Akakanyangwa akafa. Wanawe wakashikwa. Wakakanyangwa wakafa.

Hadithi imekamilika hapo.

**Kiambatisho II: Barua Ya Utangulizi**

Rebecah Wanja Kirimi,

S.L.P 128-60400

Chuka.

KWA BW/BI

**KUH: KUOMBA NAFASI YA UKUSANYAJI WA DATA YA UTAFITI KWA WAKUU WA TARAFA YA CHUKA**

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Kiswahili ambaye anahitajika kufanya utafiti wa nyanjani ili kukidhi mahitaji ya kozi hii. Utafiti huu ni wa fasihi simulizi ya inayotambulika kama ngano. Washiriki wakuu wa ni watambaji maarufu katika jamii ya Wachuka. Mtafiti anaomba kuwashirikisha watambaji hao kutoka vijiji mbalimbali ili kufanikiwa kukamilisha mradi wake wa utafiti. Data itakayokusanywa itatumika katika uchambuzi wa kifasihi wa utafiti huu wala sio kwa matumizi mengine nje ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu ya yatawasilishwa kwenu yakihitjajika pindi utafiti utakapokamilika.

Asante.

Wako mwaminifu,

Rebecah kirimi

**Kiambatisho III: Barua Ya Idhini Ya Kamati Ya Maadili Ya Chuo Kikuu Cha Chuka**

**CHUKA UNIVERSITY**

Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali

**CHUKA UNIVERSITY INSTITUTIONAL ETHICS REVIEW COMMITTEE**


Telephones: 020-2310512/18
Direct Line: 0772894438
Email: info@chuka.ac.ke,
P. O. Box 109-60400, Chuka
Website: www.chuka.ac.ke


**REF: CUIERC/ NACOSTI/329**

TO: Rebecca Wanja Kirimi

**17th January, 2023**

**RE: Mwega Wa Ujumi Katika Ngano Simulizi Za Wachuka**

This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812.* The approval period is 17th January, 2023 – 17th January, 2024.

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used

ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC.*

iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification

iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours

v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.

vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.

vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC.*

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://oris.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

**Dr. Benjamin Kanga**
**SECRETARY**

*Chuka University is....... ...Inspiring Environmental Sustainability for Better Life*

## Kiambatisho IV: Idhini Ya Utafiti

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **556453**

Date of Issue: **28/January/2023**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. Rebecah Wanja Kirimi of Chuka University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Tharaka-Nithi on the topic: MWEGA WA UJUMI KATIKA NGANO SIMULIZI ZA WACHUKA for the period ending : 28/January/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/23403**

**556453**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commission for Science, Technology and Innovation -